# Nipashe

Jumatano Januari 8, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580122

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710




## Mpango azionya taasisi za fedha kwa kutoza riba kubwa mikopo

UKURASA 22


TUJIKUMBUSHE

Ukurasa 15

M/kiti Chadema Kusini aanika mwelekeo wao joto la uchaguzi

Bobi Wine sasa 'ingizo jipya' kumkabili Museveni 2021

Ukurasa 18

siasa

JUMATANO JANUARI 8, 2020

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

Ukurasa 19

Uchaguzi 2020 watangaza nia urais Democratic wapukutika?

UCHAMBUZI

Jenerali Soleimani: Kamanda aliyeinyima usingizi Marekani

Na Anil Kija

MAREKANI imevuka mpaka katika ushindani wake na Iran kudhibiti Mashariki ya Kati, kutokana na mauaji ya Jenerali Qassem Soleimani (62). Huyo ni mkuu wa vikosi maalum vya Al Quds, vinavyoendesha mapambano Iran inayosimamia eneo lote la Mashariki ya Kati.

Jenerali Soleimani aliuawa katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Baghdad akiwa njiani aliposhuka kwenye ndege, asubuhi ya Ijumaa Januari 3.

Makao Makuu ya Jeshi la Marekani yalisema kuwa Rais Donald Trump aliamuru 'kuchukua hatua za kujilinda na kuwalinda raia wa Marekani nchi za nje kwa kumuua' mtu ambaye kiongozi mkuu wa Iran, Ayatollah Ali

INAENDELEA UK.16

Ukurasa 14

Kenya mchuano ufisadi, 'wajenga madaraja' vs Uhuru, Raila, Ruto

Jenerali Qassem Soleimani. PICHA: MTANDAO

Vita ukatili jinsia kupitia moto aliyowasha Majaliwa Ukurasa 20

UKURASA 13

# Mbaroni tuhuma kujifanya maofisa Usalama wa Taifa

**WADAIWA** kujieleza kuwa wanatoka Ikulu, wakutwa na 'ambulance', bastola na vifaa vya kiusalama...*Endelea ukurasa wa 2*



Watuhumiwa saba waliokamatwa na Jeshi la Polisi mkoani Mwanza, kwa tuhuma za kujifanya maofisa wa Idara ya Usalama wa Taifa, kutoka Ikulu, wakiwa chini ya ulinzi katika makao ya jeshi hilo, jijini humo, jana. PICHA NDOGO: Kamanda wa Polisi wa mkoa huo, Murilo Jumanne akionyesha kwa waandishi wa habari gari aina ya Toyota Ambulance lenye namba za usajili T 751 NBL, lililokuwa linatumiwa na watuhumiwa hao, pamoja na 'business cards', vitambulisho, bastola, risasi 20, redio 'call' na kifaa cha kukagulia watu. **PICHA: ROSE JACOB**

## YALIYOMO


**UKURASA WA 3**

**MATOKEO YA UCHAGUZI MKUU 2020 KUTANGAZWA DODOMA**

MKURUGENZI wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Dk. Wilson Mahera, amesema tume hiyo inatarajia...

**UKURASA WA 7**

**WADAIWA WA NIC WAANZA KULIPA MADENI**

SHIRIKA la Bima la Taifa (NIC), limesema kuwa wadaiwa wake wameanza kulipa madeni yao na kwa sasa yamebakia...


## KIGOGO CHADEMA ATISHIA KUJIUZULU

UKURASA 3






## Mwanafunzi chuo kikuu ahukumiwa kwa kumuhonga ofisa wa mitihani

UKURASA 2


**MICHEZO** MKWASA, KAHATA WANG'ARA DESEMBA UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA

# 7 mbaroni tuhuma kujifanya maofisa usalama wa Ikulu

**Na Rose Jacob, MWANZA**

WATU saba wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Mwanza, kwa tuhuma za kujifanya maofisa usalama wa Ikulu na kuwatapeli wananchi na watumishi wa serikali.

Imedaiwa kuwa watu hao walikuwa wanajifanya wako katika kazi maalumu, wakiingilia misafara ya viongozi wakuu wa nchi kwa lengo la kuiaminisha jamii kuwa ni watumishi wa taasisi hiyo nyeti na kujenga mazingira ya kupewa rushwa.

Akizungumzia tukio hilo jana, Kamanda wa Polisi mkoani Mwanza, Muliro Jumanne, alidai watuhumiwa hao wamefanya matukio kati ya Desemba 27, mwaka jana na Januari 2 mwaka huu, wakitumia gari lenye namba za usajili T. 751 BNL aina ya Toyota Ambulance, ambalo walidai ni sehemu ya msafara wa viongozi wakuu wa wamechelewa kuwahi kwenye msafara.

"Watuhumiwa hao saba walikamatwa na makachelo na waliendelea kujitambulisha kuwa wao ni maofisa wa usalama wa taifa kutoka Ikulu, lakini walipohojiwa kwa kina, ilibainika ni matapeli wenye lengo la kuwababaisha wananchi kwa manufaa yao binafsi," alidai.

Murilo aliyataja majina ya watuhumiwa hao kuwa ni Chalanga Wiliamu (45), mkazi wa Pasians, Mwanza na Arusha, Hamis Seleman (25), ni fundi magari, Philipo Petro (35), mkazi wa Usagara wilayani Misungwi, Elia Vicent (30), aliyedaiwa Mchungaji wa Kanisa la EAGT Kisesa na mkazi wa Kisesa, Hassan Juma (29), mkazi wa Mkolani na fundi wa IT, Selemani Joramu (25), mlinzi wa Chalanga na Michael Mazige, mkazi wa Morogoro.

INAENDELEA UK 8



Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, akiteta jambo na mtuhumiwa Tito Magoti, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mwanafunzi chuo kikuu hatiani kumuhonga ofisa wa mitihani

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

MWANAFUNZI wa Chuo Kikuu cha St. John's, James Gebu (27), ametiwa hatiani na kuhukumiwa kwenda jela kwa miaka mitatu au kulipa faini ya Sh. 500,000, kwa kosa la kujaribu kutoa rushwa ya Sh. 900,000 za wanafunzi wenzake kwa ofisa mitihani wa chuo hicho, ili awaongezee ufaulu katika GPA.

Adhabu hiyo ilitolewa jana na Mahakama ya Wilaya ya Dodoma, kutokana na mshtakiwa huyo kukiri kosa hilo, baada ya kusomewa kosa lake na mwendesha mashtaka wa Takukuru.

Baada ya kusomewa kosa hilo na Mwendesha Mashtaka wa Takukuru, Biswaro Biswaro, mwanafunzi huyo alikiri kosa hilo ndipo Hakimu wa Wilaya, David Msalilwa, alipomhukumu kwenda jela miaka mitatu au kulipa faini ya kiasi hicho cha fedha.

Hata hivyo, Gebu alikwepa kwenda jela kwa kulipa Sh. 500,000, hivyo kuachiwa huru.

Awali jana, Takukuru mkoani Dodoma ilisema inamshikilia Gebu, mkazi wa Dodoma kwa kosa hilo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema kosa hilo ni kinyume cha Kifungu cha Sheria cha 15 (1) cha Sheria ya Kupambana na Rushwa sura ya 329 marejeo ya 2018.

Kibwengo alisema mwanafunzi huyo wa shahada ya kwanza ya ualimu, na kwamba wenzake sita wanaendelea kuchunguzwa. Aliongeza kwamba mtuhumiwa huyo angefikishwa mahakamani wakati wowote.

INAENDELEA UK 8


## VACANCIES

The following Vacancies are existing at T.M.J. Hospital Ltd

| | |
|---|---|
| 1. DERMATOLOGIST | 1 POST (Minimum 2 Years Experience) |
| 2. OPTHALMOLOGIST | 1 POST (Minimum 2 Years Experience) |
| 3. RADIOLOGIST | 1 POST (Minimum 2 Years Experience) |
| 4. NURSING OFFICERS | 2 POSTS (Minimum 2 Years Experience) |
| 5. ENROLLED NURSES | 2 POSTS (Minimum 2 Years Experience) |
| 6. NURSING ASSISTANTS | 2 POSTS (Minimum 2 Years Experience) |
| 7. DIALYSIS TECHNICIANS | 2 POSTS (Minimum 5 Years Experience) |

APPLY TO:
C.E.O,
T.M.J. HOSPITAL LTD
P. O. BOX: 20439
MWAI KIBAKI ROAD, MIKOCHENI, DAR ES SALAAM.
e-mail: director@tmjhospital.co.tz

215575902


# ACT yashtukia uandikishaji wapigakura

**Na Said Hamdani, LINDI**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imeombwa kutekeleza majukumu yake kwa uweledi zaidi, ikiwamo kuwapatia wananchi elimu na taarifa za kutosha.

Hayo yalielezwa na Chama cha ACT-Wazalendo, kikisema hatua hiyo itaifanya jamii ivutiwe na kuona umuhimu wa kujitokeza kujiandikisha kwenye daftari la kudumu la wapigakura kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo mkoani Lindi, Isihaka Rashidi Mchinjita, ndiye aliyesema hayo alipokuwa anazungumza na wanahabari.

Alisema chama hicho kimelazimika kuwasilisha ombi hilo kwa NEC, baada ya kutilia shaka zoezi la uandikishaji kwenye daftari la kudumu la wapigakura kwa mkoa wa Lindi, kama lina dhamira ya kweli.

"Zoezi la uandikishaji wapigakura kwa mkoa wetu wa Lindi, limekuja katika utaratibu ule ule unaotia shaka kama kweli ipo dhamira ya kuandikisha wapigakura," alisema Mchinjita.

Mchinjita ametaja mambo ambayo yanampa shaka ni ufikishaji wa taarifa kwa wananchi izingatiwa kuwapo kwa zuio kwa baadhi ya vyama vya siasa kutokutana na wananchi kwa kutofanya mikutano ya hadhara, muda mdogo wa uandikishaji na utoaji elimu kwa jamii.

Alisema kitendo cha serikali kuzuia mikutano ya hadhara kwa baadhi ya vyama vya siasa na asasi za kiraia kutokuwa huru kupita utoaji elimu ya mpigakura na mabadiliko ya sheria ya vyama vya siasa, ni miongoni mwa vikwazo kwa jamii kukosa taarifa.

Aliwaomba wananchi bila kujali itikadi zao za vyama, dini, rangi au kabila kujitokeza kwa wingi Januari 12, mwaka huu wakati daftari la kudumu la wapigakura litakapoanza kuboreshwa ili kutekeleza matakwa ya kisheria kuchagua viongozi wanaowahitaji kuwaongoza.

Uboreshaji daftari la kudumu la wapigakura kwa mikoa ya Lindi na Mtwara, unatarajiwa kufanyika kwa wiki moja, kuanzia Januari 12 hadi 18, mwaka huu.

## Matokeo ya uchaguzi mkuu 2020 kutangazwa Dodoma

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

MKURUGENZI wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Dk. Wilson Mahera, amesema tume hiyo inatarajia kutangaza matokeo ya uchaguzi mkuu mwaka huu kutokea makao makuu Dodoma.

Dk. Mahera aliyasema hayo jana baada ya kufanya ziara kukagua maendeleo ya ujenzi wa ofisi za tume hizo zilizoko eneo la Njedengwa jijini hapa.

Mkurugenzi huyo alisema tume inakusudia kuhamia rasmi makao makuu ya serikali Dodoma na wanategemea matokeo ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu yatangazwa kutoka eneo hilo.

"Kama tunavyojua, mwaka huu wa 2020 ni mwaka wa uchaguzi mkuu, hivyo tunatarajia mambo yote yatafanyikia hapahapa kwenye jengo letu jijini Dodoma," alisema.

Hata hivyo, alisema lengo la ziara hiyo ambayo aliambatana na Mwenyekiti wa NEC, Jaji mstaafu, Semistocles Kaijage, ni kukagua maendeleo ya ujenzi unaotekelezwa na Suma JKT.

Alibainisha kuwa ofisi hiyo ilisitisha mkataba na mkandarasi wa kwanza ambaye ni Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kutokana na kushindwa kukamilisha kazi hiyo kwa wakati.

"Mkandarasi wa kwanza alikuwa TBA, baada ya kushindwa kukamilisha kwa wakati tuliona kuingia mkataba na Suma JKT na kuweka utaratibu wa kuandaa michoro upya kwa sababu michoro ilikuwa imekosewa sana," alisema.

Alisema ujenzi huo ulianza Julai 2017 na ulitakiwa ukamilike Juni 2018 kwa gharama ya Sh. bilioni 13, lakini mkandarasi huyo aliongeza gharama hadi Sh. bilioni 32. Hata hivyo, mradi huo bado haujakamilika na ujenzi wake ulisimama.

Alisema kwa sasa kazi hiyo inaendelea kufanyika kwa ushirikiano kati ya Chuo Kikuu cha Ardhi na Suma JKT na maendeleo yake yanaenda kwa kasi kubwa, hivyo matarajio ya tume ni ikamilike kufikia Aprili mwaka huu.

Dk. Mahera alitaja sababu za kuwa na imani ya ofisi hizo kukamilika kwa wakati kuwa ni mikakati ya Suma JKT kuweka vijana wengi kwenye eneo mradi wa ujenzi na tume imeshalipa malipo ya awali kwa ajili ya kazi hiyo.

Mkurugenzi huyo alisema Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Brigedia Jenerali Charles Mbuge, alimhakikishia kuwa ifikapo Aprili mwaka huu, mradi huo utakuwa umefikia hatua nzuri.

Alisema ujenzi wa mradi huo utakuwa na mjengo matatu ambayo ni sehemu ya ghala, jengo la kutangazia matokeo ya kitaifa na jengo litakalotumika kama ofisi.

# Kigogo Chadema atishia kujiuzulu

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

KIGOGO mmoja wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) Mkoa wa Kilimanjaro, ametishia kujiuzulu wadhifa wake, ikiwa kamati kuu ya chama hicho itarudisha majina ya wagombea ubunge katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu ambao hawakufanya kazi majimboni, akiwaita ni virusi.

Aliyeapa kutokubaliana na wagombea ubunge walioshindwa kutekeleza sera ya Chadema ni Msingi majimboni mwao ni Mwenyekiti wa chama hicho mkoa wa Kilimanjaro, Michael Kilawila.

Kilawila alitangaza vita hiyo jana mjini Moshi, wakati akifungua kikao kazi cha kimkakati cha Baraza la Wanawake Mkoa wa Kilimanjaro (Bawacha), ulioitishwa na Mbunge na Mjumbe wa Kamati Kuu, Grace Kiwelu.

"Sasa tunapojiandaa kwenda kwenye uchaguzi mkuu mwaka huu, kila mtu kwenye mkoa huu atakula alikopeleka mboga. Sijui kama mnanielewa, yaani wewe unataka kuwa mbunge utatuonyesha kazi uliyofanya, niko tayari kujiuzulu nafasi yangu ya mkoa kuliko kuletewa virusi ambavyo havikufanya kazi.

"Tumeelewana eeh, yaani wewe mwenzako akaanzishe Chadema ni Msingi, akalale nje ya ndoa yake siku tatu, nne au mwezi, halafu mtu mwingine aje na senti zake kwa sababu tu amebarikiwa kuwa na senti, anataka umwidhinishe kuwa mgombea wa nafasi fulani ndani ya chama.

"Hiyo haitakaa itokee na Mungu apitishe mbali. Sasa hivi sitaangalia sura na bahati mbaya au nzuri, niwaambie katiba yetu imebadilishwa, yaani muziki unaanzia hapo. Katiba yetu imebadilishwa na sio kule wanapitisha tena (kamati kuu) ni hapa hapa mkoani, tunanyoana hapa hapa."

Katika hotuba yake Kilawila aliwaeleza wajumbe hao wa Bawacha kuwa: "Hatutakuja kusema ooh fulani kaja katoka Marekani na ana hela, hizo hela zinamsaidia yeye, wanyonge wetu na uji wetu tutaendelea kubaki hapa, tumeelewana eeh. Kwa hiyo kafanyeni kazi, niwaombeni sana hilo mkalizingatie."

Alieleza kuwa katika watu wanaofanya vizuri sasa hivi ni Baraza la Wanawake wa Chadema na wanakwenda kwa spidi kubwa, lakini mabaraza mengine yamebaki nyuma, ingawa ana hakika kwa spidi hiyo na mikutano ya wanawake inayofanyika inakwenda kuamsha ari.

Kutokana na mwelekeo huo, Mwenyekiti huyo alisisitiza kuwa kuanzia Januari 22 mwaka huu Baraza la Uongozi la Mkoa linaanza ziara Jimbo la Same Mashariki.

"Tunakuja huko tuweke mikakati pamoja na somo litakalotolewa hapa leo, lakini tuweke mikakati ya pamoja ni namna gani tunakwenda. Tukitoka Same Mashariki, tutakuja Same Magharibi, tutakuja Mwanga, tutakwenda Rombo na tutakuja Vunjo, tutakuja Moshi Vijijini, Moshi Mjini, tutakwenda Hai na tutamalizia na Siha," alieleza Kilawila.

Awali, Mwenyekiti wa Bawacha Mkoa wa Kilimanjaro na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chadema, Grace Kiwelu, akitoa hotuba yake kuhusu mwelekeo wa mwaka wa uchaguzi (2020) kwa Baraza la Wanawake, alisema katika kufikia malengo ya ushindi ya Chadema, Bawacha Kilimanjaro itaboresha zoezi la Chadema ni msingi na kuhamasisha wanawake wengi kujisajili katika daftari la chama hicho.

"Tunataka kuwainua wanawake kwa kuwajengea uwezo wa kujitegemea kiuchumi ili kufikia azma ya kauli mbiu yetu ya maendeleo ni mwanamke. Tutaratibu mafunzo ya uongozi kwa wanawake na kuhamasisha wanawake wengi kugombea nafasi mbalimbali za uongozi," alisema Kiwelu.



# Uchunguzi anayedaiwa kujifanya ofisa wa Zimamoto wakamilika

**Na Juster Prudence**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), imesema imekamilisha uchunguzi dhidi ya mtuhumiwa aliyejifanya Ofisa wa Zimamoto aliyekamatwa katika nyumba ya kulala wageni Agosti mwaka jana wilayani Temeke, Mkoa wa Dar es Salaam.

Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Temeke, Donasian Kessy, alisema uchunguzi dhidi ya mtuhumiwa huyo umekamilika, hivyo atafikishwa mahakamani.

Kwa mujibu wa Kessy, mtuhumiwa atafunguliwa mashtaka mawili likiwamo kosa la kujifanya ofisa wa serikali kinyume cha kifungu cha sheria namba 100 kifungu kidogo B pamoja na kujipatia fedha kwa njia haramu kinyume cha kifungu cha sheria namba 302 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2002.

Alisema Takukuru inaendelea kutoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kupitia mitandao yote ya simu kwa kupiga au kutuma ujumbe mfupi wa maandishi kwa namba ya dharura 113.

Mtuhumiwa hiyo, Issa William, alikamatwa Agosti, 2019 baada ya kufika katika moja ya nyumba ya wageni Keko wilayani Temeke akiwa kama Ofisa wa Zimamoto na kuidai amefika kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa vifaa vya zimamoto na kulipwa Sh. 35,000 na zaidi ya Sh. milioni moja alizomwomba mmiliki wa nyumba hiyo ili amsaidie kufuta deni la miaka ya nyuma alilodai ni shilingi milioni tatu.



Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji Rufani (mst) Semistocles Kaijage (kushoto) na Mkurugenzi wa Uchaguzi wa NEC, Dk. Willson Mahera (wa tatu kushoto), wakiwa na maofisa wa Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT), walipotembelea eneo la Njedengwa jijini Dodoma jana, yanapojengwa makao makuu ya tume hiyo, kukagua maendeleo ya ujenzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# RC aagiza tathmini mishahara watumishi

**Na John Mapepele, SINGIDA**

MKUU wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, amesema kila mtumishi wa serikali katika mkoa wake kuanzia mwaka huu atatakiwa kuonyesha mafanikio yanayotokana na mishahara anayolipwa na serikali kupitia kaulimbiu maalum iliyoandaliwa na mkoa ya "mshahara wangu upo wapi".

Amesema tathmini hiyo itafanyaka mwisho wa mwaka huu, huku akionya watumishi kuhusu kujihusisha na mambo ya siasa, badala yake kufanya kazi kwa bidii ili kuunga mkono juhudi za serikali.

Akizungumza na watumishi wa mmma wa mkoa wa Singida katika mkutano maalum wa kwanza katika mwaka huu mjini Singida jana, Dk. Nchimbi alisema mkoa umeamua kuiishi kaulimbiu hiyo baada ya kuona mafanikio ya kupigiwa mfano yaliyopatikana kutoka kwa wanufaika wa mpango wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf).

Alisema katika mpango huo, ruzuku ya Sh. 20,000 ilitolewa kwenye kila kaya yenye sifa katika halmashauri sita kati ya saba za mkoa pamoja na fedha za masharti ya afya na elimu ambazo kila kaya yenye mtoto anayesoma shule ya msingi na sekondari na wale chini ya miaka tano, ilipewa kuanzia Sh. 2,000 hadi 6,000.

Alisema ruzuku hiyo imekuwa msaada mkubwa kwa kaya maskini katika kuwanunulia sare, madaftari na kulipia matibabu hasa kujiunga na Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii (NHIF).

Aliongeza kuwa hadi kufikia Januari mwaka huu, jumla ya kaya 38,136 kutoka katika vijiji 278 zimenufaika na ruzuku hiyo na jumla ya Sh. 37.9 ziliwafikia walengwa.

"Napenda kuwahakikishia kuwa hakuna kipindi ambacho watumishi wa umma watakuwa na maisha bora kama hiki cha serikali ya awamu ya tano, imeshaboresha kwenye kila sekta kama miundombinu, huduma za afya na elimu, itashindwaje kuboresha maisha ya watumishi umma?" Alihoji.

Dk. Nchimbi alisisitiza kuwa watumishi wazembe hawatavuka mwaka 2020 bila kuondolewa mara moja kupisha watumishi wanaoendana na kaulimbiu ya 'Hapa Kazi Tu'.

Alisema mbali na kuhakikisha kuwa mishashara ya watumishi inaleta tija kwenye familia na kuboresha uchumi, tayari mkoa unatekeleza mikakati mahsusi ya kilimo cha kisasa cha pamoja cha zao la korosho kwa wananchi wake.

Alitoa rai kwa watumishi na wananchi kujitokeza ili kupatiwa maeneo hayo ili kuyaendeleza kwa pamoja.

"Hadi sasa, Singida siyo maskini, kame wala yenye njaa kama iliyokuwa ikitafsiriwa na baadhi ya watu hapo awali. Tayari hekta 12,000 za kilimo cha pamoja (block farming), zimepandwa mikorosho na zimeanza kuzaa korosho katika Wilaya ya Manyoni.

"Ninatoa shukrani na pongezi zangu za dhati kwa Rais John Pombe Magufuli kwa kutupatia pikipiki 10 ili ziweze kusaidia katika kazi hii," alisifu.

Alisema utafiti uliofanyika hivi karibuni, umeonyesha ardhi ya mkoa huo ina ubora mkubwa wa kustawisha zao la korosho kwa muda mfupi kulinganisha na maeneo mengi nchini, hivyo hakuna sababu watumishi na wananchi kutochangamkia fursa hiyo adimu.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mary Mwanjelwa, ambaye yuko mkoani Singida kwa ziara ya kikazi ya siku nne kuazia jana, alitoa wito kwa waajiri na watumishi wa umma kuwasilisha taarifa sahihi kwa wakati kwenye ofisi yake ili zifanyiwe kazi katika kipindi kilichopangwa.

Alisema tatizo na vikwazo vingi vya watumishi kama malimbikizo ya mshahara, kulipwa mafao, kupanda madaraja, uhamisho na mafunzo vinatokana na uwasilishaji taarifa na kutozingatia muda sahihi wa kufanya hivyo.

Aliwataka maofisa utumishi kutokujifanya miungu watu na badala yake watimize wajibu wao wa kufanya kazi zao kwa weledi.

# Upelelezi wakwamisha kesi ofisa LHRC

**Na Hellen Mwango**

KESI inayomkabili Ofisa Elimu kwa Umma wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Tito Magoti (26) na Mtaalamu wa Tehama, Theodory Gyan (36), imepigwa kalenda mpaka Januari 21, mwaka huu, baada ya Upande wa Jamhuri kudai kuwa upelelezi bado haujakamilika.

Tito na mwenzake wanakabiliwa na mashtaka matatu ikiwamo kumiliki programu ya kompyuta iliyotengenezwa mahususi kufanya kosa la uhalifu na kutakatisha Sh. milioni 17.3.

Kesi hiyo ilitajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Janeth Mtega.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Mawakili wa Serikali Waandamizi Renatus Mkude na Wankyo Simon, ulidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa lakini Wankyo alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika aliomba tarehe ya kutajwa. Hata hivyo, upande wa utetezi uliomba kuharakishwa upelelezi huo.

Wankyo alidai kuwa washtakiwa wote, katika tarehe tofauti kati ya Februari Mosi na Desemba 17, mwaka jana, ndani ya Jiji la Dar es Salaam na mahali tofauti nchini Tanzania, kwa pamoja na watu ambao hawapo mahakamani kwa makusudi walishiriki kutenda makosa ya kiuhalifu ya kumiliki programu ya kompyuta iliyotengenezwa mahusus kufanya kosa la jinai na kuwawezesha kujipatia Sh. 17,354,535.

Nchimbi alidai katika tarehe tofauti kati ya Februari Mosi na Desemba 17 ndani ya jiji na mkoa wa Dar es Salaam, kwa pamoja na wengine ambao hawapo mahakamani, walimiliki programu ya kompyuta iliyotengenezwa mahusus kwa ajili ya kutenda makosa ya jinsi.

Mkude alidai katika shtaka la tatu kuwa kati ya Februari Mosi na Desemba 17, jijini Dar es Salaam, washtakiwa hao kwa pamoja walitakatisha na kujipatia Sh. 17,353,535 wakati wakijua mapato hayo yametokana na zao la kosa la kushiriki genge la uhalifu.

Washtakiwa hawakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo ya uhujumu uchumi mpaka ipate kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Mshataka (DPP) au upelelezi utakapokamilika itahamishiwa Mahakama Kuu Divisheni ya Uhujumu Uchumi na Rushwa.

TANGAZO

NICOL
The Economic Shield of the Nation

# NATIONAL INVESTMENTS PLC

# TAARIFA KWA WANAHISA

Taarifa hii inahusu habari iliyosambaa katika vyombo vya habari hivi karibuni ambayo inabainisha kwamba Mheshimiwa Luhaga Mpina (MB), Waziri wa Mifugo na Uvuvi, alitengua Mkataba wa Mauzo wa Mali za Machinjio ya Dodoma (Dodoma abattoir) ulioingiwa kati ya Wizara na Kampuni ya Uwekezaji ya Taifa (NICOL), ikisemekana kwamba NICOL imeshindwa kutekeleza baadhi ya masharti ya Mkataba huo. Zaidi ya hapo, Waziri amenukuliwa kwamba aliamuru Wizara ya Mifugo na Uvuvi ichukuwe mara moja mali zote za Kampuni ya Nyama, (Tanzania Meat Company Ltd. - TMCL) na vilevile akaagiza NICOL ilipe Wizara ya Mifugo na Uvuvi na TMCL jumla ya shilingi bilioni 15.

Kwa ufafanuzi, ieleweke kwamba mnamo mwaka 2008, baada ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuamua kusitisha uendeshaji wa shughuli za machinjio na kutangaza nia ya kuuza rasilimali za Dodoma Abattoir, ndipo tarehe 11 Septemba 2008, NICOL ilinunua mali hizo kwa kulipa Serikalini shilingi bilioni 1.3 fedha taslim, kiasi ambacho baadaye kilichukuliwa kama ni asilimia 51% ya mchango wa ubia kati yake na Serikali katika kampuni ya TMCL, na Serikali ilichukua asilimia 49% zilizobaki.

Kwa madhumuni ya kuepusha upotoshaji na kwa minajili ya kuzuia mkanganyiko wowote ambao unaweza kutokea kutokana na taarifa hizo, NICOL inapenda kufafanua kuwa ikiwa kama Mwanahisa, haikuhusika na wala haitakiwi, na **haijawahi kamwe kuhusika na uendeshaji** wa Tanzania Meat Company Ltd, ambayo ni kampuni huru iliyosajiliwa kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni Cap. 212, tarehe 28 Julai, 2008; Namba ya Usajili 66751, na inasimamiwa na kuendeshwa na Menejimenti yake yenyewe ikiongozwa na Bodi ya Wakurugenzi inayoteuliwa na wanahisa wake; Wizara ya Mifugo na Uvuvi nayo huteua mjumbe mmoja katika Bodi hiyo. Kwa hivi sasa, TMCL ina wanahisa wawili; nao ni National Investments Plc (NICOL) ambayo inamiliki asilimia 51% ya hisa, na Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), ikiwakilisha Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, inayomiliki asilimia 49% ya hisa.

Kwa mujibu wa sheria, uendeshaji na uteuzi wa wafanyakazi wa kampuni yeyote unafanywa na Menejimenti ya kampuni husika ikiongozwa na Bodi ya Wakurugenzi. Wanahisa hawaruhusiwi katu kujihusisha na uendeshaji wa kampuni; jukumu la Wanahisa huishia katika kuweka na kusimamia sera. Kwa misingi hiyo, **NICOL haijawahi kwa wakati wowote kusimamia uendeshwaji wa TMCL,** zaidi ya kusaidia kutoa msaada wa kifedha, ambapo mpaka tarehe 30 Desemba 2019, zaidi ya shilingi **bilioni 1.2** zimetolewa kama mkopo nafuu bila riba, ili kukabiliana na madeni hatarishi, kulipia mishahara, madeni ya kodi za serikali, malipo mengine ya kisheria na ununuzi wa mitambo na ukarabati wa mashine. Hivyo basi, habari iliyosambazwa ikidai kuwa NICOL ilikuwa inaendesha Tanzania Meat Company Ltd sio sahihi, inapotosha na haikubaliki kisheria. Laiti kama utaratibu huo ungekuwa unatumika, angalau basi pangalikua na Mkataba wa Huduma za Uendeshaji (Management Service Agreement), ukieleza majukumu, masharti ya wahusika na ada.

Aidha, taarifa hizo zilidai pia kwamba NICOL ilikiuka vifungu kadhaa vya Mkataba wa Mauzo wa Mali za Machinjio ya Dodoma, jambo ambalo linasemekana lilipelekea Mheshimiwa Waziri aamuru kutenguliwa mara moja Mkataba wa Mauzo, na kutoa maagizo hatua kadhaa zichukuliwe, ikiwa ni pamoja na kuweka shughuli zote za uendeshaji wa TMCL chini ya Wizara na kuteua Kaimu Meneja Mkuu kuiendesha kampuni. Katika mchakato huo, pia yalitolewa madai kadhaa dhidi ya NICOL ambayo hayakuthibitishwa, ikiwemo matumizi ya kibadhirifu ya fedha. Wanahisa wazingatie kwamba Mkataba wa Mauzo uliotajwa na Mheshimiwa Waziri ulikoma mara baada ya kuanzishwa na kusajiliwa kwa TMCL mwaka 2008, na kupewa umiliki wa mali zote zilizoainishwa katika mkataba huo **kama sehemu ya rasilimali za kampuni.** Hivyo basi, si NARCO wala NICOL inaweza kudai kwamba ina maslahi ya moja kwa moja katika umiliki wa mali za yaliyokuwa Machinjio ya Dodoma.

Wanahisa watakumbuka kuwa mnamo mwaka 2012, Mkutano Mkuu wa Wanahisa ulifukuza kutoka madarakani Bodi ya zamani ya NICOL kwa kushindwa kufuata miongozo ya Mamlaka za Udhibiti, misingi ya utawala bora na Sheria ya Makampuni. Changamoto hizo za uongozi mbovu wa Bodi ya NICOL ya wakati ule vilevile ziliathiri utendaji kampuni zake tanzu zote, ikiwa pamoja na shughuli za Bodi ya TMCL, ambayo ilidhoofika zaidi kutokana na king'ang'anizi cha Bodi ya NARCO kuendelea kutambua, kukumbatia, kuwatetea na kufanya kazi katika Bodi ya TMCL, kwa takriban miaka sita (6), na wakurugenzi waliokuwa wamefukuzwa na Wanahisa wa NICOL. Ni dhahiri kwamba katika kipindi chote hicho hakukuwa na ufanisi wala maendeleo chanya yoyote ya kibiashara kwa kuwa ufujaji mali na ubadhilifu ulitamalaki TMCL.

Mara baada ya kuteuliwa mwaka 2012, Bodi mpya ya NICOL iliomba mbia mwenza, NARCO, kushiriki katika jitihada za kuunda Bodi halali ya Wakurugenzi wa TMCL. NARCO walipinga na kukataa kutoa ushirikiano stahiki kwa kisingizio cha uwepo wa walichoita "*migogoro ya ndani ya NICOL*". Msimamo huu vilevile baadaye uliungwa mkono na Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Mheshimiwa Waziri aliyekuwepo wakati huo kabla ya uchaguzi mkuu 2015.

Ni muhimu sana kutambua kwamba tuhuma zote zilizotolewa dhidi ya NICOL katika taarifa inayodaiwa kutolewa na Mheshimiwa Waziri Mpina (MB) zinahusu matukio ya kipindi cha kati ya mwaka 2008 – 2016, na ni matokeo ya utendaji kazi duni na usimamizi mbaya wa Bodi ya TMCL ya kipindi hicho, ambayo haikuwa halali kwani ilijumuisha wakurugenzi waliofukuzwa na Wanahisa wa NICOL wakishirikiana na Bodi ya NARCO, kwa baraka za Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Bodi halali ya TMCL ilipoanza kazi mwaka 2016, ilichukua hatua za kinidhamu na vilevile kuchunguza ubadhirifu, na taarifa zilitolewa Wizarani na Polisi ambao walifungua Jalada la Uchunguzi wa Jinai Na. DOM/IR/5333/2017 baina ya TMCL na Leo Blasi Akonaay, na uchunguzi bado unaendelea, kama inavyodhihirishwa na mawasiliano kati ya wahusika Kumb DOM/CID/B.1/7/VOL. XL1/322 ya tarehe 27 Desemba 2018.

Aidha, kiutendaji Bodi halali ya TMCL vilevile ilichukua hatua kadhaa, ikiwamo kulipa madeni ya Serikali yaliyolimbikizwa, urasimishaji wa nguvu kazi, ukarabati wa vifaa vya uzalishaji ili kuigeuza TMCL kutoka machinjio pekee hadi usindikaji kamili wa nyama. Kukidhi malengo hayo, Bodi ilipendekeza kwa Wanahisa wa TMCL, ambao waliridhia, uteuzi wa Msimamizi Mtawala (Administrative Receiver) atathmini hali ya TMCL na kupendekeza namna ya kuimarisha zaidi na kuweka mkakati wa kuipa uwezo wa muda mrefu. Taarifa yake kwa Wanahisa iliidhinishwa kwa utekelezaji katika kikao chao maalum tarehe 27 Novemba 2019. Taarifa ya Administrative Receiver vilevile iliwasilishwa Wizarani, na Mheshimiwa Waziri mwenyewe aliomba na kupewa taarifa hiyo tarehe 27 Desemba 2019.

Izingatiwe kwamba ni Bodi halali ya TMCL ndiyo ilifanikisha utayarishaji wa taarifa za kifedha zilizolimbikizwa kinyume na sheria kwa kipindi cha miaka sita (6), kati ya mwaka 2009 na 2015, na kukaguliwa na wakaguzi huru wa nje wanaotambulika. Taarifa za mahesabu hayo hazioneshi uwepo deni lolote kwa kiwango kilichotajwa katika taarifa zinazosemekana kutolewa na Waziri kwenye vyombo vya habari. Hivyo basi chanzo cha deni cha Shilingi bilioni 15, ambalo NICOL inatuhumiwa nalo, ni kitendawili, na hasa inapobainika kwamba mwanahisa mwenza (Wizara) iliwahi kushiriki kuzuia utayarishwaji na ukaguzi wa mahesabu ya kampuni kwa miaka 6.

Kwa hiyo, mbali na kutokuwepo na chanzo chochote au uhalali wa deni kama NICOL ilituhumiwa nalo, ni dhahiri kwamba kwa vyovyote vile NICOL haiwezi kuwa inadaiwa shilingi bilioni 9.7 na Wizara ya Mifugo na Uvuvi (mwanahisa mwenza), au shilingi bilioni 5.4 na TMCL (kampuni tanzu iliyokuwa ikipewa mikopo nafuu na NICOL), kwani NICOL haihusiki kwa vyovyote vile na masuala ya uendeleshaji wa TMCL, ambayo ni kampuni inayojitegemea kisheria.

Pamoja na kwamba mpaka sasa NICOL haijapokea rasmi shutuma na madai kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, NICOL inakanusha bila kusita madai yote kwa ujumla wake yanayosemekana yalitolewa na Wizara hiyo katika vyombo vya habari. Tunapenda kuchukua nafasi hii kuwahakikishia Wanahisa kuwa NICOL itaendelea kushirikiana na Serikali kwa karibu katika kutekeleza majukumu yake yote, na kuzingatia sheria, sera za nchi na utawala bora, na itafanya yote yanayowezekana kulinda masilahi yao.

**KWA AMRI YA BODI**

**NICOL**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Uamuzi wa serikali kuzibana taasisi za fedha wa kupongezwa*

**MOJA** ya vilio ambavyo vimekuwa vikiwagusa wananchi ni riba kubwa ya mikopo wanazotozwa kutoka katika taasisi za fedha pindi wanapopata huduma hizo.

Kilio hiki ni cha muda mrefu na miongoni mwa taasisi ambazo zimekuwa zikishutumiwa ni benki na zile ndogo zinazotoa huduma za kifedha ikiwamo mikopo kwa wajasiriamali, wafanyakazi na wananchi wa kawaida.

Sambamba na kulalamikiwa kwa taasisi hizo kuwa zinawaumiza wakopaji, pia serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ambayo ndiyo mdhibiti zimekuwa hazikwepi lawama hizo.

Hatimaye Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, amevunja ukimya kuhusu suala hilo huku akiweka bayana kwamba riba kubwa inayotozwa na taasisi za fedha zimekuwa zikiwaumiza wananchi.

Dk. Mpango hakuishia hapo bali amewataka watumishi wa umma ambao wanaendesha huduma ndogo za fedha na kushiriki kuwapa mzigo mzito wananchi wa madeni kutokana na mikopo kuacha mara moja vinginevyo watachukuliwa hatua pindi watakapobainika kufanya hivyo.

Hata hivyo, Dk. Mpango katika mkutano wake jana na vyombo vya habari jijini Dodoma, alielekeza nguvu zaidi kuzionya taasisi zinazoendesha huduma ndogo za fedha kuwa ndizo zimekuwa zikinyooshewa kidole na kulalamikiwa kuwa zinatoza riba kubwa za mikopo.

Waziri katika kuweka sawa juu ya hilo, alisema wazi kwamba baadhi ya watoa huduma hao wamekuwa na tabia ya kujipangia riba wanavyotaka ili kujipatia faida kwa haraka bila kujali wananchi wanaowakopesha.

Kutokana na hali hiyo, alisema huduma hizo zimekuwa kikwazo kwa wananchi wengi kwa kuwa riba zinazotozwa na baadhi ya taasisi hizi hazina tofauti na viwango vya mikopo itolewayo. Kwa maneno mengine, mwananchi anaweza kutozwa riba ya asilimia 30 na anapochelewa kulipa anakumbana na adhabu ya kutozwa asilimia fulani kwa kila siku anayochelewa kupeleka rejesho.

Pamoja na kwamba tamko la Waziri limechelewa, kitendo hicho ni cha kupongezwa kwa sababu kitawasaidia wananchi ambao wameumizwa kwa kiasi kikubwa na hata kuwa maskini kutokana na huduma hizo.


Tunasema hivyo kwa sababu baadhi ya watu wamekuwa wakikopa fedha kidogo, lakini wanaweka dhamana kubwa kulinganisha na kiasi cha mikopo wanayochukua. Matokeo yake, wanaposhindwa wanafilisiwa dhamana zao na hatimaye kupoteza mali na kurudi kwenye umaskini.

Kwa mfano, baadhi ya taasisi za fedha zimekuwa zikitoa mikopo mifupi ya mwezi ambayo huenda haizidi Sh. milioni moja kwa mkopaji lakini anatakiwa kuweka dhamana ya kadi ya gari. Magari ambayo yanatakiwa kuwa dhamana ni yake yenye namba za usajili 'C' na 'D' tu na mkopaji anaposhindwa kurejesha mkopo, ananyang'anywa gari.

Hakika uamuzi ambao umechukuliwa na serikali wa kuzionya taasisi hizo ambazo zinawanyonya wananchi kupitia kivuli cha mikopo, unapaswa kufanyiwa kazi na kuleta matokeo chanya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Yamepita ya elimu 2019, sekta ipige hatua 2020

Na Beatrice Moses

TUMEINGIA mwaka mpya 2020, shule zimefunguliwa wiki hii. Wanafunzi wengi wakiwamo wa bweni, wameanza kurejea masomoni.

Kuna matukio kadhaa yameacha kumbukumbu katika sekta hii, yaliyoibuka mwaka 2019. Yapo yaliyokuwa mema na mengine mabaya, tena sana, kama ilivyo kwa mazuri sana.

Tunapaswa kumshukuru Mungu kwa kila jambo. Pia, yapo mambo ambayo ni ya ovyo, ambayo hatupaswi kwenda nayo.

Hapo nataja vitendo vya ukiukwaji maadili, ambavyo vimekuwa yakifanywa na baadhi ya wanafunzi, hivyo kusababisha kero kwa walimu, wanafunzi wenzao, wazazi na taifa kwa ujumla.

Ni wazi kila mzazi au mlezi mwenye busara na hofu ya Mungu, anapenda kusikia habari zilizo njema kuhusu mwanawe, wapo walionunua hadi zawadi na kuwakabidhi watoto wao kwa furaha, kutokana na kutajwa katika orodha ya waliofanya mambo mazuri, ikiwamo kilichowapeleka masomoni, kufaulu kwa kiwango cha juu.

Pia kuna wazazi ambao walio-jikuta katika wakati mgumu kutokana na vitendo vibaya ambayo watoto wao walitajwa kushiriki. Kuna waliolazimika kulipa fidia kwa hasara, kutokana na hatua ya kufukuzwa shule wakihusishwa na ovu shuleni.

Katika matukio yaliyoshtua na kusikitisha kwenye sekta ya elimu mwaka jana, ni linalodaiwa kufanywa na wanafunzi kadhaa wa Shule ya Sekondari Kiwanja, wilayani Chunya, Mkoa wa Mbeya, waliodaiwa kuchoma moto mabweni mawili shuleni hapo. Oktoba Mosi mwaka jana na kusababisha yateketee.

Sababu iliyotajwa kusababisha wanafunzi hao kuchoma moto mabwenini kutaka kulipiza kisasi, mara baada ya kunyang'anywa simu na uongozi wa shule hiyo.

Hatua kadhaa zilichukulia dhidi ya wanafunzi waliotajwa kuhusika, huku Mkuu wa Mkoa, Albert Chalamila, akiliagiza Jeshi la Polisi kuhakikisha wazazi wa watoto hao waliokutwa na simu kila mmoja analipa Sh. milioni moja zitakazotumika kukarabati mabweni yaliyoteketezwa.

Pamoja na maagizo hayo, Chalamila alifika shuleni mara moja na kuwacharaza bakora wanafunzi hao, iliyoendana na hatua zingine za kiuzazi. Picha za tukio hilo zilirushwa kwenye mitandao ya kijamii na kuzua mijadala mingi.

Mkuu wa Shule, Elly Mnyarape, alibainisha kuwa chanzo cha tukio hilo ni Septemba 30, 2019 na walipofanya msako na kukamata simu 26, ndipo usiku wake mabweni yaliteketezwa kwa moto.

Ni wazi, miliki ya simu kwa wanafunzi inazuiliwa kwa nia njema, kuepusha matumizi yasiyofaa, ikiwamo kuangalia picha na video za ngono zinazowachochea kushiriki au kupotoka kitabia.

Uhuru usio na mipaka ni matatizo, hasa kwa wanafunzi wa shule za sekondari ambao bado wanahitaji uangalizi wa wazazi au walezi, ili kuwasaidia katika kuwapa mwongozo.

Wanafunzi wote wanapaswa kuheshimu sheria na taratibu za shule, ili kuepuka mambo mabaya ikiwamo kukamatwa na kuadhibiwa ikiwamo kufukuzwa shule hatua ambayo itaweka doa na kumbukumbu mbaya itakayokuwa inawaumiza katika maisha yao.

Wazazi na walezi tuna wajibu wa kuhakikisha tunazungumza na watoto wetu ili wajue maadili mema na wazingatie mafundisho ya dini ambayo yatasaidia kuwapa mwongozo mwema hivyo kuepuka kushiriki kwenye vitendo viovu ambavyo vitawagharimu.

Pia walimu na viongozi wengine, hapo nikijumuisha Kamati za Shule, zina wajibika kuhakikisha wanasimamia vyema maendeleo ya wanafunzi na kuwapa mwongozo, utakaofanya shule zao ziwe na matokeo mazuri yakayowapa faraja na furaha, kuonyesha jinsi kazi yao ilivyo njema kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Aidha, upande mwingine mwaka 2019 uliandikwa historia mpya katika sekta hii ya elimu, baada ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), kufanikiwa kuanzisha tuzo za elimu.

Wanafunzi bora, walimu bora, halmashauri na mikoa iliyofanya vyema kwenye mitihani ya taifa ya kidato cha tano na darasa la saba walipewa tuzo.

Hatua hiyo inatajwa itachochea kiwango cha elimu nchini, kwa kuwa itawezesha kuongezeka ushindani katika kujifunza, kufundisha, kusimamia na utekelezaji wa sera za sekta hiyo kwa ujumla.

Waziri wa Tamisemi, Selemani Jafo, alikuwa mgeni rasmi katika hafla ya tuzo hizo iliyofanyika jijini Dar es Salaam, alikabidhi tuzo kwa washindi wa nafasi mbalimbali.

Katika mwaka huu 2020, tunatamani kuona ushindani katika tuzo hizi unaongezeka ili malengo ya kuanzishwa kwake yaweze kutimia. Ni furaha kuona sekta ya elimu ikipiga hatua kwa viwango vingine vizuri.

# Atoweka na kumwachia mume mtoto

**Na Hamisi Nasiri, MASASI**

FATUMA Salumu (38), mkazi wa kijiji cha Lukuledi, Masasi mkoani Mtwara, ametoweka nyumbani kwa mume wake, Omari Mtopwa, maarufu Mzee Omari Yanga na kumwachia mtoto mdogo wa umri wa miaka mitatu.

Akizungumza na gazeti hili jana nyumbani kwake, Mtaa wa Upanga Kata ya Napupa, wilayani Masasi, Mtopwa (60) alisema tangu mke wake aondoke nyumbani ni siku 15 hajarudi nyumbani na hajulikani aliko.

Kwa mujibu wa Mtopwa, moja ya shida kubwa anazopata kwa sasa ni jinsi ya kumlea mtoto huyo ambaye muda mwingi amekuwa akilia na kumlilia mama yake.

Mtopwa alisema Desemba 24, mwaka jana, Fatuma aliaga kwenda nyumbani kwa wazazi wake kijiji cha Lukuledi kwa ajili ya kushiriki shughuli za sherehe ya kuwatoa watoto jando.

Alisema alipoondoka kwenda huko, aliamwacha mtoto nyumbani lakini hadi sasa hajarudi tena licha ya jitihada za kumtafuta kufanyika.

Mtopwa alisema hadi anaondoka nyumbani siku hiyo hawajawahi kuwa na mgogoro wa aina yoyote katika ndoa yao na anashangaa mke wake kufanya kitendo hicho hasa cha kumwachia mtoto mdogo.

Alisema baada ya kuona siku zinazidi kwenda aliamua kufanya mawasiliano na wazazi wa mke wake kujua kama alikuwapo kwenye sherehe ya unyago ambayo aliaga kwenda kushiriki.

Mtopwa alisema tayari ameshatoa taarifa polisi juu ya kutoweka mke wake na kwenda kusikojulikana na kupewa taarifa ya yenye namba, Mass/ RB /2020 iliyofunguliwa juzi.

Baba mzazi wa mwanamke huyo, Salumu Hamisi alisema ni kweli binti yake alifika Desemba 24 alifika Lukuledi na kushiriki sherehe za unyago zilizofanyika nyumbani kwao.

Alisema Desemba 29, mwaka jana, binti yake aliaga kuwa anarudi nyumbani kwa mume wake Masasi na aliondoka kwa usafiri wa bajaji, hivyo waliamini kwamba ameshafika huko.

Hamisi alisema walishangazwa kupata taarifa kutoka kwa mkwe wao kuwa mtoto wake hajarudi hadi sasa.



Mbunge wa Jimbo la Dodoma Mjini, Anthony Mavunde (kushoto), akishiriki kutengeneza miundombinu ya barabara iliyoharibiwa na mvua katika eneo la Kata ya Ntyuka, jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wadaiwa NIC waanza kulipa madeni

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Bima la Taifa (NIC), limesema kuwa wadaiwa wake wameanza kulipa madeni yao na kwa sasa yamebakia madai machache.

Katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya 2017/2018 ilibainisha kuwa kuna madai ya kiasi cha Sh. bilioni 63.

Shirika hilo limewaondoa hofu wateja wake kuwa hali ya kifedha iko vizuri kwa kuwa waliokuwa wanadaiwa wanalipa madeni yao kama kawaida.

# Mbaroni kwa tuhuma wizi vitu

**Na Gideon Mwakanosya, SONGEA**

JESHI la Polisi mkoani Ruvuma, linawashikilia watu tisa kwa tuhuma za kukutwa na vitu mbalimbali vinavyosadikiwa kuwa vya wizi vikiwamo runinga na majiko ya gesi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, alisema jana kuwa watuhumiwa hao (majina yanahifadhiwa kwa sababu za uchunguzi), wamekamatwa katika matukio tofauti wakiwa na vielelezo mbalimbali vinavyodhaniwa kuwa vya wizi.

Maigwa alisema mali hizo walizokutwa nazo baadhi zinahofiwa viliibwa mkoani Njombe ambako inadaiwa kumekuwa na matukio mengi ya watu kuibiwa runinga (flat screen).

Alivitaja vitu ambavyo watuhumiwa hao walikamatwa navyo ni 'Flat Screen' tisa, Samsung mbili, 'home base' mbili, sola moja, Oceanic moja, LG moja na TV Flat Screen mbili LG 1 na tayari zimetambuliwa kuwa ni mali ya uwanja wa Ndege Songea ambako ziliibwa hivi karibuni.

Mali zingine ni runinga tatu za kawaida maarufu kama TV za chogo LG1, Hitachi moja, Digital moja, ving'amuzi vitatu na kati ya hivyo viwili ni vya Star Times na kimoja ni cha Azam na adapta yake.

Vingine ni dishi moja la Azam, pikipiki moja ya rangi nyeusi aina ya Haojue ambayo haina namba za usajili na redieta moja ya gari, majiko mawili madogo ya gesi aina ya Orxy na Mihan, CPU mbili Dell na LG Monitor za kompyuta mbili na Dell na Hp.

Pia alisema watuhumiwa walikutwa na redio Subwoofer aina ya Sea Piano mbili na spika zake tatu, spika zisizo na jina nyeusi nne, deki mbili aina ya Mr UK, magodoro matano na 'play station' tatu aina ya Sonny.

# Wamwangukia Rais mgogoro wa ardhi

**Na Innocent Ng'oko, MBEYA**

WANANCHI wa Kijiji cha Jangulutu –Mabanda, Mbarali mkoani Mbeya, wamemwomba Rais John Magufuli kuingilia kati mgogoro wa shamba lenye ukubwa wa ekari 57 uliodumu kwa zaidi ya miaka mitano na kuathiri shughuli za maendeleo.

Mmoja wa wakazi hao, Mika Msasi, alisema licha ya mvutano wa muda mrefu, Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Ruben Mfune, baada ya kujiridhisha juu ya eneo hilo Septemba 6, mwaka jana, aliamuru wapewe wananchi.

Alisema jambo la kushangaza, wavamizi hao, Oktoba 10, mwaka jana walifungua kesi katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Mbeya, hivyo kutoa zuio kwa wananchi kuendeleza eneo hilo.

Msasi alisema mgogoro huo uliibuka mwaka 2015 baada ya wananchi kulalamikia kitendo cha mmoja wa wananchi wa kijiji hicho, Benard Masembula, kuuza kinyemela eneo lililokuwa limetengwa na serikali kwa ajili ya kijiji hicho kama eneo la akiba.

Alisema mwanzoni mwa mwaka jana, serikali iliamua kuingilia kati mgogoro kufanya uchunguzi kupitia wataalamu wake na kubaini kuwa Masembula hakuwa na uhalali wa kuuza sehemu ya eneo la kijiji ndipo serikali ikachukua uamuzi wa kuligawa kwa wananchi.

Ofisi ya Mkoa wa Mbeya Agosti, 2018 iliuagiza uongozi wa wilaya ya Mbarali kuhakikisha wananchi hao wanarejeshewa eneo hilo haraka.

Baraka Mwilongo, alibainisha kuwa mgogoro huo umedumu kwa ziadi ya miaka mitano na kuwa licha ya jitihada za kutatua, kumekuwapo na mizengwe.

Mwilongo alisema mwaka 2018, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Amosi Makala, aliiagiza wananchi wa eneo hilo na vitongoji vingine kupewa ardhi iliyoporwa na pia kwa nyakati tofauti, kutoa maelekezo kwa ofisi ya mkuu wa wilaya kumaliza mgogoro huo. Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Mfune, amekiri kuufahamu mgogoro huo, na kuwa wanaufuatilia.

# Samaki wakaushwa chooni

**Na Daniel Limbe, CHATO**

WAKAZI wa Wilaya ya Chato mkoani Geita wako katika hatari ya kukumbwa na magonjwa ya kuhara kutokana na baadhi ya wavuvi kukausha samaki kwenye maeneo ya vyoo.

Hali hiyo inaelezwa kutishia afya ya walaji wa kitoweo hicho kutokana na wadudu warukao na watambaao kuhamishia kwenye chakula kinyesi kutoka chooni.

Nipashe imeshuhudia dagaa wakiwa wameanikwa chini ya mchanga kwenye choo cha wavuvi katika Mwalo wa Chato, huku kukiwa na ukimya wa viongozi wenye mamlaka katika kudhibiti hali hiyo.

Katika udadisi wake, Nipashe ilimtafuta Mwenyekiti wa Kikundi cha Raslimali ya Uvuvi Ndani ya Ziwa Viktoria (BMU) kwenye mwalo huo, Kamese Malima, ambaye alikiri kuwapo kwa dosari hiyo katika ukaushaji wa samaki. Malima alidai dosari hiyo inachagizwa na ufinyu wa eneo kwa ajili ya wavuvi kukausha samaki wao, hasa dagaa.

"Hali hii ni kweli ipo kama unavyoiona hapa, dagaa wameanikwa hadi eneo la choo kutokana na ufinyu wa ardhi baada ya eneo la awali kujaa maji," alisema.

Malima alidai kuwa hivi karibuni, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, alifanya ziara ya kikazi wilayani humo na walimwomba kuboresha mwalo wao ikiwa ni pamoja na kupanua eneo la kukausha dagaa kwa jua.

"Awali tulikuwa na chanja 45 za kuanikia dagaa ambazo zilitolewa na wahisani wa LVEMP. Bahati mbaya chanja zote ziliharibika na tumezihifadhi stoo na ndiyo maana wavuvi wengi wanaanika chini ya mchanga, licha ya kwamba tunatambua sheria za uvuvi zinazuia," alisema.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, dagaa safi wanaoanikwa kwenye chanja huuzwa kwa Sh. 20,000 kwa mfuko wa kilo 20 huku wale wanaoanikwa chini ya mchanga wakiuzwa kwa Sh. 7,000 kwa mfuko huo.

Alisema wavuvi wengi hulazimika kukausha samaki wao kwenye mchanga kutokana na gharama kubwa za kununua chanja, mmoja ukiuzwa kwa Sh. 250,000.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kalema, Faresi Musiba, ambaye ni Mjumbe wa Serikali ya Kijiji cha Chato, alisema kitendo cha samaki kuanikwa chini, tena karibu na choo, hakikubaliki kwa kuwa kinahatarisha maisha ya walaji wa kitoweo hicho.

Kutokana na hofu ya magonjwa ya mlipuko, Musiba alidai tayari wameshatoa maelekezo kwa uongozi wa BMU kuzuia aina hiyo ya ukaushahji wa samaki, lakini akakiri utekelezaji wa maagizo yao bado haujafanyika.

Aliahidi kuwasiliana na Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Makonzere Phinias, ili kutafuta njia mbadala ya kutatua tatizo hilo kwa kuwa BMU iko chini ya mamlaka ya kijiji kwa mujibu wa sheria za uvuvi.

Nipashe pia ilimtafuta Ofisa Uvuvi Mwandamizi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato, Deograthias Ngeleshi, kuzungumzia suala hilo, akadai hana uhakika iwapo samaki wanaoanikwa kwenye eneo la choo hicho wanatumika kwa matumizi ya chakula cha binadamu. Ngeleshi alikiri dagaa wanaoanikwa chini, wanauzwa kwa bei ndogo kulinganishwa na wanaokaushwa kwa kutumia chanja.

"Ni kweli kuna dagaa wameanikwa hapo chini karibu na choo ila sina uhakika sana kama wanatumika kwa matumizi ya binadamu. Huwa tunajitahidi kuwaelimisha namna ya kuanika dagaa kwenye chanja zinazokubaliwa kisheria, lakini hawazingatii kutokana na mazoea, tatizo hili lipo nchi nzima," alidai.

Mganga Mkuu Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Chato, Ligobeth Kalisa, alisema suala hilo linapaswa kutolewa ufafanuzi na Ofisa Afya, lakini akasisitiza "kinga ni bora kuliko tiba".



Mwananchi wakipita jirani na taka zilizotelekezwa bila ya kuzolewa kando ya barabara katika eneo la Kigogo, jijini Dar es Salaam jana.
**PICHA: MIRAJI MSALA**

## 7 mbaroni tuhuma kujifanya maofisa usalama wa Ikulu

INATOKA UK 2

Katika tukio lingine, Kamanda Murilo alidai wamemkamata Ashery Justol kwa tuhuma ya kujifanya Kamanda wa Polisi mkoani humo na kuweka picha ya Kamanda Murilo katika ukurasa wake wa mtandao wa kijamii kwa lengo la kuwaaminisha wananchi anaowapigia simu na kuwaomba msaada wa kifedha.

"Tumemkamata Ashery ambaye ni mkazi wa Igoma mkoani hapa, kabila lake Mfipa, ambaye alikuwa akiwapigia simu watu mbalimbali na kuwatumia ujumbe mfupi kuwa yeye ni Kamanda wa Polisi mkoani Mwanza.

"Amepatwa na matatizo ya kijamii, hivyo wamchangie fedha au vitu, huku akiwasisitiza wasimpigie simu maana mazingira aliyopo hawezi kuongea," alidai.

Kamanda Murilo alidai mtuhumiwa huyo alichukua picha yake kwenye mtandao yenye sare za Jeshi la Polisi na kuiweka kwenye ukurasa wake ikiwa kila anayefanya naye mawasiliano akiangalia kwenye wasifu wa namba hiyo kwenye WhatsApp anakuta picha ya Kamanda Murilo, hivyo watu hao kuamini ni kamanda kweli.

## Mwanafunzi chuo kikuu jela kumuhonga ofisa wa mitihani

INATOKA UK 2

Kutokana na tukio hilo, aliwataka wanafunzi wa vyuo kuzingatia masomo ya darasani na sikutegemea kutoa rushwa ili wapate ufaulu mkubwa bila kuwa na uwezo wa masomo.

"Nawaomba wanafunzi jijengeeni tabia ya kusoma, taifa linahitaji watu waelewa wenye uwezo wa kupeleka maendeleo mbele," alisema Kibwengo.

Alisema hakuna sababu ya kupoteza muda kutembea, badala yake wakae darasani wasome ili kuepuka kufikiria kutoa rushwa kwa sababu sheria inakataza hilo suala.

Katika hatua nyingine, alisema Sekta ya Ardhi inaongoza kwa vitendo vya rushwa kwa asilimia 31.4, ikifuatiwa na Serikali za Mitaa asilimia 22.9 na huku Polisi asilimia 14.3.

Kibwengo alivitaja vyama vya siasa kuwa ni asilimia 11.4, Mahakama (4.3), Elimu (4.3), huku sekta zilizosalia ni asilimia 11.4. Alifafanua zaidi kuwa ni muhimu kwa sekta zilizolalamikiwa sana wajitafakari na kujirekebisha kabla hawajafikiwa na mkono wa sheria.

Aliwataka wananchi kuendelea kutoa taarifa pale wanapoona kuna viashiria vya rushwa.

## Oliver Alawuba ateuliwa Mkurugenzi mpya UBA

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya United ya Afrika Plc (UBA), imetangaza safu mpya ya uongozi, huku Oliver Alawuba, akiteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa UBA Africa, anayesimamia shughuli za nchi 20 za Afrika ukiitoa Nigeria.

Hatua hiyo inatokana na baadhi ya viongozi wake kustaafu katika bodi akiwamo Victor Osadolor, ambaye alitumikia nafasi hiyo kwa miaka tisa.

UBA for Africa inahudumia wateja zaidi ya milioni 19 katika Bara la Afrika, ikitoa huduma za rejareja, biashara na taasisi za kitaifa na imewekeza katika huduma jumuishi za kifedha na utekelezaji wa miradi katika nchi za Afrika.

Taarifa iliyotolewa na benki hiyo jana, ilieleza Alawuba ana miongo mitatu ya uzoefu katika tasnia ya benki na aliwahi kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa UBA Ghana na baadaye kuwa Mkurugenzi Mtendaji UBA Africa kabla ya kurudi Nigeria kuendesha Benki ya UBA ya ukanda wa mashariki.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, chini ya uongozi wake, Benki ya UBA ya ukanda wa mashariki imekuwa ni benki inayokua kwa kasi zaidi katika Afrika.

"Pia, bodi ilimteua Msenegali Abdoul-Aziz Dia kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Hazina na Huduma ya Benki Kimataifa kwa idhini ya Benki Kuu ya Nigeria. Aziz anakuwa mkurugenzi mtendaji ni atasaidia kwa uzoefu wake aliopitia nchi mbalimbali kukuza maendeleo ya Benki ya UBA.

"Dia atawajibika kwa mtandao wa kimataifa wa shughuli za UBA huko New York, London na Paris, pamoja na Hazina kwa ujumla, ambapo UBA inatoa sehemu kubwa ya bidhaa kwa mataifa, taasisi za kimataifa na wateja wa Afrika," ilieleza taarifa hiyo.

Mbali na hao, pia Chukwuma Nweke, ameteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Huduma za Rejareja na Malipo, huku Chiugo Ndubisi akiteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu na Mkuu wa Uendeshaji wa UBA kwa idhini ya Benki Kuu ya Nigeria.

Ilielezwa katika taarifa hiyo kuwa uteuzi mpya wa bodi umezingatia uwekezaji mkubwa katika rasilimali watu kwa kuchagua watendaji wenye sifa stahiki na utendaji mkubwa katika kuendeleza benki.

## HABARI KITAIFA

# Waziri aagiza mkandarasi, mhandisi kukamatwa

**Na Mwandishi Wetu, SUMBAWANGA**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, ameagiza kukamatwa kwa mkandarasi wa ujenzi, Ding Fubing, pamoja na mshauri elekezi wa mradi wa ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) Rukwa, Swalehe Kyabega.

Ndalichako alitoa amri hiyo juzi kutokana na wataalamu hao kushindwa kukamilisha mradi huo kwa wakati huku wakiendelea kusuasua juu ya ukamilifu wa ujenzi huo ambao ulitakiwa kukamilika Desemba 30, mwaka jana, baada ya kuongezewa siku 100 lakini hadi sasa umefikia asilimia 52.

Prof. Ndalichako alisema kimkataba, mkandarasi huyo alitakiwa kuthibitisha kwa risiti matumizi ya Sh. bilioni 1.5 malipo ya awali ya ujenzi kupitia kwa mshauri elekezi ambae alishindwa kutoa vielelezo vinavyoonesha utekelezaji wa takwa hilo la kisheria.

Kadhalika, alisema mshauri huyo ameshindwa kusimamia matumizi ya fedha za serikali katika utekelezaji wa mradi huo.

"Mkandarasi aende akakae ndani mpaka vile vifaa mlivyoruhusu viondoke hapa, mpaka vitakaporudi ndio muwaachie. Naona sasa hii inakuwa kuchezeana. Hamna kitu ambacho kinachoeleweka.

"Utakwenda kukaa selo hadi utakapotoa maelezo ya ufasaha juu ya jambo hili kwa sababu huwezi kucheza na serikali namna hii. Mara ya mwisho nilipokuja hapa mlikuwa na vifaa kama vyuma chakavu. Mmeleta vifaa halafu mmeviondoa kuvipeleka sehemu nyingine. Utakaa ndani hadi vifaa hivyo vitakaporudi na uwe na watu wa kutosha kufanya kazi kwa sababu tumechoka, tunataka huu ujenzi uishe, wachukue wakae ndani," alisisitiza.

Hali kadhalika, mkandarasi huyo alionekana kuwafanyisha kazi wafanyakazi wa mradi huo kwa malipo ambayo yako kinyume cha mkataba wa serikali huku baadhi ya watendaji wengine wa sekta ya umeme wakilalamika kufanyishwa kazi bila ya mkataba maalum.

Awali, akisoma taarifa ya maendeleo ya ujenzi wa chuo hicho, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu ya Ufundi Stadi (Veta), Dk. Pancras Bujuru, alisema mkandarasi huyo tayari amelipwa Sh. 3,507,174,603 sawa na asilimi 35 ya thamani ya mradi huo na malipo ya mwisho yalikuwa Sh. 330,521,213.79 aliyopewa Desemba 12, mwaka jana.

"Mheshimiwa waziri, kwa hali hii mkandarasi amethibitisha uwezo mdogo wa kutekeleza mradi huu na hatuna imani kama utatekelezwa kwa wakati kwa sababu muda aliopewa na kuongezewa siku 100 vyote vimekwisha na bado kazi hazijaisha kwa muda. Kwa hiyo tunadhani uwezo wake wa kutekeleza mradi hauturidhishi hata sisi.

"Mshauri elekezi ana jukumu la kumsimamia mkandarasi kwa niaba yetu kwa sababu tumemwajiri kwa kazi hiyo. Tunajua kwamba amekuwa akitoa maelekezo, lakini kumekuwa na udhaifu wa kuyasimamia kwa kuchukua hatua zinazostahili na kwa muda mwafaka naye tunadhani ana upungufu," alisema.

Agosti 31, 2018 kampuni ya Tender International ilikabidhiwa kiwanja kwa ajili ya kuanza ujenzi wa chuo Veta katika Manispaa ya Sumbawanga pamoja mshauri elekezi Sky Architect Consultancy Ltd.

Mradi huo ulitarajiwa kukamilika Septemba, mwaka jana huku gharama zake zikiwa Sh. 10,700,488,940.05.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Mshauri Elekezi wa mradi wa ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi (VETA), mkoani Rukwa, Swalehe Kyabega (kulia), juu ya maendeleo ya mradi huo na namna alivyousimamia, akiwa ziarani mkoani humo juzi. **PICHA: OFISI YA RC RUKWA**

## Watakiwa kuwa na vibali umiliki nyara za serikali

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

WAGANGA wa jadi katika Halmashauri ya Ushetu, Kahama mkoani Shinyanga, wametakiwa kuandika barua za maombi za kumilikishwa nyara za serikali kisheria hali ambayo itawasaidia kutoingia kwenye mikono ya dola pindi wanapokutwa nazo.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Mbunge wa Usheru, Elias Kwandikwa, alisema hayo juzi wakati akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Mseki, Kata ya Bulungwa, huku akisema waganga wa jadi wengi wanamiliki nyara za serikali, huku wakiwa hawana vibali vya umiliki.

Alisema kila mganga wa jadi katika jimbo hilo anatakiwa kuwa na kibali cha umiliki wa nyara za serikali alizo nazo nyumbani kwake ili kuondokana na matatizo yanayoweza kujitokeza pindi operesheni itakapoanza dhidi ya waganga wa jadi.

"Tunatakiwa kujitathmini na kuchukua hatua ya kufika sehemu husika na kuchukua fomu na kujisajili juu ya umiliki wa nyara za serikali tulizo nazo nyumbani mwetu. Najua mnazo, angalieni zisije zikawakosesha amani wakati mnapokutwa nazo," alisema.

"Jitokezeni mzipeleke nyara mlizo nazo kituo cha polisi au ofisi zozote za serikali ngazi za vijiji na kata. Msikae mnajificha ficha, mimi nitawasimamia mpate vibali ili mfanye kazi zenu kwa uwazi na amani.

Kwandikwa alisema hakuna sababu inayowafanya na waganga wa jadi kuendelea kufanya shughuli zao kwa kificho na badala yake wafikie hatua ya kujitambua na kujiamini katika utendaji wao katika shughuli zao.

Alizitaja baadhi ya nyaraka hizo ambazo waganga wa jadi wanatakiwa kuwa na umiliki wake kuwa ni ngozi ya chui na mkia wa simba.

**"Jitokezeni mzipeleke nyara mlizo nazo kituo cha polisi au ofisi zozote za serikali ngazi za vijiji na kata. Msikae mnajificha ficha, mimi nitawasimamia mpate vibali ili mfanye kazi zenu kwa uwazi na amani.**

# Serikali yaja na mpango kuboresha huduma Tasaf

**Na Mwandishi Wetu, SINGIDA**

SERIKALI imeweka mkakati wa kuboresha huduma zinazotolewa kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf), ili kuwanufaisha zaidi walengwa na hatimaye kupunguza umaskini nchini.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mary Mwanjelwa, aliyasema hayo juzi katika kijiji cha Mtipa, Manispaa ya Singida. Mwanjelwa yuko Singida kwa ziara ya kikazi.

Alisema azma ya serikali ni kuhakikisha wananchi, hususani ambao bado wanaishi katika umaskini wa kipato, kupitia mpango wa kunusuru kaya maskini, wanawekewa mazingira yatakayowawezesha kutumia fursa za kujiletea maendeleo na hatimaye kuondokana na umaskini.

"Rais John Magufuli anayo dhamira ya dhati katika kuboresha maisha ya wananchi. Kinachotakiwa kwenu nyie walengwa wa Tasaf ni kumuunga mkono kwa kutumia vizuri fursa zilizoko kwenye mpango huu ulioanzishwa na serikali kupitia Tasaf," alisema.

Aidha, Mwanjelwa alitoa rai kwa walengwa wa Tasaf kuhakikisha wanatumia ipasavyo huduma za Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini ikiwamo kuwapeleka shule watoto na kufuatilia mahudhurio yao huku pia akiwataka kuanzisha shughuli za uzalishaji mali ili kujiongezea kipato.

Naibu Waziri huyo pia alizungumzia sehemu ya pili ya utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya maskini ambayo inatarajiwa kuanza baada ya kuzinduliwa rasmi na Rais Magufuli kuwa mkazo umewekwa katika kuhakikisha kuwa walengwa wenye uwezo wa kufanyakazi wanatumia nguvu zao katika utekelezaji wa miradi itakayoibuliwa kwenye maeneo yao chini ya utaratibu ujulikanao kama ajira za muda.

"Serikali inasisitiza kila mwananchi mwenye uwezo wa kufanya kazi ni lazima atumie uwezo wake huo katika shughuli za kufanyakazi ili kutoa mchango katika ujenzi wa taifa. Hata hivyo wazee na walengwa ambao hawana uwezo wa kufanya kazi kutokana na matatizo mbalimbali, yakiwamo maradhi ya muda mrefu, serikali kupitia Tasaf itaendelea kuwahudumia," alisema.

# Mkwara wa DC wakimbiza wadhalilishaji wa watoto

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

WANAUME 17 wakazi wa Wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba, wamekimbia makazi yao baada ya Mkuu wa Wilaya hiyo, Salama Mbarouk Khatib, kuahidi kuendelea kuwataja hadharani wanaowatendea watoto vitendo vya udhalilishaji.

Wakizungumza na wanahabari, wananchi wa shehia za wilaya hiyo walisema, hatua aliyoichukua Mkuu wa Wilaya imewafurahisha sana.

Walisema hatua hiyo imewatia hofu wanaowatendea watoto udhalilishaji, hivyo wanaamini litasaidia kupunguza ama kuondosha kabisa vitendo hivyo.

Walieleza vijana 17 wa kiume wameshakimbia katika shehia zao na kwenda nje ya kisiwa cha Pemba, kwani wanahisi kuwa wameshajulikana kwamba wao ndio wanaoharibu watoto.

Assaa Ali Ameir, mkazi wa Kijiji cha Mamoja alieleza kuwa: "Tunaiomba serikali ichukue hatua kali kwa wale wote wenye viashiria vya vitendo hivi, kwani wanavitia doa vijiji vyetu kutokana na historia yake ya kutoka masheikh wakubwa."

Naye Ali Mbarouk Mohamed, mkazi wa Uondwe, alieleza kuwa, walimu wa siku hizi wamekuwa wakijiingiza zaidi katika mambo ya kidunia, jambo ambalo linawasababishia kujiingiza katika vitendo viovu.

"Zamani walimu wa madrasa ilikuwa wamebobea katika dini zaidi na hawashughulikii mambo ya kidunia, ila hawa walimu wa leo ni mtihani mpaka walimu wa skuli hawaaminiki tena, hivyo tutafute walimu wanaostahiki, maana ni mtihani kwa kweli," alisema.

Saada Juma Mohamed (18), aliiomba serikali kuwafunga wahalifu hao miaka isiyopungua 50, kwani wamekuwa wakiwabaka na kuwalawiti watoto bila ya kuwa na huruma.

Mtoto Hamad Abdalla Shaame anayesoma darasa la nne, alieleza kuwa, amekuwa akiwaona watoto wenzake wakichukuliwa na kijana mwenye umri wa miaka 15 (jina limehifadhiwa) na kupelekwa msituni kwenda kuwalawiti.

Sheha wa Shehia ya Shumba Viamboni, Time Said Omar, alisema baada ya Mkuu wa Wilaya kufanya mikutano na kuwataja wahalifu hao, imekuwa imani katika vijiji vyao, kwani hata mambo ya starehe kama kuonyesha TV usiku nje yamepungua.

"Ilikuwa saa zote unakuta watoto wa

INAENDELEA UK. 24



Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, akishiriki kupika uji lishe kwa ajili ya watoto wakati wa Siku ya Lishe eneo la Tanangozi, mkoani Iringa juzi, wakati wa ziara yake mkoani humo kukagua shughuli za afya na maendeleo ya jamii. **PICHA: WAMJW**

# TPA yaimarisha bandari zote kwenye Ziwa Nyasa

**Na Elizabeth Zaya, Aliyekuwa NYASA**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), imesema imeimarisha miundombinu katika bandari zote za Ziwa Nyasa ili kurahisisha usafiri wa majini kwa wananchi wanaozunguka ziwa hilo.

Meneja wa Bandari za Ziwa Nyasa, Abedi Gallus, alisema katika Bandari ya Itungi tayari wamejenga gati lenye urefu wa mita 70, karakana na jengo la ofisi.

Pia alisema katika Bandari ya Kiwira, wamejenga gati la urefu wa mita 15 kwa ajili ya matumizi wa muda mfupi pamoja na ghala la kuhifadhia mizigo, huku katika Bandari ya Mbambabay nako wakijenga gati la muda mfupi wakati wakijiandaa kwa maboresho makubwa.

Gallus alisema katika mwaka wa fedha 2019/2020, TPA imesaini mkataba wa ujenzi wa Bandari ya Ndumbi yenye thamani ya Sh. bilioni 12. 28 utakaotekelezwa kwa muda wa miezi 22.

Katika Bandari ya Liuli, alisema wameanza maboresho huku katika Bandari ya Manda nako uboreshaji unaendelea.

"Kwa kweli tunajivunia kazi kubwa inayofanywa na serikali ya awamu ya tano, maboresho makubwa yamefanyika na tunaona impact (matokeo) yake kwa sasa, hata vyombo vya majini kwa sasa tumepata vya kutosha," alisema Gallus.

"Wananchi wengi wanaoishi pembezoni mwa ziwa hili, wengi wao wanategemea usafiri wa maji, lakini ilikuwa shida sana kipindi cha nyuma kwa sababu hakukuwa na meli, walikuwa wanatumia maboti na mitumbwi ambayo hata hivyo haikuwa salama, lakini kwa sasa tunavyozungumza tuna meli tatu, mbili za mizigo na moja inabeba mizigo na abiria kwa pamoja."

## Bil.1/- zasaidia ufugaji Njombe

**Mwandishi Wetu, RUVUMA**

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) mwaka jana ilitoa zaidi ya Sh. bilioni moja katika kuongeza tija ya mnyororo wa thamani kwa miradi ya viwanda na ufugaji mwaka jana kwa Mkoa wa Njombe.

Hayo yamebainika katika ziara ya TADB mkoani hapo, ya kutembelea miradi ya kilimo iliyowekezwa na benki pamoja na wanufaika wakiwamo wakulima na wafugaji. Lengo la ziara hiyo ni mkakati wa benki kuanza mwaka mpya kwa kutathmini na miradi inavyoendeshwa, hatua zilizofikiwa na kutafuta fursa na maeneo mapya ya uwekezaji ili kuwaongezea tija wakulima.

Ziara hii ya Mkurugenzi Mtendaji wa TADB iliambatana na Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Ruth Msafiri, ambapo walitembelea kiwanda cha kuongeza thamani ya maziwa, kiitwacho Njombe Milk.

Kiwanda ambacho kinamilikiwa na chama cha wafugaji wa mkoa wa Njombe pamoja na kiwanda cha kuchakata mahindi kiitwacho Mama Seki Group.

John Kusila, meneja wa kiwanda cha Njombe Milk, alieleza jinsi TADB ilivyoweza kusaidia kuongeza uzalishaji wa maziwa pamoja na kuongeza vitendea kazi ambavyo vinaongeza ufanisi.

Alisema zaidi ya wafugaji 900 wa vyama vya msingi wataendelea kunufaika, na kuwa ana furaha kubwa kwani TADB inaendelea kutoa ushirikiano, ushauri na kuwajengea uwezo waendeshaji wamradi huo nje ya fedha iliyowekeza.

Vilevile TADB imewezesha kufanikisha ndoto za kukuza miradi ya vijana na wanawake. mmiliki wa kiwanda cha Mama Seki Group, Lucy Yona alieleza TADB imesaidia kutimiza ndoto yake ya kuwa na mashine kubwa zenye uwezo wa kutengeneza vifungashio na kuchakata mahindi tani 30 kwa saa 24 tu.

Alisema licha ya kuwa na ndoto hii kwa muda mrefu kipindi anauza mkaa kwa baiskeli na kuutembeza, kusaga na kukoboa mahindi katika viwandavingine, na kuwa kwa kupitia TADB ndoto yake imetimia na kuweza kuajiri vijana zaidi ya 12 mpaka sasa.

Kadri Mama Seki anavyoongeza utayarishaji wa chakula cha binadamu na mifugo kwa kuchakata mahindi, ndivyo wakulima wa mahindi watazidi kunufaika kimasoko.

Hivyo hivyo, kwa wafugaji wa ng'ombe wa maziwa, pamoja na hayo katika mkoa wa Njombe TADB imeshawekeza takribani Sh. bilioni 1 ikiwamo katika mradi wa kilimo cha parachichi," alisema Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine.

Naye DC Msafiri ameipongeza benki hiyo kwa kuwiwezesha viwanda hivyo kwani ni chachu ya maendeleo hasa kwa wakulima na wananchi, kwani wengi wananufaika na ajira na kuviwezesha viwanda hivyo kuendelea kuongeza uzalishaji zaidi na kuzidi kuwa wabunifu na kuendelea kushirikiana na benki ili kuendelea kunufaika.



## HABARI ARUSHA

# Walalamikia mfumo dume

**Na Mwandishi Wetu, BABATI**

WANAWAKE wa vijiji vinne vya Wilaya ya Babati mkoani Manyara, wamekiri kuwa mila na desturi zinazokumbatiwa na wanaume zimekuwa kikwazo kwao kushindwa kuwa na haki ya kumiliki ardhi.

Wanawake hao walipaza sauti zao mwishoni mwa wiki iliyopita wakati wakipewa mafunzo ya nanma ya kupata haki ya kumiliki ardhi yaliyoandaliwa na Shirika lisilo la kiserikali la Cosita.

Wanawake waliohudhuria katika mafunzo hayo ya kuwajengea uwezo walitoka katika vijiji vya Kiongozi, Malangi, Chemchem na Mtuka.

Mwanaidi Ramadhan mkazi wa kijiji cha Kiongozi, akizungumza na Nipashe baada ya mafunzo hayo, alisema mafunzo hayo yatawabadilisha na watakwenda kutoa elimu kwenye jamii.

Alisema kwa kipindi kirefu wanaume wamewaonea wanawake huenda baada ya kupata mafunzo hayo watakwenda kuleta mabadiliko katika jamii.

Philomena Homa kutoka kijiji cha Chemchem alisema elimu waliyoipata itawasaidia kuamka na kudai haki yao ya kumiliki ardhi na mali katika jamii.

Homa alisema iwapo watapata ardhi itawasaidia kuinuka kiuchumi kwa kuwa wataitumia kufanya uzalishaji wa mali na hatimaye wao kuchangia shughuli za kimaendeleo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Cosita, Patrice Gwasma, alisema wanatekeleza mradi wa haki za ardhi kwa wanawake na unafadhiliwa na Shirika la Foundation for Civil Society (FCS).

Gwasma alifafanua kwa mujibu wa utafiti wa kamisheni ya umoja wa mataifa uliofanyika mwaka 2012, kwa kishirikiana na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden (Sida), lililofanya utafti mwaka 2015, wote kwa pamoja walibaini asilimia 20 ya wanawake duniani ndio wanamiliki ardhi.

Alisema asilimia 80 ya wanawake duniani hawamiliki ardhi, hivyo ameitaka jamii kubadilika na kutoa elimu ili wanawake na wanaume wote wawe na haki sawa ya umiliki ardhi.

Alitumia fursa hiyo, kutoa elimu kwa wanawake ya haki ya kumiliki ardhi ili waitumie kwa ajili ya kuwatetea watoto wao.

**Gwasma alifafanua kwa mujibu wa utafiti wa kamisheni ya umoja wa mataifa uliofanyika mwaka 2012, kwa kishirikiana na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden (Sida), lililofanya utafti mwaka 2015, wote kwa pamoja walibaini asilimia 20 ya wanawake duniani ndio wanamiliki ardhi.**

# Mtoto wa kipaji cha pekee awasili shuleni

**Na Isack Allan, ARUSHA**

MTOTO Baraka Raphael (3) mkazi wa Mrombo jijini Arusha, mwenye uwezo wa kipekee wa kiakili juzi alianza rasmi elimu ya awali katika shule ya mchepuo wa Kiingereza ya Pison iliyoko kata ya Sokoni 2 jijini hapa.

Akizungumza shuleni hapo baada ya kumpeleka mtoto huyo, mama mzazi wa mtoto huyo, Marcelina Asango, alisema amefurahi kuona ndoto ya mtoto wake imetimia.

Mama huyo alisema mtoto huyo alikuwa akitamani kusoma katika shule za mchepuo wa Kiingereza lakini tatizo lilikuwa kutokuwa na uwezo.

Asango alimshukuru mfanyabiashara Philemon Mollel, maarufu kama Monaban, kwa kuchukua jukumu la kumsomesha mtoto huyo.

"Jamani nashukuru mtoto wangu kuanza safari yake ya kutimiza ndoto za kusoma kwa kuwa alikuwa akitamani muda mrefu. Pia nawashukuru waandishi wa habari kwa kuibua suala hili kwenye vyombo vya habari na hatimaye tumepata mfadhili. Nimefurahi sana," alisema.

Monaban alisema baada ya kupata taarifa kuhusu mtoto huyo, alifika nyumbani kwao na alichukua jukumu la kumsaidia kwa kumpeleka katika shule ya watoto wenye vipaji maalumu ya mchepuo wa Kiingereza.

Mollel alisema akiwa mdau wa elimu, amekuwa akimuunga mkono Rais John Magufuli, kwa kuwasaidia watoto wenye vipaji maalumu wasiokuwa na uwezo na kwamba huyo ni mtoto wa tatu kumsaidia lengo likiwa kuhakikisha wanatimiza ndoto walizojiwekea.

Aliwataka wadau mbalimbali wa elimu kumuunga mkono katika kumsaidia mtoto huyo, ili atimize ndoto zake.

"Mtoto huyu tayari ana akaunti yake ambayo kwa yeyote atakayeguswa kumsaidia atatuma hela kupitia akaunti hiyo na fedha hizo zitapelekwa shuleni kwa ajili ya mtoto huyu kutimiza ndoto zake," alisema Mollel.

Mkuu wa Shule ya Pison, Gilbert Sarungi, alisema shule hiyo iko tayari kumsaidia mtoto huyo kutokana na uwezo mkubwa wa kiakili alio nao kulingana na umri wake.

Aidha, alisema wana imani kubwa kuwa mtoto huyo atafanya vizuri zaidi ka-




Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo (kushoto), akijadiliana jambo na Mkurugenzi wa Jiji hilo, Dk. Maulid Madeni, baada ya kukagua zoezi la wananchi kusajili laini za simu kwa alama za vidole katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Wajumbe kamati ya madini watumbuliwa

**Na Allan Isack, SIMANJIRO**

WAJUMBE wawili wa kamati ya usuluhishi kitalu "B" Opec kwenye machimbo ya madini ya Tanzanite, mji mdogo wa Mirerani, Simanjiro mkoani Manyara, wameondolewa kwenye nafasi zao kwa kukiuka taratibu za kazi.

Kaimu Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Kimadini wa Simanjiro, Mhandisi Castro Maduwa, aliyasema hayo juzi Mirerani wakati akizungumzia na waandishi wa habari ofisi kwake.

Mhandisi Maduwa aliwataja wajumbe hao kuwa ni Elisafi Lema na Yusuph Mnyoti.

Alisema ametengua nafasi zao na hawataruhusiwa kujihusisha na shughuli zozote za kamati hiyo ndani na nje ya eneo tengefu la Mirerani tofauti na hapo watakuwa wanafanya kosa la jinai.

"Katika kutekeleza majukumu ya kazi zao walifanya makosa ambayo yamesababisha tuwachukulie hatua ya kuwaondoa kwenye nafasi zao," alisema Maduwa.

Alisema mchakato wa kuwapata wajumbe wengine wawili utaanza muda siyo mrefu kwa watu kujaza nafasi hizo mbili ili kuwapata wajumbe wapya.

Kwa mujibu wa Maduwa, wamechukua hatua hiyo kwa kuwa kamati ya usuluhishi ipo chini ya Mamlaka ya Kamishna wa Madini na kwa sasa inatambulika kama Tume ya Madini kwa mujibu wa kanuni maalum za uchimbaji wa tanzanite Mirerani za mwaka 2002.

Mmoja wa wajumbe waliotumbuliwa, Lema, aliwashukuru wajumbe waliomchagua na viongozi wa madini waliomtumbua.

Lema alisema ameshukuru kitendo cha kupumzishwa katika shughuli hiyo, ambayo alisema lawama ni lazima zitolewe wakati uamuzi unapotolewa huwezi kuwapendeza watu wote.

Mjumbe mwingine, Mnyoti, alisema ameondolewa kwenye nafasi hiyo bila hata viongozi wa kamati yake kuambiwa.

# Viongozi wa vitongoji, mkandarasi kuhojiwa

**Na Godfrey Mushi, SAME**

VIONGOZI wa vitongoji, wataalamu waliohusika katika ujenzi wa mradi wa maji wa Vumari wilayani Same na mkandarasi aliyepewa kazi hiyo, wanasubiri kuhojiwa na kamati maalum iliyopewa kazi ya kuchunguza madai ya udanganyifu katika utekelezaji wa mradi huo.

Watu hao wanahojiwa kutokana na maelekezo ya Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, aliyetoa siku tano kufanyika kwa uchunguzi huo.

Alipotafutwa jana kuthibitisha taarifa za kuhojiwa kwa baadhi ya watu hao, Senyamule amekiri kuhojiwa kwao lakini akasema kazi hiyo alishaiachia kamati ya uchunguzi.

"Kama kamati itaona kuna umuhimu wa kuwahoji itawahoji kwa mujibu wa taratibu, kama mradi ulikuwa kwao kuna kila sababu ya kupata maoni yao ili kujua ulikwamaje kwa miaka yote. Mimi nilishaunda kamati maalumu ya kuchunguza madai ya udanganyifu katika utekelezaji wa mradi wa maji wa Vumari ambao ulikuwa unatarajiwa kuhudumia vijiji 10," alisema.

Juzi, Mkuu huyo wa Wilaya alisema uamuzi wa kuundwa kamati hiyo unatokana na taarifa za udanganyifu kuwa mradi umekamilika kwa asilimia 80 na vitongoji vinavyopata huduma kwa sasa ni saba kati ya 10, wakati taarifa za serikali zinaonyesha uhalisia wa kitongoji kilichofikiwa na mradi huo ni kimoja tu.

Senyamule alinukuliwa na Nipashe akisema: "Nimeipa kamati ya uchunguzi muda wa siku tano kuja na majibu, hata hivyo niliwaambia wahusika kwamba haiwezekani tukavumilia, tayari tumechukua hatua kunusuru mradi wa maji wa Vumari ambao unatekelezwa kwa fedha za serikali.

"Kimsingi huo mradi ulikuwa wa vijiji 10 na ulikuwa ukitekelezwa kwa fedha za umma tangu wakati wa utawala wa serikali ya awamu ya nne na mpaka serikali ya awamu ya tano chini ya Rais Dk. John Magufuli inaingia madarakani hadi kufikia sasa mradi huo haukuweza kuisha kwa wakati."

Mradi huo wa maji ulitengewa na serikali zaidi ya Sh. milioni 870 na kisha kukwama kwa zaidi ya miaka miwili kutokana na ukata wa fedha kufikia mwaka 2017.

Mradi huo ulisimama tangu Juni mwaka 2015 na ukaendelea tena mwaka 2017.

Kuchelewa kukamilika kwa mradi huo kunadaiwa kusababisha wananchi zaidi ya 3,700 kupoteza muda mwingi kutafuta maji, badala ya kufanya shughuli za kiuchumi.

# Wataka kurudiwa uchunguzi mtoto aliyebakwa

**Na Mwandishi Wetu, HAI**

WANAHARAKATI wa haki za binadamu mkoani Kilimanjaro, wameanzisha mchakato wa kuzishawishi mamlaka zinazohusika na udhibiti wa masuala ya ukatili wa kijinsia, kuridhia kurudiwa kwa uchunguzi wa kitabibu dhidi ya tuhuma za kubakwa mara kadhaa mwanafunzi wa darasa la sita katika Wilaya ya Hai.

Wakili maarufu mkoani Kilimanjaro ambaye ni Mkurugenzi wa Shirika la kiraia la Kwieco, Elizabeth Minde, alisema jana kuwa tayari wameanza mazungumzo na baadhi ya mamlaka hizo ikiwamo Idara ya Ustawi wa Jamii na Polisi.

"Tunataka uchunguzi dhidi ya mwanafunzi huyo wa darasa la sita anayeishi huko Masama Mbweera urudiwe ili haki ya mtoto ipatikane. Tunazo taarifa kwamba wako watu wanafanya ujanja ujanja kupindisha ushahidi na tunaomba pia mamlaka nyingine zifuatilie sakata hilo kujua mwenendo wake," alisema Minde.

Mwishoni mwa mwaka jana, kuliibuliwa tuhuma za ubakaji dhidi ya mwanafunzi huyo kuhusishwa kimapenzi na mzee wa miaka 80, mkazi wa Kijiji cha Masama Mbweera.

Desemba 30, mwaka jana, Obed Ndosi maarufu kama Ulong'a, mkazi wa Kijiji cha Masama Mbweera, alipandishwa kizimbani katika Mahakama ya Wilaya ya Hai akikabiliwa na shtaka la kumbaka mwanafunzi huyo wa darasa la sita.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, Ulong'a anadaiwa kutenda kosa hilo kinyume na kifungu 130 (1), (2), (e) na 131 (1) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 cha Sheria iliyofanyiwa Marejeo Mwaka 2002.

Katika hati ya mashtaka iliyosomwa mahakamani hapo na Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Lobulu Mbise, inadaiwa kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo katika Kijiji cha Masama Mbweera Desemba 8, mwaka jana kwa nyakati tofauti.

Mwanafunzi huyo wa darasa la sita anayedaiwa kubakwa kwa nyakati tofauti na Ulong'a ana umri wa miaka 13.

Kesi hiyo namba 333 ya mwaka 2019, inasikilizwa na Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Devotha Msofe.




Baadhi ya watoto wenye mahitaji maalumu (wanaoishi na viusi vya Ukimwi) wilayani Siha, mkoani Kilimanjaro, wakifurahia zawadi ya maziwa waliopatiwa na Taasisi ya Mtandao wa Wasanii wa Injili Tanzania (TAGOANE). Taasisi hiyo pia imewakatiwa bima ya afya watoto 100 wenye mahitaji maalumu, wilayani humo, ili waweze kupata huduma za tiba na kukabiliana na changamoto za gharama za matibabu. **PICHA: JAMES LANKA**

# Mfanyabiashara aliyefia gesti azikwa

**Na Mwandishi Wetu, MWANGA**

SAFARI ya mwisho duniani ya mfanyabiashara na mmiliki wa mabasi ya Sahara, Abdalah Msangi (47), aliyefia katika nyumba moja ya kulala wageni mjini Moshi, ilihitimishwa jana baada ya kuzikwa nyumbani kwao Ndorwe-Usangi, mkoani Kilimanjaro.

Msangi alikutwa akiwa ameshafariki dunia katika moja ya nyumba ya wageni iliyopo Mtaa wa Dar es Salaam, mjini Moshi.

Mfanyabiashara huyo alisafirishwa juzi kupelekwa nyumbani kwao Ndorwe, kwa ajili ya mazishi na jana familia yake, ndugu, jamaa na marafiki walimhifadhi rasmi katika nyumba yake ya milele.

Juzi, Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Kilimanjaro, James Manyama, alithibitisha kuwa mfanyabiashara huyo kabla ya kifo chake, alikuwa na rafiki yake wa kike chumbani lakini baada ya kuona mwenzake anaishiwa nguvu na kuanza kutokwa na povu puani na mdomoni alikimbia na kutokomea kusikojulikana.

"Huyu mfanyabiashara alikuwa na rafiki yake wa kike kwenye chumba cha wageni huko Dar es Salaam Street, baada ya kuona ameishiwa nguvu na kuanza kutokwa na povu mdomoni alitoroka," alisema.

Aidha, taarifa zaidi zilieleza kuwa baada ya polisi kupata taarifa na kufika eneo la tukio, walipekua gari la Msangi na kukuta dawa ya kienyeji ambayo makachero hao waliichukua kwa ajili ya kwenda kuifanyia uchunguzi.

Baada ya upekuzi huo kukamilika ndipo mwili wake ulipelekwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro ya Mawenzi kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

Mabasi ya Sahara yaliyokuwa yakimilikiwa na Msangi, yanatoa huduma za usafiri kati ya mikoa ya Arusha na Kilimanjaro na Dar es Salaam.

TUJIKUMBUSHE



Ukurasa 15

**M/kiti Chadema Kusini aanika mwelekeo wao joto la uchaguzi**

Bobi Wine sasa 'ingizo jipya' kumkabili Museveni 2021



Ukurasa 18



Ukurasa 19

**Uchaguzi 2020 watangaza nia urais Democratic wapukutika?**


# siasa

JUMATANO JANUARI 8, 2020

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




Ukurasa 14

**Kenya mchuano ufisadi, 'wajenga madaraja' vs Uhuru, Raila, Ruto**

UCHAMBUZI

# Jenerali Soleimani: Kamanda aliyeinyima usingizi Marekani

**Na Anil Kija**

MAREKANI imevuka mpaka katika ushindani wake na Iran kuidhibiti Mashariki ya Kati, kutokana na mauaji ya Jenerali Qassem Soleimani (62). Huyo ni mkuu wa vikosi maalum vya Al Quds, vinavyoendesha mapambano Iran inayosimamia eneo lote la Mashariki ya Kati.

Jenerali Soleimani aliuawa katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Baghdad akiwa njiani aliposhuka kwenye ndege, asubuhi ya Ijumaa Januari 3.

Makao Makuu ya Jeshi la Marekani yalisema kuwa Rais Donald Trump aliamuru 'kuchukua hatua za kujilinda na kuwalinda raia wa Marekani nchi za nje kwa kumuua' mtu ambaye kiongozi mkuu wa Iran, Ayatollah Ali

**INAENDELEA UK.16**



Jenerali Qassem Soleimani. **PICHA: MTANDAO**

**Vita ukatili jinsia kupitia moto aliyowasha Majaliwa** Ukurasa 20

UCHAMBUZI

# Kenya mchuano ufisadi, 'wajenga madaraja' vs Uhuru, Raila, Ruto

## • Mtihani kukamilisha Katiba Mpya ya 2013



Rais Uhuru Kenyatta.



Makamu wa Rais, William Ruto.



Raila Odinga. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

**Na Ani Jozeni**

MIAKA saba tangu kufikiwa makubaliano ya kubadilisha muundo wa serikali ambao Kenya imefuata tangu uhuru mwaka 1963, hatua zimeanza kuchukuliwa kuona kama inawezekana kuingia katika hatua nyingine ya suala hilo, huku maeneo tofauti ya nchi yakiwa na mawazo kinzani.

Hatua za sasa zinafuata mkasa katika uchaguzi mkuu wa 2017, ambao mgomo ulianza kutoka kwa wafuasi wa upinzani na majimbo nchini yenye wabunge, maseneta na wawakilishi upinzani kwa wingi zaidi, kususia biashara ambazo zina uhusiano wa karibu na Rais Uhuru Kenyatta. Ikaonekana kuwa hatua itakayofuana ni uasi.

Ndipo ilifuata hatua ya 'kupeana mikono' kati ya Rais Kenyatta na kiongozi wa upinzani Raila Odinga, ambayo kimsingi yalijikita katika maeneo mawili; kuanza kupambana na rushwa katika idara tofauti za serikali na kuweka mikakati mikubwa ya maendeleo.

Ni mikakati ambayo ilisimamiwa kwa karibu isivurugwe na makundi ya wala rushwa na kuchukua hatua kuhusu yasiyotekelezwa katiba mpya ya 2013.

Siyo jambo la kushangaza kuwa hatua hizo ziligubikwa na sintofahamu ya nani atamrithi Uhuru akimaliza muhula wa pili katika uchaguzi wa mwaka 2022, huku upinzani mkubwa kwa hatua hizo ukionekana kwa Makamu wa Rais, William Ruto.

Ilionekana kwa mfano kuwa, vita dhidi ya rushwa ilikuwa inalenga wafuasi wa Ruto au walioungana mkono kampeni zake na anaowatazamia kumsaidia katika kinyang'anyiro cha kupewa bendera ya chama tawala cha Jubilee kwa ajili ya uchaguzi mkuu 2022.

> Ni mikakati ambayo ilisimamiwa kwa karibu isivurugwe na makundi ya wala rushwa na kuchukua hatua kuhusu yasiyotekelezwa katiba mpya ya 2013.

Licha ya kuwa kazi ya ujenzi wa madaraja kati ya jamii tofauti za raia wa Kenya, inafanywa kwa pamoja kati ya Uhuru na Raila, kuna sintofahamu ya nafasi ya Raila katika uchaguzi mkuu ujao, kama ni mgombea tena au anawaachia viongozi wengine.

### DARAJA JIPYA?

Pia, kuna uwezekano usiowahi kuwa msimamo wa chama chochote, Uhuru awe mgombea mwenza wa Raila.

Mkakati huu wa 'kujenga madaraja' umekuwa ngome ya shughuli za kusimamia maendeleo na kujenga umoja wa nchi katika kipindi hiki, hasa kuanzia Agosti mwaka jana, na inavyozidi kwenda inaonekana kuna uwezekano wa kupiga kura nyingine ya maoni, kama mapendekezo ya 2013 yatekelezwe kwa mabadiliko ya ziada ya katiba, na muundo wa serikali.

Tayari Kenya imeshaacha mtindo wa jadi wa kuongozwa na rais akisaidiwa na Baraza la Mawaziri, halafu Bunge na pia kuteua wakuu wa mikoa na wilaya.

Waliunda mfumo uitwao 'county' ambazo kwa mfano wa Tanzania ni kama kuunganisha wilaya mbili kupata 'county' moja, hivyo mikoa iondolewe kuwe na 'county' takribani 50 au 55, kufanana na Kenya.

Katika mabadiliko yaliyoonekana kupitia Uchaguzi Mkuu wa 2017, wabunge mashuhuri zaidi na waliopata kuwa mawaziri waligombea nafasi za useneta na waliobaki wakagombea uwakilishi na orodha tofauti za viti maalum.

Mkakati wa BBI (Building Bridges Initiative), kimsingi unachukua sehemu kubwa ya wafuasi wa Raila na mkusanyiko wa Nasa kwa jumla, ingawa wapo wanaotaka Ruto arudi upinzani, kutokana na kusuguana na Rais wake, Uhuru.

Hiyo inamfanya awe mgombea wa mkusanyiko mpya wa upinzani, ambao kwa sasa wapo zaidi katika maeneo ya pwani na Magharibi ya nchi hiyo, wakati katikati ya nchi na kaskazini ni Jubilee.

Ruto hadi sasa ni kiongozi wa Jubilee na hasa anapigania kukubalika katikati ya nchi 'county' kadhaa tiifu kwa Uhuru na ambako kuna wanasiasa wengi tu wasiotaka kusikia lolote kuhusu Raila, hasa kiitikadi.

Haielekei kama itakuwa kazi rahisi kufika hatua hilo linaweza likawekwa mezani, kwani hadi kufikia Agosti mwaka jana, ilikuwa miaka sita tangu mapendekezo hayo yatolewe, lakini kamwe Bunge haikuweka muda wa kujadili.

### UFISADI

Baadhi ya wachunguzi wa habari wana shaka na mapendekezo yanayopunguza nguvu muundo wa serikali kwa jumla, kwani hata katika hizi 'county' mdudu wa wizi na ubadhirifu wa mali ya umma amejijenga, kutokana na uhuru tarajiwa wa kujiendesha wenyewe.

Kuna miradi ya kujenga mabwawa makubwa kukabiliana na uhaba wa mvua na hitaji la unyweshaji mazao na mifugo, ambako upitiaji wa miradi hiyo katikati ya mwaka jana ulibaini miradi hewa, mabilioni lukuki.

Inaelekea hata kwa wenye jukumu la kuandaa ajenda za kuchapishwa katika gazeti la kisheria la serikali kwa suala hilo hawaelewani ni kitu gani hasa kinatakiwa kufanyika.

Kwa mfano, viongozi au wenyeviti wenza wa kikosi kazi cha BBI, seneta Yusuf Haji wa Garissa na seneta Amos Wako (aliyelalamika juzi kukataliwa kuingia Marekani kwa tuhuma za rushwa) wanaripotiwa kuficha undani wa ripoti yao ya mwisho na wanaonya kuhusu taarifa za uzushi katika vyombo vya habari kuhusu suala hilo.

Ni matamshi yanayoashiria pia kwamba, kwa kiwango fulani wao kama wenyeviti wenza, wana uwezo wa kuamua nini kiorodheshwe na nini kiachwe, wakiwasiliana na wakuu wao wa vyama kitaifa.

Wakati inaaminika Raila anataka mapendekezo ya mwaka 2013 yaingizwe katika taarifa ya mwisho ya BBI kwa matazamio yatawekwa katika mkakati wa utekelezaji, wachunguzi wa habari wanasema hata katika 'kikosi kazi' cha BBI, mapendekezo hayo ni kaa la moto.

Rais Uhuru, naye anasemekana hana shauku ya kurudisha malumbabo makali ya kufikia katiba mpya, mwelekeo wake ni kwamba mapendekezo ya ziada (nje ya kubadili muundo wa Uwakilishi, Bunge na mikoa) yalifikiwa ili tu kupata muafaka. Anaungana na wengi wengine kutaka yaachwe tu na kusahaulika.

UNAMKUMBUKA SELEMANI MATHEW?

# M/kiti Chadema Kusini aanika mwelekeo wao joto la uchaguzi

• Apiga debe 'shime tujiandikishe'

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimekuja na mkakati unaolenga kuwapata viongozi bora wa kukiwakilisha, katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwaka huu.

Mkakati huo unatajwa na Mwenyekiti wa Chadema wa kanda hiyo, Seleman Mathew, ni wa kuwataka wanachama wenye nia ya kuwania uongozi katika uchaguzi huo kujitokeza mapema, ili wapimwe utendaji wao.

"Yaani ni kwamba, chama kinawataka wajitokeze mapema wapimwe utendaji wao katika maeneo wanayotoka, ili kuona kama wanafaa kuteuliwa na kukiwakilisha chama hicho, katika uchaguzi mkuu," anasema Mathew.

Mwenyekiti, aliyewahi kuwa mwanasoka nafasi ya ulinzi kwa vilabu vya Yanga na Tukuyu Star, anasema, wanachama hao ni wale wa ndani na nje ya kanda, ambao wana nia ya kuwania udiwani, ubunge ukiwamo wa viti maalum na hata urais mwaka huu.

"Wajitokeze mapema ili tujiandae mapema kwa ajili ya uchaguzi mkuu, mwaka huu 2020 ni uchaguzi mkuu na katika kanda yetu, tuna jumla ya kata 515 na majimbo 27 ya uchaguzi," anasema.

Mathew anafafanua kwamba, kanda hiyo inajumuisha mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma na kwamba viongozi wamekutana na kujadili jambo hilo na kuamua kuwaomba wanachama wanaotaka kuwania uongozi wajitokeze mapema.

Anasema, suala la kuwapima wanachama wao mapema ni la msingi kwa maendeleo ya chama hicho na kwamba ni muhimu kwa wenye nia ya kujitosa kinyang'anyiro; cha uongozi, wakazingatia hilo.




Mwenyekiti wa Chadema Kanda ya Kusini, Suleman Mathew (katikati), akizungumza katika mkutano wa chama hicho juzi mjini Mtwara. **NA MPIGA PICHA WETU**

### UTARATIBU

Mathew anataja utaratibu wa kugombea uongozi kwamba, mwanachama anayetaka udiwani, anatakiwa kuwasilisha kusudio lake kwa maandishi katika ofisi za chama katika kata husika na nakala kupelekwa wilayani, ambayo iko kata anayotaka.

"Anayetaka kugombea ubunge, awasilishe kusudio lake la kuwania kwa katibu mkuu kupitia kwa katibu wa kanda na nakala ya kusudio hilo awasilishe kwa katibu wa mkoa, ambao jimbo analotaka kugombea limo na kwa katibu wa jimbo husika analotaka kugombea," anasema.

Anasema, anayetaka kugombea urais anatakiwa kuwasilisha kusudi la kugombea kwa katibu mkuu, hivyo wanachama wote wenye sifa wanakaribishwa kutangaza kusudio la kugombea nafasi hizo.

"Tunatoa wito kwa wanachama wote walioko ndani na nje ya kanda yetu wenye nia ya kugombea nafasi za udiwani na ubunge ukiwamo wa viti maalum na urais, wajitokeze sasa ili wapimwe utendaji wao mapema katika maeneo wanayogombea," anasema.

> "Awamu ya hili linafanyika katika mikoa ya Njombe, Ruvuma, Lindi, Mtwara na Visiwa vya Unguja na Pemba.

### DAFTARI LA KURA

Mathew anasema, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Nec), imekuwa ikiboresha Daftari la Kudumu la Wapigakura kwa nyakati tofauti katika maeneo mbalimbali nchini, ili kupata taarifa sahihi za wapigakura kwa ajili ya uchaguzi mkuu ujao.

"Awamu ya hili linafanyika katika mikoa ya Njombe, Ruvuma, Lindi, Mtwara na Visiwa vya Unguja na Pemba. Tumefuatilia kwa ukaribu zoezi hili, lakini kwa bahati mbaya sana haliendi kama vile inavyotarajiwa.

"Tunataka wananchi wa Kanda ya Kusini na maeneo mengine wapate haki yao ya kujiandikisha na baadaye wapate fursa ya kupigakura kuwachagua viongozi wanaowataka katika uchaguzi mkuu," anasema.

Mathew anarejea Sheria ya Uchaguzi, kwamba inaruhusu daftari hilo kuboreshwa mara mbili kwa kipindi cha miaka mitano, hata hivyo anadai bado kasi haimridhishi.

"Kwa sasa uboreshaji huo unafanyika kwa kipindi kifupi sana cha siku saba, ambacho tunaona uboreshaji huu hautakuwa na mafanikio makubwa kwa sababu vyama vya siasa vimezuiwa kufanya siasa kwa takriban miaka minne sasa. Hivyo, hamasa kwa wananchi itakuwa ndogo," anasema.

Mwenyekiti huyo anawahimiza viongozi wa ngazi mbalimbali katika kanda na wanachama, kuhamasishana kwenye vitongoji na matawi, umma kwenda kujiandikisha katika daftari hilo.

Anasihi uhamasishaji usiwe kwa wanachama tu, bali hata wananchi wengine katika maeneo yao, ili nao waende kujiandikisha na hatimaye wapate haki yao ya kupiga kura katika uchaguzi mkuu ujao.

Anarejea taraifa alizo nazo akidai, uandikishaji kwa maeneo yote ya mkoa wa Lindi na Mtwara, utaanza Januari 12 hadi 18 mwaka huu na anafafanua:

"Kwa ratiba hiyo, ninawaomba wananchi mjitokeze kwa wingi ili mpate haki yenu ya kuchagua viongozi mtakaowataka katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 25 mwaka huu."

### KUSINI & RASILIMALI

Mwenyekiti huyo anasema, ukanda wa Kusini una rasilimali nyingi, ikiwamo gesi, makaa ya mawe, mazao ya bahari, korosho, kahawa, ufuta, mahindi, maharage, mbaazi, choroko.

Anasema, utajiri wa rasilimali hizo zinaweza kuwanufaisha wananchi wa Kusini na kukuza uchumi wao kwa jumla, jambo analoamini chama chake kikiingia madarakani, itahakikisha wahusika wananufaika na rasilimali zao.

Anataja mazao ya choroko na mbaazi bado yamekuwa na bei ndogo sana na wakati mwingine kukosa kabisa wateja, jambo analolalamika kuna pengo la uratibu kibiashara.

"Chadema tunaamini katika utawala wa majimbo, hivyo Kusini kama moja ya jimbo (province) baada ya ushindi katika uchaguzi mkuu, tutahakikisha suala matumizi ya rasilimali za kusini kupaumbele ni Kusini kwanza," anasema.

Anasema, utawala wa Jimbo la Kusini ndiyo utakaokuwa na wajibu mkubwa wa kusimamia rasilimali za Kusini, kwa kuwatafuta wawekezaji na masoko ya mazao ya wakulima wa huko.

"Tunaunga mkono pia malelekezo yaliyotolewa na Katibu Mkuu wa Chama John Mnyika ya kutekeleza na kusimamia vipaumbele vitano vya chama kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka huu," anasema.

Mathew anavitaja vipaumbele hivyo, kuwa ni: Kudai tume huru ya uchaguzi; kuendeleza Chadema ni msingi; maandalizi ya wagombea; Chadema 'digital'; na ilani ya uchaguzi.

# Jenerali Soleimani: Kamanda aliyeinyima usingizi Marekani



Maombolezo ya Jenerali Qassem Soleimani, nchini Iran. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**INATOKA UK.13**

Khamenei, alishasema kuwa ni 'shahidi (mfia dini) ambaye bado anatembea.'

Wakati utawala wa Rais Hassan Rouhani, ukiahidi kujibu vikali shambulio hilo, waandamanaji walisambaa jijini Baghdad na kwingineko kusherehekea shambulio hilo, kwani moja ya madai ya msingi ya waandamanaji ni kuondolewa kwa majeshi yote kutoka nje, kuvunjwa kwa vikosi vya kidini na kuweka misingi ya demokrasia halisi.

Mfumo wa utawala na siasa kwa jumla, pamoja na usimamizi wa uchumi katika nchi kama Iran, Irak na Lebanon na kwa upande fulani Syria, una misingi ya kidini, dhehebu na nafasi ya kijamii inayoendana na utii kidini.

### USHUJA A WAKE

Wachunguzi wa habari walianza mara moja kubashiri kuwa 'hali imebadilika,' kwani ni watu wachache katika taifa hilo la Uajemi waliokuwa na sifa au ushujaa hata miongoni mwa watu wa kawaida

> Mudavadi ana uwezo kutatua matatizo ya kiuchumi tunayokabiliana nayo nchini mwetu…anaweza kushughulikia ugumu wa ki-fedha unaotukabili.



Jenerali Qassem Soleimani. **PICHA: MTANDAO.**

au kujulikana nchi za nje, kama Jenerali Soleimani.

Alijenga jina lake katika vita vya miaka minane kati ya Iran na Iraq akiwa bado kijana mwaka 1980 hadi 1988, na kusahaulika kiasi fulani katika siasa na masuala ya ulinzi na usalama baada ya kutofautiana na Ali Akbar Hashemi Rafsanjani.

Wakati wa vita na Irak, alikuwa mwakilishi wa Imam Khomeiny (Kiongozi Mkuu wa Mapinduzi ya Kiislamu) na jeshi, au tuseme katika uwanja wa vita na mshauri wake wa karibu kuhusu vita inavyoendeshwa.

Akawa Rais Iran mwaka 1989 hadi 1997 na alipoondoka madarakani ndipo nyota ya Soleimani, ikaanza kupanda kwa kasi.

Wanaofahamu kwa undani kuhusu vita vya Iran na Irak wanaweza kupambanua chanzo cha tofauti kati ya Soleimani na Rafsanjani, kwani watafiti nchini Ufaransa waliainisha vita vimefikia tamati yake mwaka1989 hadi 1990, baada ya kampeni ya 'Kerbala V' Rafsanjani alikata tamaa.

Kazi kuu ya majeshi ya Iran ilikuwa ni kuteka eneo la kusini lenye maeneo ya maji yaliyotuama, hadi jiji la Basra ambako ni kubwa Kusini ya Irak na ndiyo maskani muhimu ya watu wa dhehebu la Shia. Iran ingeteka eneo hilo, ingejikusanyia wapiganaji wengi wa ziada miongoni mwa wafuasi hao, iteke maeneo mengine.

Ukiangalia alivyojipambanua katika jeshi la Iran na mapigano aliyokuwa akiendesha nchi za jirani hasa Syria na Irak au kusimamia vikosi tiifu kwa Iran vya Hezbollah nchini Lebanon, unaona kuwa Kamanda Soleimani angekuwa mmoja wa wale ambao wangempinga kwa nguvu zote Rafsanjani, kuhusu umuhimu wa kuacha mapigano na Iraq na kukubali amani.

Ni mwelekeo uliokuwa na nguvu miongoni mwa wanamapinduzi wa mstari wa mbele na ikachukua miaka mitatu mingine hali ya mstari wa mbele wa vita ya kuung'oa utawala wa Rais Saddam Hussein wa IraK iko pale pale.

Ilifikia mahali, hata utii wa askari wa chini vijana kukanyaga mitego ya mabomu ilipuke wafe, hivyo vifaru vya Iran vipite ukaanza kuingia shakani, ndipo Imam Khomeiny alikubali kusitisha mapigano, akidai ni kunywa 'kikombe cha sumu.'

Cha kushangaza ni kwamba, kifo cha Jenerali Soleimani kimekuja kutokana na mbinu wanayoitumia Iran katika ushindani na mapambano ambayo si vita vya wazi na Marekani waliyoitumia dhidi ya Iraq baada ya mapinduzi ya mwisho wa 1978 kuingia 1979.

Kwa zaidi ya mwaka mmoja, Iran ilikuwa inafanya mashambulizi ya kushtukiza mpakani na Iraq, halafu askari watimke. Iraq ikavumilia halafu ikapiga.

Kiongozi wao Saddam Hussein, aliagiza mashambulizi ya nguvu ili kuilazimisha Iran ifanye mazungumzo ya amani, mashambulizi ya kushtukiza mpakani yakomeshwe, kumbe anaingia katika mtego wa Khomeiny.

Alikuwa ameweka sera ya mashambulizi ya aina hiyo ili kuamsha ari za wa-Shia nchini Iraq kuamini serikali imedhoofika waingie harakati za kumng'oa Saddam - aliyekuwa katili dhidi ya wanaohujumu utawala wake au kudhaniwa wangefurahia hilo, ikiwa ni pamoja na kuwakata masikio wafuasi wa chama cha upinzani cha ki-Shia, al Daawa.

Nje ya hapo, Saddam alifanya mashambulizi makubwa dhidi ya Iran angekuwa ametangaza vita mwenyewe, hivyo Khomeiny akapata nafasi kutangaza jihad, vita ya kidini.

Soleimani alisimamia kufanya mashambulizi ya hapa na pale, hadi kufikia kuuawa kwa askari wa Marekani katika makambi ya kulinda maskani ya serikali jijini Baghdadl yasifumuliwe katika vita vya wanamgambo wanaosimamiwa na makundi tofauti ya maimamu, madhehebu kinzani.

Ndipo Marekani ikachukua hatua ya kupiga mabomu makambi vya vikosi mpakani mwa Syria na Iraq kwa pande zote mbili ambavyo vilikuwa vinaendesha mashambulizi dhidi ya makambi ya kijeshi ya Marekani.

Hapo ikazua hasira ya watawala Iran, walioaandaa maandamano makubwa kuzingira ubalozi wa Marekani jijini Baghdad, wakashambulia kwa kutupia moto maofisa wa ubalozi, ikabidi wachukuliwe kwa ndege za kiusalama.

Baada ya uvamizi nchini Marekani, ilifuatia shambulio la kushangaza la kigaidi la Septemba 11, mwaka 2001 nchini Marekani. Iran ilianza kuwa na nafasi maalum katika siasa za nchi hiyo baada ya utawala wa ki-Sunni kuanguka ukaingia wa ki-Shia, kama alivyokuwa akiota Khomeiny.

Wachunguzi wa habari wa Marekani wanasema, Iran ilikuwa inawasha moto kwa upande mmoja na kuzima moto kwa upande wa pili, yaani pale ambako kuna jeshi la wanamgambolenye nguvu, Iran inawatuliza, lakini kwa masuala mengine inachochea harakati, maandamano, mashambulizi, kutaka Marekani iondoke Iraq.

Baada ya shambulizi huko Kerbala (moja ya maeneo muhimu ya kidini ya wa-Shia) lililoua askari watano wa Marekani Januari 2007, wahusika wa vikosi vya Al Quds na kamanda huyo shupavu kulianza kusambaa.

> Rais ndiye mwenye mpira mikononi mwake, huenda anaweza kuutupa kwa Mudavadi.

### ASAKWA KWA FEDHA

Hadi kufikia Desemba 5, 2019 Jeshi la Marekani bado lilikuwa linatoa tangazo la kutolewa zawadi ya Dola milioni 15 kwa atakayetoa taarifa kuhusu mhusika wa Iran aliyepanga shambulio hilo, baada ya takriban miaka 12 kupita.

Katika hali kama shambulio limesahaulika, vikosi vya Quds vilianza mashambulizi mengine dhidi ya kambi za Marekani. Hatimaye, jeshi la Marekani lilipiga kambi na kuua askari 25, pia kujeruhi 55.

Mambo yakapamba moto, ikawa ni suala la kitaifa kwa viongozi wa nchi hizo mbili, ndipo ikaja mkasa wa ubalozi wa Marekani jijini Baghdad ulizingirwa, ukavunjwa na moto kutupwa maeneo tofauti.

Rais Trump alitoa onyo kuwa, Iran italipa gharama kwa mashambulizi dhidi ya ubalozi, hivyo akatia saini amri ya kuuawa Kamanda wa Quds ambaye ni mtu maalum kwa Jeshi la Marekani tangu mwaka 2007, asiyesahaulika.

# ZEC na darasa la maana halisi ya uchaguzi ulivyo



Homa ya uchaguzi ilivyowahi kutokea Zanzibar. **PICHA: MTANDAO**

**Mwandishi Wetu**

UCHAGUZI hasa wa viongozi katika nchi ni utaratibu (mchakato) rasmi unaoendeshwa kwa mujibu wa sheria kuwawezesha wananchi kufanya uamuzi kwa njia ya kuwapigia kura kuwachagua watu ambao wanawataka kuwaongoza kwa kipindi maalum.

Uchaguzi ni utaratibu wa kawaida wa demokrasia wa kuwapata wawakilishi wa kisiasa ambao umekuwa ukitumika tangu karne ya 17.

Kuna aina tatu za msingi za uchaguzi zinazotumiwa kuwapata viongozi kulingana na mfumo unaotumiwa na nchi husika. Aina hizo ni Uchaguzi wa Rais, Uchaguzi wa Wawakilishi katika Baraza la Kutunga Sheria na Uchaguzi wa Viongozi wa Serikali za Mitaa. Vyama vya siasa kwa upande wao, navyo huendesha chaguzi ambazo zinajulikana kwa jina la 'Chaguzi wa Msingi zinazotumika kuwachagua wateuliwa wa vyama katika aina za uchaguzi ambazo zimetajwa hapo juu.

Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Sheria ya Uchaguzi Namba Nne ya mwaka 2018 Kifungu cha Tatu, inauelezea uchaguzi kuwa maana yake Uchaguzi wa Rais wa Zanzibar, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi au Madiwani na inahusiana na uchaguzi mdogo na uchaguzi wa marejeo. Uchaguzi katika nchi ya Zanzibar unafanywa kwa mujibu wa maelekezo ya Sheria ya Uchaguzi. Kifungu cha 34(1) kinaeleza kuwa "kwa mujibu wa masharti ya Katiba, kutakuwa na Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar ambao utafanyika kila baada ya miaka mitano".

Kifungu cha Pili, cha Sheria hiyo, kinaeleza kuwa kinaeleza kuwa Uchaguzi Mkuu chini ya kifungu kidogo cha kwanza, utajumuisha uchaguzi wa Rais, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani.

Pamoja na maelezo hayo, Sheria inaruhusu kufanyika kwa Uchaguzi Mdogo ambao kwa mujibu wa maelezo ya kifungu cha 40(1) cha Sheria ya Uchaguzi, uchaguzi mdogo utafanyika kutokana na mambo yafuatayo:-

- Kwa upande wa Rais, utafanyika kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha kwanza cha kifungu cha 34 cha Katiba;
- Kwa upande wa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, utafanyika kwa mujibu wa masharti ya Kifungu Kidogo cha Kwanza cha Kifungu cha 71 cha Katiba; na
- Kwa upande wa Diwani, utafanyika kutokana na kifo, kujiuzulu au sababu nyengine yoyote ambayo itamfanya diwani kupoteza sifa ya kuwa diwani.

Kwa kawaida Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, hufanya maandalizi ya uchaguzi mdogo baada ya kupokea taarifa rasmi kutoka katika mamlaka kama vile Baraza la Wawakilishi na Waziri anayehusika na masuala ya Serikali za Mitaa kwa kiti kilicho wazi cha Uwakilishi au Udiwani.

Vile vile, pale Tume itakuwa haikuridhika kabla ya kutangaza matokeo ya uchaguzi kwamba kulikuwa na kutokufuatwa kwa taratibu, matumizi mabaya au ukiukwaji wa taratibu za uchaguzi au pale ambapo kura za wagombea waliopata kura za juu imelingana. Tume itasimamisha au kufuta uchaguzi au sehemu yoyote ya uchaguzi na itatangaza siku nyengine ya kurudiwa kwa uchaguzi huo.

**Kwa mujibu wa tovuti ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar.**

# Bobi Wine sasa ‘ingizo jipya’ kumkabili Museveni 2021




Robert Kyagulanyi, maarufu kama Bobi Wine, katika nyendo zake za kisiasa. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mashaka Mgeta**

IMEKUWA kawaida katika Uchaguzi Mkuu wa Uganda kuwashuhudia washindani wawili wakongwe, Rais Yoweri Museveni wa National Resistance Movement (NRM), kupata ushindani wa karibu kutoka kwa Kizza Besyige wa chama cha Forum for Democratic Change (FDC).

Hali hiyo ilijitokeza katika Uchaguzi Mkuu wa Uganda uliofanyika kwa nyakati tofauti katika miaka ya 2001, 2006, 2011 na 2016. Mara zote hizo, Rais Museveni ameibuka na ushindi na kuendelea kutawala tangu alipoingia madarakani Januari 26, 1986.

Lakini, uchaguzi mkuu wa mwakani nchini humo, unatarajiwa kupata ‘ingizo jipya’ la Mbunge wa Kyaddondo Mashariki, wilayani Wakiso katika mkoa wa Kati, Robert Kyagulanyi, maarufu kama Bobi Wine.

Mbunge huyo ambaye ni msanii wa muziki wa pop, ameshatangaza nia hiyo, ingawa kwa kuandamwa na ‘kash kash’ nyingi za kisiasa.

Mwanasiasa huyo aliyezaliwa takribani miaka minne kabla ya Museveni kuingia madarakani, mara ya kwanza, hivi sasa akiwa na miaka 37, wakati Rais huyo aliyedumu madarakani kwa muda mrefu zaidi katika ukanda wa Afrika Mashariki, ikikaribia siku chache kuingia mwaka wa 34 sasa.

> “Ninajua hatari ninayokwenda kukutana nayo kukabiliana na Museveni, lakini nimepewa nguvu na ushawishi mkubwa na Waganda wanaoniona mimi ndiye kiongozi ninayewafaa.

Bobi Wine anayejulikana pia kwa jina la utani la ‘Rais wa Ghetto’ ni mkosoaji mkubwa wa Rais Museveni anayeungwa mkono na Waganda wengi hususani kundi la vijana.

Bobi Wine aliwekwa ndani kutokana na madai ya kushiriki tukio la kupigwa mawe kwa msafara wa Rais Museveni. Alikana kuhusika katika tuhuma hizo na akaachiwa kwa dhamana.

“Kwa niaba ya watu wa Uganda, nitashindana na wewe (Museveni) katika uchaguzi mkuu ulio huru na haki mwaka 2021,” Bobi Wine, alinukuliwa kutamka hayo jijini Kampala.

“Ninajua hatari ninayokwenda kukutana nayo kukabiliana na Museveni, lakini nimepewa nguvu na ushawishi mkubwa na Waganda wanaoniona mimi ndiye kiongozi ninayewafaa,” amekaririwa na shirika la habari la AFP.

Bobi Wine anajinasibu kuwa mtetezi wa watu maskini na kielelezo cha haki na demokrasia kwenye jamii.

Bunge la Uganda, liliondoa kifungu kinachoweka ukomo wa mtu anayetaka kugombea urais nchini humo kuwa na miaka isiyozidi 75, hali ambayo ilifungua milango kwa Museveni aliyezaliwa Agosti 15, 1944 kuwa mnufaika mkuu wa hatua hiyo, hivyo kugombea tena kwa mara ya sita.

Wanaomuunga mkono Rais Museveni katika kuwania kwake urais wanasema, kiongozi huyo anapaswa kubaki madarakani kwa maslahi ya utulivu na maendeleo ya kiuchumi ya nchi hiyo.

Badahi ya vyombo vya habari vilihamisha tafsiri ya siasa hizo kuwa vijana wa Uganda, wana utashi na Bobi Wine na ndio sehemu kubwa ya wananchi.

### ATAWEZA?

Kuna swali gumu linaloibuka kwamba, bado hajaweka mpango mpana wa namna atakavyoshughulikia kero sugu zinazoikabili nchi hiyo na watu wake, hasa ukosefu wa ajira na huduma duni za afya na elimu.

Bobi Wine anatamba kuwa, yeye ni kiongozi na kwamba Uganda ina wataalamu na wanataaluma wengi wanaoweza kushughulikia masuala ya kitaalamu.

Kwa upande wake, Rais Museveni amekuwa anaishusha thamani hoja hizo akimuita ni ‘msanii wa nyimbo kwenye klabu za usiku.’ Lakini, katika kipindi cha takribani miezi 18 kabla ya uchaguzi mkuu ujao wa 2021, amekuwa akizunguka nchi nzima akitoa pesa kwa makundi maalum ya kijamii, ikiwa sehemu ya operesheni ya kukuza utajiri wao.

Pamoja na kujiongezea umaarufu kwa Waganda na nje ya taifa hilo lililo mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Bobi Wine, anaendelea kupata misukosuko kisiasa ikiwamo kukamatwa na polisi mara kadhaa.

Kamanda wa Polisi mwenye dhamana ya operesheni, kwenye Kituo cha Polisi cha Kasangati, Supritendat Msaidizi (ASP) Andrew Angume, alijeruhiwa wakati wa makabiliano kati ya vyombo vya dola na wananchi (wanaomuunga Bobi Wine) kwenye Halmashauri ya Mji wa Kasangati.

ASP Angume, aliongoza timu ya askari kumkamata Bobi Wine na wanachama wengine wa vuguvugu la ‘nguvu ya umma’ walipokuwa kwenye mkutano unaohusu azma ya mwanasiasa huyo kuwania urais 2021.

Polisi walimshutumu Bobi Wine pamoja na Mbunge wa Manispaa ya Bugiri, Asumani Basalirwa na mwenzao wa Kawempe Kaskazini, Latif Ssebagala, kwamba waliitisha mkutano wa mashauriano hayo kinyume cha sheria za nchi hiyo.

Baada ya kuwakamata wabunge hao, walipelekwa kwenye Kituo cha Polisi cha Kasangati, wilayani Wakiso aliloshikiliwa kwa muda kasha alihamishiwa kwenye Kituo cha polisi Nagalama, wilayani Mukono.

Hata hivyo, ghasia zilizuka kati ya wafuasi wa ‘nguvu ya umma’ na polisi kiasi cha kusababisha wanausalama hao kufyatua risasi na mabomu ya machozi kuwatawanya.

ASP Angumea alijeruhiwa kwa bomu la machozi lililorushwa na askari mwenzake, likiwalenga ‘nguvu ya umma’.

Naibu Msemaji wa Kituo Kikuu cha Polisi cha Kampala, Luke Owoyesigyire, alithibitisha kujeruhiwa kwa ASP Angume, pasipo ufafanuzi wa kinai.

Mapambano hayo yalitokea, baada ya kutanguliwa na tukio alilopanga kulifanya jimboni mwake, lakini ‘likazimwa’ na askari polisi waliofika mapema kwenye eneo la tukio na kuwasambaratisha.

Waandamanaji walichoma matairi ya magari na kufunga barabara wakati polisi wakisaidiwa na magari ya kiaskari.

Polisi ilisema wanasiasa hai hawapaswi kufanya mkutano wa hadhara, inayolenga kusaka ‘makubaliano mbele ya umma.’

“Mkutano unapaswa kufanyika sehemu ya ndani kama inavyoelekezwa na Tume ya Uchaguzi,” anatamka msemaji wa polisi, Enanga, alipozungumza na waandishi wa habari.

Bobi Wine, aliwahi pia kukamatwa mara kadhaa alipofanya tamasha la muziki akiwa mbunge, katika matukio ambayo alipigwa marufuku tangu mwaka 2017.

Kwa mujibu wa sheria ya uchaguzi ya Uganda, mgombea urais mtarajiwa anapaswa kufanya mashauriano ya kutaka kuungwa mkono nchi nzima katika kipindi cha miezi 12, kabla ya kufanyika kwa uchaguzi mkuu.

JICHO URAIS MAREKANI...

# Uchaguzi 2020 watangazao nia Democratic wapukutika?

• Chasakwa kigingi kumng'oa Donald Trump



Julian Castro. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



Rais wa Marekani, Donald Trump.

**Na Ani Jozeni**

WACHAMBUZI wa habari wamekuwa na kazi ya ziada hivi karibuni nchini Marekani, kuangalia mazingira ya kusitisha mbio za kutafuta kupewa bendera ya chama cha Democratic, kwa uchaguzi wa rais nchini huko baadaye mwaka huu.

Moja ya sababu za mahangaiko hayo ni kuwa aliyeng'atuka katika mbio hizo, Julian Castro, alikuwa mtangaza nia pekee aliyebakia kwenye kundi hilo ambaye ni mzaliwa wa jamii ya ki-Hispania, wanaotokea Amerika ya Kusini kwa kuzaliwa.

Ili mtu aweze kugombea urais nchini Marekani, inabidi awe amezaliwa nchini humo, lakini kwa kawaida mizizi haiondolewi machoni.

Moja ya sababu za jambo hilo kuleta sokomoko au kujitafuta kwa kiasi fulani, ni hisia miongoni mwa wananchi wengi nchini humo wenye asili ya Kihispania kuwa itafika wakati nao watapata kiongozi anayeweza kuungwa mkono kugombea urais.

Inajulikana, kama ilivyo kwa watu wenye asili ya Afrika wenye asili ya Amerika ya Kusini, pia wanategemea chama cha Democratic, ndiko anakoweza kuibuka mtangaza nia mwenye uwezo na kukubalika na siyo chama cha Republican. Ina maana, hakuna uwezekano mwanasiasa kutoka jamii hiyo kujitokeza kuinua matumaini yao 2020.

Mwanasiasa huyo alikuwa Waziri wa Nyumba katika zama za Rais Barack Obama, pia alikuwa Meya wa Jiji la San Antonio, jimbo la Texas na hadi aking'atuka mbio hizo hapakuwa na mtangaza nia mwingine anayetokea jamii hiyo aliyethubutu kujipambanua.

> Castro alionyesha pia dhamira ya kulinda maeneo yanayokaliwa na watu wenye utamaduni wa asili, kulinda hifadhi za wanyama na hata wanaofugwa...

Alianza kampeni yake na kuisogeza mbele kwa kuelezea nia ya kutaka nchi ya Marekani, iwe ni taifa ambalo kila mwananchi ana umuhimu ambako kila mmoja anaweza kupata kazi nzuri, kuangaliwa afya na mahali panapofaa kuishi.

Wachambuzi wa habari wanasema, alipokuwa katika kinyang'anyiro hicho alikuwa kielelezo kwa utungaji sera kuhusu uhamiaji na kupambana na umaskini na kwa maana hiyo, unaweza kusema hata nchi za Afrika zimepoteza rafiki.

Katika ufafanuzi wao, wanasema kuwa Casto (mwenye umri wa miaka 45 ni mpenda siasa za kimaendeleo, ambao nchini Marekani wanaitwa 'waliberali' wakati barani Ulaya wanaitwa 'progressives' jambo ambalo ni kama kitu kilichosahauliwa na magazeti, redio na televisheni wakati wa kampeni yake.

Licha ya kuinua hisia kali wakati wa kampeni miongozi mwa wafuasi wa chama hicho katika majimbo tofauti, hakufaulu kuingia katika anga za watangaza nia watano wa juu, au kuwa gumzo miongoni mwa wafuasi wa chama hicho na jamii kwa jumla.

Kuondoka kwake ni hatua nyingine ya kupungua idadi ya watangaza nia kutoka jamii mbalimbali za taifa la Marekani na kuainisha ugumu kwa kurudia alichofanya Barack Obama, aliposhinda kinyang'anyiro cha kupata mgombea Democratic na kushinda uchaguzi wa 2008.

Akitoa waraka wa video kujionoa katika kinyang'anyiro hicho, mwanasiasa huyo alisema amefikia tamati kuwa ni wazi kwamba wakati haujafika kwake yeye au mtu kama yeye kuwa na umuhimu katika kinyang'anyiro hicho.

Alikuwa kwenye kampeni hiyo kwa mwaka mzima ambako alitembelea maeneo ya mpakani na makazi ya watu wasio na nyumba, akaona kiwango cha kutokuwa na shauku na kampeni yake miongoni mwa vyombo vya habari na wapigakura, akabwaga manyanga.

Alisema bado yuko katika harakati, licha ya kutosema kuwa baada ya kuondoka katika kampeni hiyo, anataka kufanya nini, hasa katika siasa akiainisha dhamira yake ya kuendelea na kampeni ya haki za msingi kwa wote.

Moja ya maeneo ambayo Castro aliyafanyia kazi wakati akiwa katika kampeni ni mauaji holela ya raia wa Marekani wenye asili ya Afrika au ya Amerika ya Kusini, tatizo ambalo limezidi kukua miaka ya karibuni.

Wakati Rais Obama alipokuwa madarakani, polisi katika miji au jiji mbalimbali ya Marekani, walikuwa na tabia ya kutumia kisingizio chochote kupiga risasi badala ya kumkamata mtu ili kumhoji, endapo ana asili ya Afrika. Alipoingia madarakani Rais Donald Trump, raia kutoka kusini ndiyo taabu.

Inatajwa pia kuwa Castro alikuwa anafikiriwa na aliyekuwa mgombea wa urais wa chama hicho mwaka 2016, Hillary Clinton ambaye alishindwa katika uchaguzi na Trump, kuwa Castro angeweza kuwa mgombea mwenza wake.

Moja ya michango yake iliyoleta mijadala katika chama hicho na kwingineko Marekani ni wazo lake kuwa wanaovuka mpaka bila vyeti vya kusafiria (hasa kutoka Mexico) wasitajwe kama wahalifu.

Inasemekana alichosema kulianza kuwa mtego kwa wagombea wengine wa chama hicho ambacho wapigakura wake wengi wanatoka katika jamii ya ki-Hispania, na baadhi wakakubaliana naye.

Castro alipokuwa Meya wa San Antonio, alianzisha mpango wa kupeleka watoto malezi kabla ya shule, prekindergarten, yaani wakiwa wadogo kabisa kuwezesha mama vijana wafanye kazi wajiendeleze kimaisha, kwani Marekani si rahisi kulipa mtu kusaidia malezi.

Alitoa hotuba katika mkutano mkuu wa uchaguzi wa chama hicho mwaka 2012 ambayo iliminua katika ngazi za siasa kitaifa, akitoa orodha ya mapendekezo kuhusu maeneo kama nyumba, elimu, usimamizi wa kesi za jinai, uchumi na kuainisha wapi mfumo wa usimamizi wa kazi za polisi unaweza kuboreshwa.

Castro alionyesha pia dhamira ya kulinda maeneo yanayokaliwa na watu wenye utamaduni wa asili, kulinda hifadhi za wanyama na hata wanaofugwa na kupunguza kwa kiasi kikubwa sumu inayotokana na risasi inayoingia katika maji.

Alitoa pendekezo la kuongeza kodi kwa mali za kurithi hasa wale wanaorithi mamilioni ya fedha Dola za Marekani, akijaribu kuondoa umaskini, kufuta kabisa hali ya kukosa chakula ambayo ilipanua kufahamika kwake kwa matabaka ya chini kabisa.

Hakuweza kuungwa mkono na matabaka ya kati, na licha ya kufaulu kuingiza kiasi cha dola laki nane za michango ya kuendeleza kampeni yake, hakupata viwango vya kuridhisha vya kukubalika kwa wapiga kura katika kura za maoni za hapa na pale kuhusiana na kampeni wa watangaza nia Democratic.

Alishiriki mijadala minne ya kwanza ya watangaza nia, lakini hakupata viwango vya kukubalika kwa wapigakura kuendelea nazo.

UCHAMBUZI

# Vita ukatili jinsia kupitia moto aliyowasha Majaliwa




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiwa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu (wa pili kulia), Mratibu Mkazi wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa Nchini, Alvaro Rodriguez (kushoto) na Mratibu wa Kitaifa wa Shirika la Wanawake Katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika ( WILDAF), Anna Kulaya , alipowasili kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, kuzindua Kampeni ya Siku 16 ya Kupinga Ukatili wa Kijinsia, mwaka jana. **PICHA: ZANZIBAR NEWS**

**Na Sabato Kasika**

LICHA ya juhudi mbalimbali za kukomesha vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto, bado vinaendelea kuwapo, hivyo serikali inalazimika kuja na mpango wa taifa wa kuvikabili.

Lengo la mpango huo, ni kupunguza kiwango cha ukatili kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2022, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2000.

Vilevile, linagusa Mkakati wa Taifa wa Maendeleo ya Jinsia (2005), Sera ya Maendeleo ya Mtoto (2008) na Sheria ya Makosa ya Kujamiiana ya Mwaka 1998.

Desemba mwaka jana, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akizindua kampeni ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, alisema serikali imeandaa Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto.

Anasema, utekelezaji wa mpango huo utachangia katika utekelezaji wa mipango na mikataba ya kikanda na kimataifa, kuhusu usawa wa kijinsia, uwezeshaji wanawake na wasichana pamoja na haki na ustawi wa mtoto.

Hivyo, anawaagiza wakuu wa mikoa wote wahakikishe wanasimamia uanzishwaji wa kamati za ulinzi wa wanawake na watoto kama inavyoelekezwa katika mwongozo wa uratibu wa mpango wa taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto na kutenga bajeti maalum.

> “Kwa ujumla, ni kwamba ukatili wa kijinsia ni unyanyasaji wowote unaofanywa na mtu dhidi ya mwingine bila kujali umri, maumbile, kabila, rangi, dini au mtazamo wa kisiasa.




Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Lilian Liundi, akizungumza kwenye ufunguzi wa kongamano la siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia lililofanyika katika viwanja vya TGNP Mtandao, Dar es Salaam mwaka jana. **PICHA: MTANDAO.**

Binafsi ninaamini kuwa pamoja na kwamba wakuu wa mikoa wamepewa jukumu hilo, bado jamii ina nafasi ya kushiriki kikamilifu, katika kusaidia kukomesha vitendo hivyo vya ukatili.

Kila mmoja ni mdau wa vita dhidi ya vitendo vya ukatili na anaweza kufanikisha mpango huo wa serikali, hivyo asiwepo wa kujenga na kudhani hausiki kwa lolote, bali ni mdau muhimu.

Hiyo inatokana na ukweli kwamba, vitendo vya ukatili vinatokea ndani ya jamii, hivyo inaweza kuwa inajua chanzo chake na kutoa taarifa kwa mamlaka husika, ili hatua za kisheria zichukuliwe.

Katika mazingira hayo, vitendo hivyo vinaweza kupungua kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2022, kama ambavyo serikali imepanga ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2000.

Kwa mujibu wa takwimu za Wizaya ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, mwaka 2017 pekee zaidi ya matukio 40,000 ya ukatili wa kijinsia yaliripotiwa.

Naibu mwenye dhamana, Dk. Faustin Ndungulie, aliyekaririwa na vyombo vya habari, akisema mwaka jana, alipozungumzia jinsi ya kutimiza Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG).

Anagusia zaidi lengo Namba Tano la Usawa wa Kijinsia ifikapo 2030, kwamba Umoja wa Mataifa unaendelea kuzihimiza nchi wanachama kuchukua hatua kuhakikisha ukatili huo unakomeshwa.

Tayari serikali imeanza kuchukua hatua hizo ambazo zilielezwa na Waziri Mkuu na kinachotakiwa ni kila Mtanzania kwa nafasi yake kushiriki katika vita ya kupunguza kama siyo kumaliza kabisa vitendo vya ukatili nchini.

Ikumbukwe, ukatili wa kijinsia ni hali ya kutenda vitendo viovu, vinavyodhalilisha, vinavyotesa, vinavyonyanyasa, vinavyokandamiza, visivyojali haki za kuishi kwa binadamu anaweza kuwa wa kiume au kike.

Vilevile ukatili wa kijinsia huja katika taswira nyingi ikiwamo vipigo, ubakaji, ukeketaji, ulawiti, matusi, lugha na vitendo vya udhalilishaji pamoja na kunyimwa fursa za kushiriki katika shughuli za kiuchumi.

Kwa ujumla, ni kwamba ukatili wa kijinsia ni unyanyasaji wowote unaofanywa na mtu dhidi ya mwingine bila kujali umri, maumbile, kabila, rangi, dini au mtazamo wa kisiasa.

Unyanyasaji huo unahusisha mambo mengi kama kumpiga mwanamke au mwanamume, kumnyima mtoto elimu, kumlawiti mtoto wa kike au kiume, kumbagua mtu katika mahitaji ya msingi na hata kuwanyima urithi.

Hayo yote mambo ambayo yamekuwa yakitokea ndani ya jamii, ndiyo maana nikasema kuwa kila mmoja ni mdau wa vita dhidi ya vitendo vya ukatili kulingana na nafasi yake kwenye jamii inayomzunguka.

Kwa maana hiyo lisiwe jukumu la serikali na asasi za kiraia tu, bali raia wote wana nafasi ya kufanikisha mpango wa taifa wa kukabiliana na vitendo vya ukatili kwa wanawake na watoto.



HABARI MBEYA

# Kampuni yabadili mbolea ya tumbaku

**Na Nebart Msokwa, CHUNYA**

KAMPUNI ya Petrobena East Africa Ltd inayosambaza pembejeo za kilimo nchini, imesema imebadili aina ya mbolea ya kupandia tumbaku baada ya ile ya awali kulalamikiwa na wakulima kuwa haifanyi vizuri.

Akizungumza wakati wa kukabidhi mbolea mpya kwa viongozi wa Chama Kikuu cha Wakulima wa Tumbaku wilayani Chunya (Chutcu), Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Peter Kumalilwa, alisema wameamua kubadilisha mbolea hiyo baada ya ile ya awali kutoendana na mazingira ya Chunya.

Alisema kutokana na kilio cha wakulima hao, kampuni imeamua kupeleka mbolea inayoendanana na hali ya hewa ya wilaya hiyo, ili kusaidia wakulima kunufaika na kilimo cha zao la Tumbuku kama ilivyokuwa awali.

"Tumeamua kufanya hivi kutokana na wakulima wa zao la Tumbaku kulalamika kuwa mbole ya awali iliyopelekwa kwenye vyama vyao vya msingi haikuleta mabadiliko kutokana na hali ya hewa, lakini kwa sasa tumeshaleta mbolea nyingine," alisema Kumalilwa.

Alisema licha ya kupeleka mbolea hiyo ya kubadilisha, bado kampuni inasubiria matokeo ya uchunguzi wa mbolea iliyochukuliwa sampuli na Mamlaka ya Udhibiti Ubora wa Mbolea Tanzania (TFRA), na kwamba endapo itabainika kuwa ilikuwa na madhara watawafidia wakulima.

Chutcu imempongeza mkurugenzi huyo kwa kusikia vilio vya wakulima hao kwa kuwabadilishia mbolea nyingine ili kuhakikisha wakulima hao wanapata mavuno mengi na mazuri kama walivyokuwa wamekusudia.

Makamu Mwenyekiti wa Chutcu, Onesmo Lupyana, alisema Kampuni ya Petrobena EA Co.Ltd ilisambaza mbolea na pembejeo mapema kwa wakulima tofauti na msimu wa kilimo wa mwaka jana ambapo zilifika kwa kuchelewa.

"Mwaka jana mbolea ilifika Januari na wakulima wakiwa wameshapanda mbegu kwenye vitalu, lakini mwaka huu wakala huyu kupitia amewahisha, ila changamoto ilikuwa ni hali ya huku kutoendana na mbolea hiyo," alisema Lupyana.

Alisema wakala wa kampuni hiyo alipopatiwa taarifa juu ya mbolea hiyo kushindwa kuendana na hali ya hewa ya wilaya hiyo, alikubali na kuamua kutafuta mbadala wake ili wakulima wasipoteze malengo yao waliyokuwa wamejiwekea.

Kaimu Ofisa Kilimo wa Wilaya ya Chunya, Joely Mkono, alisema wakulima wanatakiwa kuwa na subira kipindi hiki ambacho serikali inalifanyia ufumbuzi tatizo hilo lililoikumba nchi nzima kwa wakulima wazalishaji wa zao la tumbaku.

Alisema kwa sasa wakulima hao wanatakiwa kuendelea kutumia mbolea mbadala iliyosambazwa na wakala huyo ya kupandia ili kuhakikisha zao hilo linakua vizuri.

# NEMC kuteketeza tani 10 mifuko ya plastiki

**Na Innocent Ng'oko, MBEYA**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini lipo kwenye mpango wa kuteketeza zaidi ya tani 10 za mifuko ya plastiki iliyokamatwa hivi karibuni mkoani Songwe baada ya kuingizwa nchini kinyemela.

Meneja wa NEMC kanda hiyo inayojumuisha mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe na Songwe, Arnold Mapinduzi, alisema mifuko hiyo yenye tani 10.56 ilikamatwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ikiingizwa kinyemela nchini pamoja na kilo 67.68 za mifuko hiyo iliyokamatwa mkoni Songwe.

Mapinduzi akiwaomba wananchi wa maeneo ya mipakani hususani katika mpaka wa Tunduma mkoani Songwe na mpaka wa Kasumulu mkoani Mbeya kuhakikisha wanakuwa mabalozi wazuri katika kudhibiti mifuko ya plastiki.

Alisema baraza linaendelea na msako mkali kwa watu wasiowaaminifu ambao wamekuwa wakiingiza mifuko hiyo iliyopigwa marufuku nchini kinyemela kutoka nchi jirani au kutengeneza vifuko hiyo ndani ya nchi.

Alisema tangu kupigwa marufuku kwa mifuko hiyo, NEMC imekuwa ikikabiliana na watu wanaozalisha, kuingiza na kusambaza mifuko hiyo katika maeneo mbalimbali ya mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na kuwa hivi karibuni walifanikiwa kukamata mifuko iliyokuwa ikizalishwa katika moja ya kiwanda mkoani Mbeya.

"Nadhani unafahamu hivi karibuni tulifanikiwa kukamata mifuko iliyopigwa mafuruku na kuwatoza Sh. milioni 20 ambayo ilikuwa inazalishwa kinyemela na moja ya kiwanda mkoani Mbeya na pia tulifanikiwa kukamata mifuko ya plastiki kwenye chumba cha kuhifadhia vitu mbalimbali na kutoza faini," alisema Mapinduzi.

Aidha, alifafanua kuwa umefika wakati wananchi wa kawaida kuacha kutumia mifuko ya plastiki iliyopigwa marufuko na kuwa atakayekamatwa sheria inamtaka kulipa faini ya Sh. 30,000 hadi Sh. 200,000 au kifungo cha siku saba jela au vyote kwa pamoja.

Aidha, alisema kuwa NEMC inakusudia kuendesha msako mkali kwenye mabasi ya abiria na magari ya mizigo kutokana na baadhi ya magari hayo kukutwa yakiwa yamebeba mifuko ya plastiki iliyopigwa marufuku na serikali.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (kushoto), akiwa na baadhi ya viongozi wa kiwanda cha kusindika mchele cha kampuni ya Rapha Group, kilichopo Uyole jijini Mbeya juzi, ikiwa ni sehemu ya mkakati wake wa kukagua viwanda vilivyomo mkoani humo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Sido yabuni mashine 270 za wajasiriamali

**Na Innocent Ng'oko, MBEYA**

SHIRIKA la Viwanda Vidogo (Sido) mkoani Mbeya kupitia Kituo cha Uendelezaji wa Teknolojia, limefanikiwa kutengeneza mashine 273 kwa ajili ya wajasiriamali wadogo ikiwa lengo ni kuanzisha viwanda vidogo.

Msimamizi wa karakana Sido mkoani Mbeya, Japhet Kasonda, alisema kuwa mashine hizo ni kwa ajili ya kusaidia kuchakata mazao yanayolimwa Mbeya na mikoa jirani ya Iringa, Rukwa, Njombe na Songwe.

Alisema zaidi ya ajira 700 zimeweza kupatikana kutokana na utengenezaji wa mashine hizo katika maeneo tofauti ya mkoa wa Mbeya, ambapo wananchi wengi wamezinunua na kuanzisha viwanda vidogo ambavyo vimewasaidia kujipatia ajira.

Kasonda alisema kuwa miongoni mwa mashine zinazotengenezwa na kituo hicho hadi sasa ni za kuchakata mahindi zikiwamo mashine za kupukuchua mahindi, mashine za kukoboa mahindi, mashine kubwa na ndogo za kusaga unga pamoja na mitambo ya kisasa kwa ajili ya kusaga unga.

Alizitaja mashine zingeni kuwa ni za kuchakata alizeti zikiwamo mashine za kukamua mafuta, mashine za kuchuja mafuta, mashine za kuchekecha alizeti na utengenezaji wa matangi ya kisasa ya kuhifadhia mafuta ya alizeti.

Alisema baadhi ya mashine hizo zinazotengenezwa na kituo hicho zimebuniwa katika awamu hii ya tano zikiwamo za kuchakata mazao ya kahawa ikiwamo ya kukoboa kahawa mbichi, mashine za kukoboa kahawa kavu, mashine za kukaanga kahawa pamoja na mashine za kisasa za kusaga kahawa kwa ajili ya matumizi ya majumbani.

Aidha, alisema kituo hicho katika kuendeleza teknolojia zimesaidia kuwapo na ubunifu wa teknolojia mbalimbali za mashine za kisasa na mitambo ya kisasa katika kuchakata mazao ya malighafi mbalimbali ikiwamo mashine za kuchakata vyakula vya mifugo.

Pia kituo hicho cha teknolojia kimekuwa kikitengeneza mashine mbalimbali za ujasiriamali zikiwamo mashine za kufyatulia tofali za mkono na mashine za kufyatulia tofali kwa kutumia umeme ambazo kwa sasa zimekuwa na uhitaji mkubwa maeneo ya vijijini kutokana na maeneo hayo kufikiwa na umeme wa gridi ya taifa.

Alisema uamuzi wa wajasiriamali katika kuanzisha viwanda vidogo kutaongeza thamani ya mazao pamoja na kuchangamkia fursa za kibiashara ndani ya nchi na katika nchi jirani kutokana na kuzalisha bidhaa zenye ubora kutokana na mchango wa ubunifu na utengenezaji wa mashine za kisasa zinazofanywa na kituo cha kuendeleza teknolojia.





# Riba kubwa mikopo zamkwaza Mpango

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, ameshtukia riba kubwa inayotozwa na taasisi za fedha ambazo amesema zinawaumiza wananchi.

Sambamba na hilo, awewataka watumishi wa umma ambao wanaendesha maeneo ya huduma ndogo za fedha kuacha mara moja kabla serikali haijawabaini na kuwachukulia hatua kali.

Dk. Mpango aliyasema hayo jijini hapa alipokuwa akizungumza na vyombo vya habari kuhusu uendeshaji wa huduma ndogo za fedha nchini ambazo zimekuwa zikilalamikiwa kwa utozaji wa riba kubwa kwa wananchi.

Alisema kuwa moja ya changamoto nchini katika uendeshaji wa huduma ndogo za fedha ni riba kubwa za mikopo ambazo zimekuwa zikitolewa katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Alisema hivi sasa watoa huduma ndogo za fedha, wamekuwa na tabia ya kujipangia riba vile wanavyotaka ili kujipatia faida kwa haraka bila kujali wananchi wanaowakopesha.

"Huduma ndogo ya fedha nchini imekuwa kikwazo kwa wananchi wengi. Unakuta leo watu wanamkata mtu riba karibia hata mshahara wake mzima, hivyo lazima ufanyike utaratibu ambao utasaidia kuondoa suala hili. Lakini watumishi wa umma ambao wanaendesha huduma hizi wajitoe mara moja kwani haiwezekani wao ndiyo wawe wanawaumiza wenzao," alisema Dk. Mpango. Dk. Mpango alimwagiza Gavana wa Benki Kuu (BOT) kuhakikisha kuwa anaitisha mkutano wa nchi nzima utakaowajumuisha watoa huduma wote wa huduma ndogo za fedha.

"Lazima Gavana, uwaite watu wote wanaotoa huduma ndogo ya fedha ili mjadiliane nao namna ya uendeshaji wa huduma hizi. Si watu kutaka kutajirika kupitia migongo ya Watanzania maskini, lazima riba iwe nafuu kwa mkopaji ili ajikwamua kiuchumi na sio kunyonywa kama ilivyo sasa," alisema Dk. Mpango.

Kuhusu changamoto ya utengenezaji na usambazaji wa fedha bandia, Dk. Mpango alisema hilo ni jambao ambalo linamuumiza sana kwa kuwa linaathiri uchumi wa nchi.

"Mimi hawa watu ingekuwa maamuzi (uamuzi) yangu (wangu) ningekata mikono yao... wakati sisi tunapambana kupandisha uchumi wa nchi mtu mwingine anaingiza fedha bandia katika mzunguko. Huyo hana tofauti na yule ambaye mpo naye kwenye mtumbwi halafu anautoboa," alisema.



Mkazi wa Jiji la Dodoma, akikata kiu kwa maji ya dafu katika eneo la Mji Mpya. Dafu moja liliuzwa kwa bei ya 1,000/-. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Bila vyeti vya kuzaliwa hakuna kuandikishwa darasa la kwanza

**Na Ibrahim Joseph, DODODMA**

WAZAZI wametakiwa kuhakikisha wanapeleka vyeti vya kuzaliwa vya watoto wao wanaoandikishwa darasa la kwanza ili kuweka taarifa sahihi na kuwaepushia usumbufu wa kubadili majina baadaye.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kisasa, Jesca Mwarabu, alipokuwa akizungumza na wazazi wanaoandikisha watoto wao shuleni hapo kuanza darasa la kwanza katika mwaka huu wa masomo.

Mwarabu aliwataka wazazi hao kuhakikisha wanapeleka vyeti vya kuzaliwa vya watoto wao ili kuweka taarifa sahihi.

"Hatukatai kuwaandikisha watoto wenu, lakini kuna changamoto imekuwa ikijitokeza kwa baadhi ya watoto kudai kubadilishiwa majina na waliowaleta inakuwa inatupa shida sisi kwenye taarifa zetu," alisema.

Kwa mujibu wa mwalimu mkuu huyo, vyeti vinasaidia kuweka kumbukumbu sawa za mtoto kuanzia tarehe ya kuzaliwa jambo ambali linamsaidia pia mtoto husika.

Aliongeza miaka ya nyuma walikuwa wakichukua taarifa za kadi ya kliniki za watoto wanaoandikishwa, lakini kuna baadhi yao wamekuwa wakidai kuwa jina la mtoto aliloandikishwa halikuwa sahihi na kupeleka majina mengine.

"Kwetu sisi inatupa wakati mgumu kuanza kubadilisha jina la mtoto kwa sababu hatua zake ni ndefu za kufanya mabadiliko hayo na wakati mwingine huyo mtoto anakuwa alishafanya mtihani wa darasa la nne. Sasa kubadilisha jina inaleta shida," alisema Mwarabu.

Alisema kuna baadhi ya watoto wanakuwa wanaishi na bibi zao au shangazi na wakati wa kuwaandikisha wanatumia jina tofauti na lililoandikwa kwenye cheti za kuzaliwa.

Kwa wale wenye kadi za kliniki, alisema hawatapokewa mpaka mzazi au mlezi atakapoleta kivuli cha karatasi alizojaza fomu kwa msajili wa vizazi na vifo (Rita) huku cheti cha kuzaliwa kinaandaliwa.

"Nashukuru wengi wenu mmeitikia wito wa serikali wa kuwataka kuja na vyeti vya kuzaliwa vya watoto. Hakikisheni mliobaki mnafanya hivyo ili watoto wetu wasome," alisema.

Awali, baadhi ya wazazi walilalamika kuhusu watoto wao kukataliwa kuandikishwa shuleni hapo kwa sababu ya kutokuwa na vyeti vya kuzaliwa .

Mmoja wa wazazi, Zanura Faraja, alisema ana kadi ya kliniki ya mtoto anayetaka kumwandikisha na alisoma darasa la awali shuleni hapo, lakini amekataliwa kuandikishwa mpaka awe na cheti za kuzaliwa.

Hata hivyo, baada ya kikao, watoto wasio na vyeti vya kuzaliwa walitakiwa kufuata taratibu za kwenda ofisi za Rita kwa ajili ya kupewa vyeti hivyo kwa faida ya watoto wao kuwa na kumbukumbu sahihi katika maisha yao.

# Wakulima michikichi wapatiwa kibarua

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

SERIKALI imewaagiza wakulima wa michikichi kuandaa vitalu kwa ajili ya kupokea miche ya kisasa inayooteshwa kwa ajili ya kuboresha zao hilo linalopatikana kwa wingi mkoani Kigoma.

Miche hiyo imepangwa kuoteshwa katika moja ya vituo maalumu mkoani Kigoma kwa ushirikiano baina ya serikali, taasisi za umma na binafsi.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mazao kutoka Wizara ya Kilimo, Nyasebwa Chimago, alisema wizara kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali, imeamua kushirikiana nao ili kuona namna ya kutatua tatizo la upatikanaji wa mbegu bora za kisasa za zao hilo ambalo huzalisha mafuta ya mawese.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni kutaka kupunguza uagizwaji wa mafuta kutoka nje ya nchi kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

Alisema kila mwaka wamepanga kuzalisha miche milioni tano ambao ni mkakati uliopangwa ndani ya miaka minne.

"Tumejipanga kwenda na mkakati wa miaka minne na kila mwaka tumepanga kupanda mbegu milioni tano," alisema Chimago.


Alisema mkakati huo wa serikali unalenga kuokoa kiasi cha fedha ambacho hutumika kila mwaka kuagiza mafuta kila mwaka.

Chimago alisema mkakati huo ulianza mwaka wa fedha wa 2018/19 kwa lengo la kukuza upatikanaji wa mbegu bora za kisasa kwa ajili ya zao hilo ndani ya miaka minne.

Nyasebwa alisema upandaji wa miche hiyo wanashirikiana na Jeshi la Magereza Kwitanga, Ilagala na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Kambi ya Burombola na taasisi mbalimbali zinazojihusisha na masuala ya mbegu.

**"Tumejipanga kwenda na mkakati wa miaka minne na kila mwaka tumepanga kupanda mbegu milioni tano," alisema Chimago.**

HABARI ZANZIBAR



# Waziri ataka kulindwa majengo ya kihistoria

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Haji Omar Kheri, amesema bila historia hakuna utalii ulio hai utakaoweza kuleta tija kwa nchi na wananchi wake.

Akizungumza jana baada ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi mpya wa Kasri (jengo la historia) la Mwinyi Mkuu huko Dunga Wilaya ya Kati, Waziri Kheri alisisitiza haja ya kuyatunza na kuyalinda majengo ya kihistoria ili kuvutia watalii wengi zaidi kila mwaka.

Alisema haitoshi watalii kuja nchini na kulala kwenye hoteli nzuri, kula, kutembelea fukwe na kucheza baharini pekee, bali pia wanahitaji kuona mambo tafauti yanayokosekana katika nchi zao ikiwamo historia na majengo ya kale ya Zanzibar.

Kwa hivyo, alisema hatua ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, kuunda wizara maalum inayoshughulikia mambo ya kale na historia ni ya kupongezwa kwani itasaidia kukuza pato la nchi kupitia sekta ya utalii wa kimataifa.

Aidha, alisema kujengwa upya kwa Kasri la Mwinyi Mkuu kutaongeza harakati za kibiashara na kiuchumi kwa wananchi wa Dunga, Wilaya ya Kati na Mkoa wote wa Kusini Unguja, hivyo kupunguza umaskini.

"Jengo hili lilikuwa na ofisi za mtawala wa jadi aliyeitwa Mwinyi Mkuu miaka mingi kabla ya Mapinduzi, ni sehemu muhimu kwa historia ya nchi yetu ambayo kila mtu anapaswa kuijua, lakini sasa kuitumia pia kwa malengo ya kiuchumi kupitia utalii," alisema.

Waziri huyo aliipongeza Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale kwa kufanya matumizi mazuri ya fedha ilizopewa kwa ajili ya kuyafanyia matengenezo majengo yote ya kale na kuyerejesha kwenye hadhi ya awali.

Kwa upande mwingine, aliwataka wananchi wawe tayari kuunga mkono azma ya serikali kuhamasisha utalii wote badala ya kuyatunza majengo ya kale pekee. Pia alishauri kuyatembelea na kuyatumia.

"Ni aibu, ni fedheha na kashfa kwa Wazanzibari, iwe wa Kaskazini au Kusini, kuwa hawajafika wala hawayajui maeneo yaliyopo, wakidhani ni kwa ajili ya wageni tu. Tubadilike tuijue historia ya nchi yetu, tusisimuliwe na watu wasiokuwa wa hapa," alisisitiza.

Waziri huyo alisema asili ya maendeleo yote hayo ni Mapinduzi ya mwaka 1964 yaliyoongozwa na Rais wa kwanza wa Zanzibar, Hayati Abeid Amani Karume, ambayo dhamira yake ni kujenga ustawi wa wananchi wake kiuchumi, na kuwapa huduma nzuri za kijamii.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Khadija Bakari Juma, alisema matengenezo ya kasri hilo yanayofanywa na kampuni ya Yassin & Sons Ltd, yamegharimiwa kwa asilimia 100 na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Alisema kazi hiyo inafanyika kwa mujibu wa agizo la Ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) mwaka 2015/2020, ambayo pamoja na mambo mengine, imeelekeza kufufuliwa na kuimarishwa majengo yote ya kihistoria nchini.

Alisema awamu ya kwanza ya ujenzi huo ulioanza Mei 25, 2018 na kuchukua mwaka mmoja, imegharimu Sh. 385,229,869, na kwamba awamu ya pili ambayo ni kupandisha ghorofa itagharimu Sh. 802,474,303.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, alisema wananchi wa mkoa huo wameipokea vyema dhana ya utalii kwa wote, na kwamba wako tayari kutumia fursa za kuimarishwa maeneo ya kihistoria kwa kuleta matokeo chanya.



Mwalimu Mkuu wa Shule ya Kibeni katika Jimbo la Mkwajuni, Haji Simai Mcha (kushoto), akizungumza na Mwakilishi wa Mkwajuni, Ussi Yahya, aliyefika shuleni hapo, jana, kuangalia maendeleo ya ujenzi wa shule hiyo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## SMZ yafagiliwa utekelezaji wa malengo ya mapinduzi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar, imepongezwa kwa kufanikiwa kutekeleza malengo ya Mapinduzi ya Januari 12, mwaka 1964, kwa kuwapatia huduma muhimu za jamii yakiwamo majisafi na salama pamoja na matibabu bure.

Hayo yalisemwa jana na Waziri asiye na Wizara Maalumu, Juma Ali Khatib, wakati akizindua mradi wa uchimbaji visima na usambazaji majisafi na salama Kilindi Wilaya ya Chakechake Pemba ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 56 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Aliwataka wananchi wa kisiwa cha Pemba wasikubali kubabaishwa na kudanganywa, badala yake waelewe kuwa Mapinduzi ya Januari ndiyo yaliyowakomboa wananchi wa Unguja na Pemba.

Alisema huduma za majisafi pamoja na elimu na matibabu zilikuwa zikitolewa kwa njia ya matabaka, huku idadi kubwa ya wananchi wakishindwa kufaidika na huduma hizo.

"Mapinduzi ya Zanzibar ya Januari 12 mwaka 1964 ndiyo yaliyowakomboa wananchi wa Unguja na Pemba na sio uhuru wa Desemba 10...msikubali kudanganywa," alisema.

Khatib ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Ada Tadea, alizipongeza juhudi zinazochukuliwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, kwa kufanikiwa kufikisha huduma za maji hadi vijijini kwa asilimia 100 ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa ilani ya CCM.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Rais Ali Mohamed Shein imefanikiwa kusambaza huduma muhimu za maji hadi vijijini kwa asilimia 100 ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa ilani ya Chama Cha Mapinduzi," alisema.

Naye Waziri asiye na Wizara Maalumu, Said Soud, aliwataka wananchi wa kisiwa kidogo cha Kokota kuilinda miundombinu ya usambazaji wa majisafi na salama ambayo imesaidia kuwapatia huduma za maji.

Soud alisema juhudi za Rais Shein zinatakiwa kuungwa mkono kwa sababu visiwa vidogo sita vimeunganishwa na nishati ya umeme pamoja na majisafi kwa kutandaza mabomba chini ya bahari.

"Hayo ndiyo matunda ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo CCM imeahidi wananchi wake wote kufaidika nayo kwa kupata huduma muhimu za jamii," alisema.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba, Nishati na Maji, Salhina Ameir Mwita, alisema mradi wa Kilindi utanufaisha jumla ya shehia 14, huku watu 3,000 wakinufaika na majisafi na salama.

Alisema katika kisiwa cha Kokota Wete mradi huo umegharimu Sh. milioni 225.8, huku watu 507 wanaoishi katika kisiwa hicho wakinufaika.

Kabla ya mradi huo, wananchi walikuwa wakilazimika kuvuka bahari kwenda hadi Wete kuchota maji kwa kutumia madumu.

## Mwarobaini wa ajali wapatikana

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Zanzibar inakusudia kutunga sheria ya adhabu ya papo kwa papo kwa ajili ya kudhibiti ajali ambazo zimekuwa zikisababisha vifo vya wananchi wengi.

Hayo yalisemwa na Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Mustafa Aboud Jumbe, jana wakati akitoa maelezo kuhusu mradi wa ujenzi wa barabara ya Mtuhaliwa-Chokocho-Mtambile Mkoa wa Kusini Pemba.

Alisema matukio ya ajali nyingi za barabarani zimekuwa zikisababishwa na uzembe unaotokana na madereva kushindwa kufuata sheria za barabarani.

Alieleza kuwa wapo madereva wanadharau sheria na alama za barabarani, ambapo njia pekee ya kudhibiti ajali ni kuweka sheria kali ikiwamo kunyanganywa leseni kwa dereva aliyesababisha ajali.

"Tunafikiria kutoa adhabu za faini papo kwa papo kwa ajili ya kudhibiti ajali ikiwamo kuwanyang'anya leseni madereva wanaosababisha ajali hizo," alisema.

Naye Waziri wa Wizara hiyo, Dk. Sira Ubwa Mamboya, alisema mtandao wa barabara katika kisiwa cha Pemba umeimarishwa kwa kiasi kikubwa kwa lengo la kurahisisha huduma za usafiri.

Alisema mtandao wa barabara zenye urefu wa kilomita 1,561 umeimarishwa hadi vijijini, na kusaidia juhudi za wananchi katika kuimarisha kilimo.

"Tunaendelea na kazi za kuimarisha miundombinu ya barabara hadi vijijini kwa ajili ya kuimarisha huduma za mawasiliano na usafirishaji," alisema.

Mapema akifungua barabara hiyo, Aboud alisema ujenzi wa barabara hadi vijijini ni moja ya hatua muhimu ya kukuza uchumi na kuleta maendeleo.

Aliwataka wananchi ambao barabara imepita katika maeneo yao kuwa walinzi wazuri na kamwe wasikubali matukio ya uharibifu yatakayofanywa na watu wachache kwa sababu barabara zinatumia fedha nyingi za walipakodi. Ujenzi wa barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 5.6 umegharimu jumla ya Sh. milioni 570, na utasaidia sana maeneo ya kilimo cha karafuu.

**'Tunaendelea na kazi za kuimarisha miundombinu ya barabara hadi vijijini kwa ajili ya kuimarisha huduma za mawasiliano na usafirishaji," alisema.**

## Nyasa yajivunia ubora miundombinu

**Na Elizabeth Zaya, aliyekuwa NYASA**

MKUU wa Wilaya ya Nyasa, Isabela Chilumba, amesema katika kipindi cha miaka minne ya serikali ya awamu wa tano, wananchi wake wanajivunia mambo makubwa ambayo yamefanywa na serikali katika wilaya hiyo.

Chilumba alitaja mambo hayo ni pamoja na kutengenezewa meli tatu zinazofanya shughuli zake katika Ziwa Nyasa, ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami yenye urefu wa kilomita 67 kutoka Mbinga-Mbambabay.

Jambo jingine alilosema wanajivunia ni uboreshaji wa huduma muhimu za jamii ikiwamo uboreshaji wa miundombinu ya elimu, na afya.

"Kwa upande wa usafiri kwa sasa hatuna shida kama ilivyokuwa zamani iwe majini au kwa njia ya barabara, hapo nyuma barabara hii ya Mbinga hadi Mbambabay ilikuwa ni korofi sana, na tumeteseka kwa miaka mingi hasa kipindi cha masika haikupitika kwa urahisi, lakini kwa sasa tunashukuru serikali imetuona na sisi," alisema Chilumba.

"Leo hii sote ni mashahidi barabara inatengenezwa, haijaisha lakini mpaka hatua hii ni jambo la kushukuru sana. Katika sekta ya elimu na afya nako kuna mambo makubwa ambayo yamefanywa katika miaka hii minne ya awamu ya nne."

Katika sekta ya elimu, Chilumba alisema miongoni mwa mambo yaliyofanyika ni uboreshaji wa miundombinu ya shule ikiwamo Shule ya Sekondari ya Mbambabay.

Katika miaka minne ya serikali ya awamu ya tano, Chilumba alisema tayari wamejenga Hospitali ya Wilaya ya Nyasa pamoja na vituo viwili vya afya.

"Huwa najionea maajabu kwa sababu mimi ni mtumishi wa siku nyingi katika serikali za mitaa, nimeanzia ngazi ya chini kabisa hadi sasa nimekuwa mkuu wa wilaya, katika utumishi wangu huko nyuma sikuwahi kuona tumejenga hospitali 67 za wilaya, haya ni maajabu," alisema Chilumba.

Pia Chilumba aliipongeza Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) kwa maboresho makubwa inayoyafanya katika bandari zilizopo katika Ziwa Nyasa.

# Waliokosa madarasa 1,695 kuanza masomo

**Na Said Hamdani, LINDI**

WANAFUNZI 1,695 kati ya 13,916 waliofaulu mtihani wa kuhitimu darasa la saba mwaka jana mkoani Lindi na kukosa nafasi ya kuendelea na elimu ya sekondari mwaka huu kutokana na upungufu wa vyumba vya madarasa, hatimaye watajiunga na wenzao kuanza masomo yao baada ya shule zitakapofunguliwa mwezi huu.

Katika Mkoa wa Lindi wanafunzi 18,197 wakiwamo wasichana 9,622 na wavulana 8,575 walifanya mtihani wa kuhitimu elimu ya msingi mwaka 2019, kati yao 13,037, wavulana 6.736 na wasichana 6,301 ambao walifaulu.

Kaimu Katibu Tawala wa mkoani wa Lindi, Majid Myao, aliyaeleza hayo alipokuwa akitangaza uchaguzi wa wanafunzi wa kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza mwaka 2020, mbele ya wakurugenzi wa halmashauri nne kati ya sita katika kikao kilichofanyika mjini hapa.

Myao akizungumza katika kikao hicho kilichohusisha wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya Kilwa, Nachingwea, Lindi/Mtama na Ruangwa, alisema wanafunzi hao 1,6,95 wakiwamo wavulana 818 na wasichana 877, waliokosa nafasi katika chaguo la kwanza, wataendelea na masomo kupitia vyumba vilivyopangwa.

Alitaja vyumba vilivyopangwa kutumiwa na wanafunzi hao kwa wakati wakisubiria kukamilika kwa ujenzi wa madarasa kwenye shule husika, ni halmashauri hizo nne kati ya sita ni maabara, maktaba na mabweni.

Pia alisema Kilwa ndiyo inayoongoza kwa kuwa na idadi ya wanafunzi 962, wakiwamo wasichana 516 na wavulana 447, na kwamba inahitaji vyumba 25, ikifuatiwa Nachingwea 317, ambapo wasichana ni 187 na wavulana 130 na kuhitaji vyumba nane; Ruangwa 248 ambapo wavulana 136 na wasichana 112 ambapo vinahitajika vyumba saba; Lindi Vijijini/Mtama wanafunzi 167 wavulana 105 na wasichana 62, huku vikihitajika vyumba vinne.

Alisema chaguo hilo la pili ni utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu, Kasimu Majaliwa, alilolitoa kwamba wanafunzi wote wa kidato cha kwanza ifikapo juzi, wawe wameanza masomo.

Myao alisema lengo la kutumia vyumba vya maabara, maktaba na mabweni ni kuhakikisha wanafunzi hao wanaenda sambamba kimasomo na wenzao waliopata nafasi katika chaguo la kwanza.



Mmoja wa madaktari kutoka kwenye meli ya Jeshi la Wanamaji la Pakistani (kulia), akiwahudumia wananchi katika kambi ya matibabu bure, iliyoandaliwa na jeshi hilo, katika Shule ya Almuntazir, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mkwara wa DC wakimbiza wadhalilishaji wa watoto

**INATOKA UK. 10**

nakupita, mara wanaenda huku wengine kule, eti wanakwenda kuangalia TV na wengine wanakwenda kwenye dufu, lakini DC amepiga marufuku, hivyo imesaidia sana maana watoto hawadhururi ovyo."

Naye Sheha wa Shehia ya Konde, Mohamed Omar Abdallah, alisema mikutano aliyoifanya DC katika shehia zao wanaamini italeta mafanikio kwani wahalifu wataingiwa na hofu.

Kiongozi wa Dini katika Shehia ya Konde, Omar Khamis Hamad, alisema hawawezi kuficha haki kwani utakuwa unafanya dhuluma katika jamii, hivyo kuwaweka wazi wanaotenda vitendo vya udhalilishaji ni jambo zuri.

"Kila mmoja anapaswa kujikinga, haya matendo yako kila sekta lakini inapotokezea kafanya mwalimu wa madrasa linakuwa kubwa zaidi kwani wao ni viongozi na wanaaminiwa katika jamii," alisema.

Mratibu wa Tamwa, Pemba, Fat-hiya Mussa Said, alisema juhudi zinahitaji kwa kila mmoja kwa nafasi yake kupambana na matendo ya udhalilishaji na ukatili kwa wanawake na watoto.

"Kila siku tunatakiwa tubuni mbinu mpya ambayo itatusaidia kutokomeza matendo haya, kama hii mbinu aliyoitumia DC Micheweni ni nzuri sana, naamini itasaidia kama itaendelezwa," alieleza.

Mkuu wa Wilaya ya Micheweni Pemba, Salama Mbarouk Khatib, alisema walioна kuwa kutajwa kwa watuhumiwa hao hadharani ni njia moja wapo ya kusaidia kuondosha vitendo hivyo na ndio maana wakaamua kufanya mikutano kila shehia na kuwataja.

"Kila tukikaa matukio yanazidi, ndio tukabuni njia nyingine ya kufanya ambayo ni kuwataja hadharani," alisema na kuendelea:

"Hii imesaidia maana kila anayejijua ni muhusika wa vitendo hivyo, basi ameshakimbia, lakini tunaendelea kuwasaka na tukiwajua tutawataja, na hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao."

Alisema kuwa, watoto hushindwa kusema baada ya kufanyiwa udhalilishaji huo, kwani wahalifu huwatishia kuwaua na kuwachinja, jambo ambalo lilikuwa likiwatia hofu na kuendelea kudhalilishwa kila siku zinapoendelea.

"Tulipita shehia baada ya shehia na tulikuwa na kaulimbiu isemayo 'Pasuka Vunja Ukimya'. Kupitia kauli mbiu hii ilisaidia wananchi kuvunja ukimwa na kueleza ukweli, hali ya udhalilishaji ni kubwa katika jamii," alisema.

Alieleza kuwa lengo ni kutekeleza sera, sheria na miongozo ya Serikali, hivyo watashirikiana kuhakikisha ifikapo mwaka 2020 matendo ya udhalilishaji yanaondoka katika jamii.

Hivi karibuni DC Khatib alitangaza kuwa hataacha hata siku moja kuwatangaza hadharani wale wote wanaowaharibu watoto na wanawake kwa kuwadhalilisha hadi hapo watakapoacha tabia hiyo kwa hiari yao.

## HABARI KIMATAIFA

## Miguna Miguna apigwa 'stop' kuingia Kenya

**NAIROBI,** Kenya

WAKILI wa Kenya, Miguna Miguna, amedai kuwa mamlaka nchini Ujerumani imemzuia kuingia ndani ya ndege iliyokuwa inaelekea Kenya.

Alisema kuwa tahadhari imetolewa kwamba asiondoke Uwanja wa Ndege wa Berlin kuelekea Uwanja wa Kimataifa wa JKIA au nchi yoyote ya Afrika.

Ndege ya Shirika la Lufthansa aliyokuwa asafiri nayo kuelekea Kenya ilikuwa imepangiwa kuondoka nchini Ujerumani saa 5:20 na kuwasili Nairobi saa 3:25 usiku, majira ya Afrika Mashariki.

Hatua hiyo inajiri saa kadhaa baada ya mahakama ya juu nchini Kenya kutoa agizo la kuitaka serikali ya Kenya kutomzuia wakili huyo.

Serikali ya Kenya imesema kuwa itashughulikia suala hilo ili kumsaidia mwanasiasa huyo wa upinzani kurejea nchini siku ya Junanne, karibu miaka miwili baada ya kufukuzwa na kukimbilia Canada.

Taarifa iliyotolewa na Wizara ya Mambo ya Ndani ilieleza kuwa itazingatia agizo la mahakama la mwaka 2018 ambalo liliagiza serikali impatie Miguna stakabadhi za kumsaidia kurejea nchini humo.

Mahakama hiyo pia iliamuru maofisa wa kutetea haki za binadamu kuruhusiwa kuingia katika uwanja wa ndege kufuatilia mchakato huo.

Miguna alizaliwa katika kijiji cha Magina, katika Jimbo la Kisumu, Magharibi mwa Kenya.

Amekuwa kiongozi wa kundi linaloitwa National Resistance Movement (NRM, Vuguvugu la Taifa la Kupinga Serikali, ambalo liliundwa na muungano wa upinzani wa National Super Alliance siku moja kabla ya kufanyika kwa uchaguzi wa marudio Oktoba 26, 2017 ambao Raila Odinga alisusia.

Januari 30, siku ya kuapishwa kwa Odinga kuwa Rais wa wananchi, muungano huo uliorodheshwa kuwa kundi haramu na Waziri wa Usalama Dk. Fred Matiang'i.

Mwaka 1988, Miguna aliwahi kukamatwa na serikali ya wakati huo ya Rais Daniel Arap Moi. **BBC**

# Watu 35 wafariki dunia mazishi ya Soleimani

**TEHRAN,** Iran


WAKATI idadi kubwa ya wananchi wa Iran wakijitokeza kuuaga mwili wa aliyekuwa jenerali wa kikosi maalum cha jeshi la nchi hiyo, Qasem Soleimani, imeripotiwa watu zaidi ya 35 wamefariki dunia kwa kukanyagana.

Kadhalika, zaidi ya watu 40 wamejeruhiwa katika kisa hicho kilichotokea mjini Kerman, kwa mujibu wa ripoti hizo.

Soleimani alizikwa jana nyumbani kwake ambako mamilioni ya watu walikusanyika pembezoni mwa barabara kumuaga.

Mauaji yake yameibua hofu ya kuzuka kwa mzozo kati ya Marekani na Iran.

Soleimani alikuwa mtu wa pili mashuhuri nchini Iran baada ya kiongozi mkuu wa kidini, Ayatollah Ali Khamenei.



**Soleimani aliuawa katika mapambano ya anga na Jeshi la Marekani nchini Iraq siku ya Ijumaa, baada ya Rais Trump kutoa amri kuwa auawe.**

Marekani ilimchukulia Soleimani kuwa ni mtu gaidi na tishio kwa vikosi vyake vinavyohudumu eneo la Mashariki ya Kati.

Idadi kubwa ya waombolezaji waliyovalia mavazi meusi wamejitokeza kutoa heshima za mwisho ya kumzika.

Soleimani aliuawa katika mapambano ya anga na Jeshi la Marekani nchini Iraq siku ya Ijumaa, baada ya Rais Trump kutoa amri kuwa auawe.

Kundi kubwa la watu walijitokeza katika shughuli za mazishi mjini Tehran.

Iran iliapa kulipiza kisasi mauaji hayo ya kiongozi wao wa juu kijeshi na siku ya Jumapili, ilijitoa katika vizuizi vya matumizi ya nyuklia ya 2015.

Soleimani, alifariki akiwa na umri wa miaka 62, akiongoza kundi la jeshi la Quds, kazi yake kubwa ni kulinda usalama wa Iran na kuongeza ushawishi wa taifa hilo la Mashariki ya Kati.

Katika mji wake, Soleimani alitambuliwa kama shujaa wa taifa na alifahamika kama mtu wa pili ambaye ana nguvu zaidi katika taifa hilo akimfuatia kiongozi wa Iran Khamenei. Lakini sio raia wote wa Iran walimwona kuwa ni mtu mzuri.

Alikuwa kiongozi aliyeongoza jeshi kuua waandamanaji wengi mwishoni mwa mwaka 2019.

Alitumia fedha nyingi kujenga uhusiano na majeshi mengine ya Lebanon, Yemen, Iraq na Syria wakati ambao Marekani ilikuwa inaweka vikwazo vingi dhidi ya Wairan. **BBC**



Wajumbe wa Baraza la Umoja wa Mataifa wakiwa katika kikao wakiijadili Libya. **PICHA: REUTERS**

# Majeshi ya Marekani yagoma kuondoka Iraq

**WASHINGTON,** Marekani

WAZIRI wa Ulinzi wa Marekani, Mark Esper, amekanusha madai kuwa majeshi yake yanataka kuondoka Iraq, baada ya barua kutoka kwa Mkuu wa Majeshi wa Marekani kupendekeza waondoke.

Barua ambayo ilivuja mwishoni mwa wiki ilieleza kuwa Marekani itaondoa vikosi vya majeshi yake siku zijazo au wiki baada ya wabunge wa Iraq kuwataka waondoke. Esper alisema kuwa hakuna maamuzi yeyote ya kuondoka ambayo yaliondolewa.

Mkanganyiko huu wa vitisho ulikuja baada ya Jeshi la Marekani kumuua kamanda wa Jeshi wa Iran, Qasem Soleimani.

Jenerali Soleimani aliuawa katika mapambano ya anga huko Baghdad siku ya Ijumaa baada ya Rais wa Marekani Donald Trump kuamuru wafanye hivyo.

Mauaji hayo yameongeza mvutano katika ukanda huo, huku Iran ikitishia kulipiza kisasi. Inaonekana kuwa barua iliyotumwa na Brigedia Jenerali William H Seely, Mkuu wa Jeshi la Marekani katika kikosi kilichopo Iraq, kwenda kwa Mkurugenzi Msaidizi wa Opereshani ya pamoja, Abdul Amir.

Barua hiyo ilieleza kuwa: "Ndugu, kwa heshima ya Jamuhuri ya Iraq, na maombi yaliyotolewa na Bunge la Iraq, pamoja na Waziri Mkuu na Mkuu wa Operesheni za pamoja (Combined Joint Task Force) tutaondoa vikosi vyetu vya jeshi katika siku zijazo au wiki kadhaa ili kujiandaa na hatua nyingine".

"Hatua kadhaa zitafanyika ikiwa pamoja na kuwa na ndege nyingi angani wakati wa saa za usiku ili kuhakikisha kuwa wanaondoka kwa usalama na utaratibu unaofaa. Vilevile hatua hii itaondoa mitazamo kuwa labda tuna mpango wa kuongeza majeshi zaidi katika ardhi ya Baghdad," ilieleza barua hiyo.

Esper aliwaambia waandishi wa habari kuwa nchini Marekani: Hakuna hatua yeyote iliyofanywa kuhusu majeshi ya Marekani kuondoka Iraq. Sifahamu chochote kuhusu barua hiyo... Tunajaribu kufuatilia kujua barua hiyo imetokea wapi na ina maana gani? Kiufupi, hatujafanya maamuzi ya kuondoka Iraq".

Kiongozi wa juu wa Jeshi la Marekani, Mark Milley, alisema kuwa barua hiyo ilikuwa ya kimakosa kwa sababu ilikuwa imeandikwa vibaya, haikuwekwa sahihi na haikupaswa kutolewa.

Alisema barua hiyo ilikuwa ikisambazwa kwa ajili ya kuongeza maelezo, kutoka kwa wananchi wa Iraq.

"Barua ilitumwa kwa baadhi ya viongozi wa Jeshi la Iraq ili kuweka utaratibu wa usafiri wa anga pamoja na mambo mengine muhimu. Na barua ilitumwa kwao na kuanza kusambazwa kwa watu na sasa imeleta mtazamo wa uhasama."

Jenerali Milley aliendelea kusisitiza kuwa vikosi vya Marekani havitaondoka Iraq. **BBC**

# Waziri acharuka ulegevu usimamizi misitu nchini

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, ameelezea masikitiko yake kwa maofisa maliasili wa halmashauri zote nchini kwa kushindwa kuisimamia ipasavyo misitu iliyo chini ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi).

Hatua hiyo, amesema imesababisha misitu hiyo kuwa katika hali mbaya ya kuvamiwa na wananchi kwa kukata miti ovyo na kuanzisha makazi.

Kanyasu alisema hayo jana wakati akizungumza na watumishi wa Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) Kanda ya Ziwa mkoani Geita alipokuwa akikabidhi mizinga 200 kwa vikundi 10 kutoka majimbo ya Geita Mjini, Geita Vijijini na Busanda.

Kutokana na usimamizi huo hafifu. Kanyasu aliwataka watumishi hao kufanya doria badala ya kuwekeza nguvu nyingi katika mageti ya barabarani ambako kuna fedha.

Pia aliitaka TFS kuimarisha ulinzi katika maeneo ya misitu ya hifadhi ili kuwadhibiti wahalifu kabla ya kukata miti kwa ajili ya mbao na mkaa badala ya kuwekeza nguvu nyingi katika kukusanya mapato kutoka kwa wahalifu katika mageti yaliyo barabarani wakati misitu imeshaharibiwa.

Aidha, aliwataka maofisa maliasili wa halmashauri zote nchini kufanya kazi kwa kushirikiana na TFS kwa kulinda na kuhifadhi misitu badala ya kuiachia TFS pekee kwa kuamini kuwa hilo ndilo jukumu lake.

Kanyasu alisema kitendo cha kuwakamata wahalifu wakiwa na mazao ya misitu barabarani katika mageti hakisaidii kulinda na kuhifadhi misitu kwa vile uharibifu unakuwa tayari umeshafanyika.

Naibu Waziri alisema kuna misitu inayosimamiwa na vijiji, Tamisemi na serikali kuu kwa bahati mbaya lawama nyingi zimekuwa zikielekezwa kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kuwa imeshindwa kuisimamia jambo ambalo si kweli.

"Tumeamua kuhakikisha watumishi wote mnapata mafunzo ya kijeshi ili kuwasaidia kupambana na waharibifu huko msituni kabla hawajaleta athari za misitu yetu badala ya kusimama magetini huku misitu yetu ikiendelea kuteketea," alisema.

Kanyasu alisema hali hiyo ikiendelea ya kujikita kukamata wahalifu magetini, kuna siku misitu itaisha yote na hatimaye watakosa kazi ya kufanya.

Akizungumzia hatua ya halmashauri nyingi kuanza kuirudisha misitu iliyokuwa ikisimamiwa na serikali kuu, Kanyasu amesema hatua hiyo ni mbaya katika uhifadhi na inaonyesha kuwa wahalifu kuwazidi nguvu maofisa maliasili.

Katika hatua nyingine, Kanyasu aliwataka wananchi kuacha kuvamia maeneo ya hifadhi kwa kukata miti na kuanzisha makazi kwa vile athari za kuharibu misitu ni kubwa na zina gharama kwa watu wote.

Aliwaonya baadhi ya wananchi ambao wameanza kuvamia maeneo mapya ya hifadhi za misitu wakiamini kuwa Rais John Magufuli atawaonea huruma na kuwaachia kwa ajili ya kuanzisha makazi.



Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini, Stephen Masele, akizungumza na waandishi wa habari, mjini Shinyanga jana, kuhusu utekelezaji wa ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), katika kipindi chake cha miaka yake 10 ya ubunge. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Kesi ya mtuhumiwa wa 'Tereza' yakwama

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Kigoma, mkoani Kigoma, imeahirisha kesi inayomkabili mkazi wa Gungu Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Joseph Richard, ambaye anadaiwa kuwa mmoja wa wahalifu wa kikundi cha ujambazi maarufu kama 'Tereza'.

Hatua hiyo ilifikiwa jana, baada ya upande wa mashtaka kudai kuwa haujaandaa maelezo ya awali dhidi ya mashtakiwa.

Mshtakiwa huyo alifikishwa hapo mahakamani jana asubuhi akitokea mahabusu katika Gereza la Bangwe na kupandishwa kizimbani mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Eva Mushi.

Mshtakiwa huyo anakabiliwa na shtaka moja la kumshambulia Mwamini Hussein kwa kumkata na panga sehemu ya kichwani na kwenye mguu wa kushoto, na kumsababishia majeraha.

Upande wa Mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Clement Masua, ulidai kuwa hajaandaa maelezo ya awali dhidi ya mshtakiwa huyo, hivyo kuomba mahakama ipange tarehe nyingine kwa ajili ya kumsomea mshtakiwa maelezo hayo.

Hakimu Mushi alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi kesho kwa ajili ya kumsomea mashtakiwa huyo maelezo ya awali.

Aidha, Hakimu Mushi alisema mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu hadi hapo atakapopata mdhamini, na kuutaka upande wa mashtaka ujitahidi kuandaa maelezo ya awali siku hiyo, ili kesi hiyo imalizike mapema.

Masharti ya dhamana kwa mshtakiwa huyo ni kuwa na mdhamini mmoja mwenye barua ya utambulisho kutoka kwa ofisa mtendaji wa kata na mali isiyohamishika yenye thamani ya shilingi milioni mbili.

Awali akisoma hati ya mashtaka Wakili wa Serikali, Raymond Kimbe, alidai kuwa Agosti 8, mwaka 2019 majira ya usiku eneo la Muongwe Mkoa wa Kigoma, mshtakiwa alimshambulia Mwamini kwa kumkata na panga sehemu za kichwani na kwenye mguu wa kushoto na kumsababishia majeraha.

# Hati chafu yakwamisha fedha za mradi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MBUNGE wa Shinyanga Mjini, Stephen Masele, amebainisha kuwa maombi ya awali ya fedha za mradi wa ujenzi wa barabara kilomita 13 kwa kiwango cha lami mjini hapa kutoka Benki ya Dunia, yalikwama kutokana na Manispaa ya Shinyanga kuwa na hati chafu.

Masele ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais Bunge la Afrika (PAP), alibainisha hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari juu ya utendaji wake wa kazi kwa miaka 10 ya ubunge wake tangu mwaka 2010.

Alisema maombi ya awali ya ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita 13 kwa kiwango cha lami katikati ya mji wa Shinyanga, yalifanyika mwaka 2011, lakini kutokana na halmashauri kuwa na hati chafu yaligonga mwamba.

Hatua hiyo, alisema ilibidi wachukue hatua ya kuisafisha kwanza halmashauri hiyo, ndipo wakatuma maombi mengine na kupata mradi huo.

"Baada ya halmashauri yetu kupata hati safi ndipo tukapata mradi huu wa ujenzi wa barabara kutoka Benki ya Dunia na ujenzi wake ulianza mwaka 2013/14 chini ya Kampuni ya Jasco," alisema Masele.

"Sasa hivi mradi huu wa ujenzi umekamilika sambamba na kufungwa taa na mji wa Shinyanga umependeza na unakua kimaendeleo. Ndivyo nilivyokuwa nataka mji huu uwe," aliongeza.

Pia alisema kwa sasa yuko kwenye hatua za mwisho kupata ufadhili mwingine wa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kilomita 18, ili kukamilisha maeneo mengine ya mji ambayo hayana lami kabisa, zikiwamo kata za Mwasele, Ndala, Chibe, Bugweto, Kolandoto na Kitangili.

**Maombi ya awali ya ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita 13 kwa kiwango cha lami katikati ya mji wa Shinyanga, yalifanyika mwaka 2011, lakini kutokana na halmashauri kuwa na hati chafu yaligonga mwamba.**

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### VIWANJA /MASHAMBA

**Viwanja vinauzwa** Kibaha Misugusugu. Ukubwa ni mita 20 kwa 20 (400m2). Bei ni 2,000,000/- Milioni mbili tuu. (5,000/=1m2). Unaweza kulipa kwa awamu ndani ya miezi mine. Huduma zote zipo. Kwa mawasiliano: 0714 090009 / 0767 090008. Vimepimwa.

### MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MKOPO WA HARAKA KUTOKA ENTERPRISE FINANCE LIMITD (EFL).** Kwa mahitaji kama kulipa ada ya shule, kodi, kuboresha biashara, kumalizia tenda etc. Kwa maelezo zaidi piga 0758 112 332. Karibu EFL.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**au piga simu: 0782253676**


### CHETI KIMEPOTEA



**MTASI MWAIPOPO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba S.0108/0559 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa Mwaka 2012 katika shule ya Sekondari IFUNDA TECHNICAL.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kwenye kituo cha polisi kilicho karibu.

**Taarifa ya polisi: IR/RB/2216/2013.**

115575402

### CHETI KIMEPOTEA



**STEVEN MASHAURI SHADRACK** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba S.0333/0664 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa Mwaka 2014 kupitia MWANZA SEKONDARI.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kwenye kituo cha polisi kilicho karibu.

**Taarifa ya polisi: UD/RB/2503/2019.**

115575502

### UMOJA WA WAVUVI WADOGO WADOGO DAR ES SALAAM (UWAWADA)

Mwenyekiti wa **UWAWADA SALEHE MSEANI** anatangaza kupotelewa na **CERTIFICATE OF REGISTRATION NO. SO 8061** iliyotolewa tarehe **13/3/1995.** Cheti hicho kilitolewa na WIZARA YA MAMBO YA NDANI KWA WAVUVI WADOGO WADOGO. Hivyo usomapo tangazo hili na kuokota cheti hiki tafadhali kirudishe au piga simu namba: **0715 786591**. Taarifa ya polisi: **DAR/CEN/RB/350997/2019.**

115576102

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**Abbas Karim Khan** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Ford Ranger yenye namba za usajili **T 244 ARP.** Chassis namba **MNBBSFE407W638167** na engine namba **WLAT774290.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **KAH/TR /RB/ 05/2020.**

115576002

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**GEOFREY GODFREY KAHWILI.** Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki, yenye Namba: T448 BGJ, Chasis No: **LBRSPJB53A9001316,** Engine **No: CA905423.** Kadi ilipotea, na aliripoti kituo cha polisi ngara tarehe **11/11/2019** na kupewa No: **NGR/RB/2353/2019.** Kwa yeyote atakayeiona haipeleke kituo cha polisi kilichoko karibu naye.

115576602

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

SHABANI SALUMU anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 417 APZ aina ya Suzuki Maruti.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Taarifa ya Polisi: DAR/SEL/RB/563005/2019.

1155752

### CHAMPION AUCTION MART

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa niaba na mamlaka tuliyopewa na **MUCYO MICROCREDIT TANZANIA LTD** tutauza kwanjia ya mnada waadhara Nyumba na Dhama zilizowekwa kama dhamana ya mkopo yao, mteja/wateja wameshindwa kulipa mikopo yao kwa wakat ikwamujibu wa mikataba walioingia na taasisi husika. Mnada utafanyika kam aifuatavyo.

1) JINA LA MTEJA-AGNESS LUCAS KATUMA, DHAMANA YAKE – NYUMBA, MAHALI -BUHONGWA, MNADA UTAFANYIKA TAREHE 24/1/2020 SAA 6 KAMILI MCHANA
2) JINA LA MTEJA -REGINA FORTUNATUS MZAGA, DHAMANA YAKE -NYUMBA, MAHALI- MKOLANI NYAG'HINGI A, MNADA UTAFANYIKA TAREHE 24/1/2020 SAA 3 KAMILI ASUBUHI

**Masharti ya mnada**

i) Mshindi anatakiwa kulipa 25% ya kiasi atakachoshinda mara tu dalali atakapomtangaza kuwa mshindi na salio la 75% n ilazima ilipwe ndani ya siku 14 kutoka siku ya mnada
ii) Kiasi cha 25% kitakacho kuwa kimelipwa hakitarejeshwa endapo mshindi atashindwa kulipa kias ikilichobaki cha 75% ndani ya siku 14 toka tarehe ya mnada
iii) Gharama zote ikiwemo kubadilisha taarifa za nyarakani ni za mnunuzi

**Kwa mawasiliano zaidi piga 0753959568/0755244442**

115575702


***Uza, Chenye Thamani***

***Kubwa Kwa***

***Kutangaza Nasi***

***Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila

Nipashe

MWANGA WA JAMII



**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# ARTETA ASEMA ARSENAL SASA WAMEJIFUNZA

**LONDON,** England

MIKEL Arteta anafikiri Arsenal itanufaika baada ya kupelekwa puta na Leeds United Jumatatu kabla ya hasira zake za kipindi cha kwanza kuiimarisha timu na kuweza kupata ushindi.

Washikabunduki hao walipata ushindi wa 1-0 pale kwenye dimba la Emirates shukrani kwa bao la Reiss Nelson lililofungwa kipindi cha pili.

Arsenal walizidiwa na wageni hao katika kipindi cha kwanza, huku shuti la Patrick Bamford likigonga mwamba na golikipa Emiliano Martinez akiokoa hatari kadhaa langoni mwake wakati alipopigiwa mashuti 15.

Arsenal waliimarika kipindi cha pili na Arteta ana matumaini kwamba wachezaji wake watakuwa wamejifunza somo zuri kutoka kwenye mchezo huo.

"Sasa kwa hakika nimekuwa na amani, lakini tuliona timu mbili tofauti kabisa kutoka kipindi cha kwanza hadi cha pili," alisema akiiambia BBC Sport.

"Nilijaribu kuwaambia nini ambacho watakabiliana nacho na baada ya dakika 32 mambo yalibadilika, nafikiri. Tulibadilisha mtazamo wetu, muundo wa timu na kipindi cha pili tulikuwa tofauti kabisa.

"Wakati mwingine wanatakiwa kupata uzoefu kwenye mechi ngumu kama hii na namna gani ya kupambana.

"Nilitazama mechi nyingi za Leeds na walikuwa wakicheza kwa ushindani mkubwa kwenye kila mchezo. Lilikuwa jambo zuri kwa wachezaji wangu kujifunza kwa kile walichokipitia dimbani."

# Guardiola: Siwezi kufundisha United, Madrid

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amesema ni heri akaishi katika visiwa vya Maldives kuliko kuwanoa wapinzani wao wakubwa wa jiji moja kwenye Ligi Kuu England, Manchester United.

Timu hizo jana Jumanne zilikuwa zinakutana kwenye nusu fainali ya Kombe la EFL katika dimba la Old Trafford ukiwa ni mchezo wa kwanza.

Guardiola alikuwa akihusishwa na mpango wa kutua United kabla ya kutua Bayern Munich na baadaye City mwaka 2016 na kocha huyo wa zamani wa Barcelona akaenda kutawala soka la Uingereza akishinda mara mbili mfululizo taji la Ligi Kuu, EFL, FA na Ngao ya Jamii.

Alipoulizwa kama angeweza siku moja akaondoka City na kwenda kwa wapinzani wao, Guardiola – ambaye amekuwa akihusishwa na kutaka kuondoka hapo kwenye dimba la Etihad alisema – haiwezekani kabisa.

"Baada ya kuinoa City, siwezi kuwa kocha wa United. Kama ilivyo kama kwamba siwezi kuwa kocha wa Real Madrid," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari.

"Ni bora nikaishi kule Maldives kama sitapata ofa ya kuzinoa klabu nyingine. Maldives, kwa sababu hakuna kozi ya mchezo wa golf, lakini ni mahali pazuri tu."

Wakati City imekuwa kwenye kiwango kizuri tangu kutua kwa Guardiola, wapinzani wao United wamekuwa kwenye wakati mgumu.





# *Conte ajibu tuhuma dhidi ya kikosi, Lukaku*

**MILAN,** Italia

ANTONIO Conte amejibu tuhuma dhidi ya Inter na mshambuliaji wake nyota, Romelu Lukaku baada ya kikosi chake kubakia kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Italia, Serie A, ikiwa pointi sawa na Juventus.

Lukaku alifunga mara mbili wakati Inter ikiichapa Napoli 3-1 nyumbani kwao Jumatatu, baada ya Juve kupata ushindi wa 4-0 dhidi ya Cagliari mapema siku hiyo.

Baada ya kusherehekea ushindi wake wa 100 kwenye Serie A kama kocha, Conte aliamua kujibu shutuma kuhusu uimara wa mashambulzi ya kushtukiza ya Inter.

"Sidhani kama Inter ilicheza kwa kujilinda na kushambulia kwa kushtukiza, tulijaribu kusukumiza mashambulizi mbele kwa Napoli na tuliingia kwenye eneo lao katika kipindi chote cha mchezo," alisema Conte akiiambia Sky Sport Italia.

"Nawasikia watu mara zote wakizungumza kuhusu soka la mashambulizi ya kishtukiza, lakini timu hii inajua nini inatakiwa kufanya kila inapokuwa na mpira.

"Tunacheza kukijua kila kitu tunachotakiwa kukifanya wakati wote tukiwa dimbani. Bahati nzuri wapinzani wetu wanatuheshimu zaidi kuliko vyombo vya habari vinavyoona.

"Watu wanasema tunashinda ugenini kwa sababu tunacheza kwa kujilinda na kushambulia kwa kushtukiza, lakini hiyo sio staili yetu ya uchezaji."

Lukaku ambaye alisajiliwa na Inter kwa ada iliyoweka rekodi klabuni hapo, alifikisha mabao 14 kwenye Serie A baada ya kufunga mara mbili pale kwenye dimba la San Paolo, ambako Lautaro Martinez pia alifunga.

Lukaku amekuwa nyota tangu alipotua hapo akitokea Manchester United, ambako alifunga mabao 12 kwenye Ligi Kuu katika mechi 32 msimu uliopita.

"Nimesikia watu wanasema Lukaku alikuwa punda. Nimesikia mengi kwa muda mwingi! Ni rahisi kuzungumzia jinsi Lukaku anavyopaa kwa sasa," amesema Conte.

"Mara zote nilisema Romelu alikuwa almasi chafu ambayo ilihitaji kusafishwa. Lautaro Martinez hivyo hivyo. Hawa ndio kwanza wana umri wa miaka 26 na 22, bado vijana wadogo.

# De Rossi aondoka Boca Juniors

**BUENOS AIRES,** Argentina

DANIELE De Rossi ameamua kuondoka Boca Juniors na kustaafu kucheza soka la ushindani.

Boca walimsajili De Rossi akiwa mchezaji huru Julai mwaka jana baada ya mkataba wake na AS Roma kumalizika, akiwa amecheza kikosi cha kwanza kwa misimu 18.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 36 alianza kuifungia timu hiyo ya jiji la Buenos Aires kwenye mchezo wa Copa Argentina wakati wakiibuka na ushindi dhidi ya Almagro, lakini alicheza mechi sita tu.

Hata hivyo, De Rossi amevunja mkataba wake na Boca na atarudi Italia ili kuwa karibu na familia yake.

De Rossi aliichezea Roma mechi 616, akiwa ni wa pili kwa kucheza mechi nyingi, huku akiwa amepitwa na na gwiji wa klabu hiyo, Francesco Totti, wakati Timu ya Taifa ya Italia ameichezea mechi 117 akishinda Kombe la Dunia mwaka 2006.

Akielezea uamuzi wake wa kustaafu soka wakati akizungumza na waandishi wa habari Jumatatu, De Rossi alisema: "Hakuna mtu yoyote kwenye familia yangu ambaye ana matatizo ya kiafya. Nataka kufafanua hilo kutoka na vitu vinavyozungumzwa kwenye vyombo vya habari.

"Nahitaji tu kuwa karibu na binti yangu, na familia yangu. Hicho ndio kitu pekee, na hasa ikizingatia umri wangu pia. Nina miaka 36, ni wakati muafaka wa kupumzika sasa. Kama ningekuwa na miaka 25, mambo yangekuwa tofauti.

"Sikuwa na tatizo na watendaji au makamu wa raia wa Boca, (Juan Roman) Riquelme au mtu yoyote. Walinihudumia kwa upendo; wameelewa maamuzi yangu."




# ERIKSEN AKATALIWA INTER MILAN




**MILAN,** Italia

KIUNGO wa Tottenham, Christian Eriksen amekuwa akihusishwa kwa muda mrefu na kumpango wa kutua Inter Milan, lakini Giuseppe Marotta amesisitiza hawajafanya mawasiliano yoyote kati ya klabu hizo mbili.

Mkataba wa Eriksen na Spurs utamalizika mwishoni mwa msimu, lakini imeripotiwa kwamba Inter ipo tayari kulipa euro milioni 20 na kumsajili kipindi hiki cha dirisha la Januari

Kiungo wa Barcelona, Arturo Vidal pia inaeleweka kwamba anawaniwa na Nerazzurri hao na Ofisa Mtendaji Marotta amethibitisha wanampango wa kuongeza kiungo na winga wakati huu wa dirisha dogo la usajili.

Hata hivyo, Marotta alikanusha madai kwamba Spurs wapo kwenye mazungumzo na mchezaji huyo wa kimataifa wa Denmark.

"Inter mara zote inahusishwa na wachezaji wenye ubora na hatuna tatizo na hilo, lakini hatuna mawasiliano yoyote na Tottenham," alisema akiambia Sky Sport Italia.

"Eriksen ni mchezaji mwenye kipaji, sihitaji kuzungumza kuhusu hilo, na atakuwa mchezaji huru Juni mwaka huu.

"Nafikiri klabu nyingine zinamtaka, ni mchezaji anayevutia, lakini siwezi kusimama na kuwaambia kwamba tupo kwenye mazungumzo na klabu yake au wakala wake."

Alipoulizwa kuhusu Vidal, Marotta alisema: "Tupo kwenye mawasiliano na mawakala kadhaa na klabu kwa ajili ya kuongeza ubora wa kikosi chetu."

# *Haaland: Dortmund ilinishawishi*

**DORTMUND,** Ujerumani

ERLING Haaland amesema mipango ya Borussia Dortmund "ilimshawishi" yeye kuchagua kujiunga na kikosi hicho cha Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, badala ya miamba wa Ligi Kuu England, Manchester United.

Mshambuliaji huyo kinda wa kimataifa wa Norway, Haaland amesaini mkataba wa miaka minne na nusu na Dortmund, licha ya kutakiwa zaidi na United, RB Leipzig na Juventus, zilikuwa miongoni mwa klabu zilizokuwa zinawania saini ya Haaland - ambaye alifunga mabao 28 katika mechi 22 alizochezea Salzburg kwenye mashindano yote msimu huu.

Haaland alibainisha kwanini aliamua kujiunga na Dortmund, huku 'dogo' huyo mwenye umri wa miaka 19 akisema: "Walikuja na kuniambia kwa uwazi kabisa 'tunakuhitaji mbele, tunapenda staili yako ya uchezaji na tunataka kuwa na wewe'.

"Nilipenda namna walivyozungumza na mimi na ndio maana nilishawishika kusaini kwao. Nilihisi tu kuwa mimi na Dortmund tutakuwa na muunganiko mzuri."

Haaland alijiunga na Dortmund iliyopo nafasi ya nne kwenye msimamo wa Bundesliga ikipitwa pointi saba na vinara Leipzig baada ya mechi 17.

"Nimekutana na watu wazuri hapa kwenye mazoezi na nitaona kama nitacheza zaidi, hatua kwa hatua," amesema Haaland.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SAFARI YA SAMATTA ENGLAND YAKARIBIA

●●● Ni baada ya klabu tatu za EPL kuonyesha nia ya kumsajili nahodha huyo wa Stars...

**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Simba, Mbwana Samatta huenda akawa Mtanzania wa kwanza kucheza katika Ligi Kuu England endapo mchakato wa kuhamia kwenye ligi hiyo utakamilika.

**Klabu tatu zinazoshiriki Ligi Kuu England ambazo ni pamoja na Brighton, Crystal Palace na Norwich zimeonyesha nia ya kumsajili mshambuliaji huyo anayeichezea klabu ya Ligi Kuu Ubelgiji, Genk katika kipindi cha dirisha dogo la Januari.**

Imeelezwa kuwa ada ya kuvunja mkataba wa Samatta, ambaye aliifungia Genk bao pekee katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Liverpool katika mechi iliyochezwa Novemba, mwaka jana ni pauni milioni 10.

Mkataba wa mshambuliaji huyo wa zamani wa African Lyon ya Dar es Salaam, Tanzania unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu ujao.

Imebainika kuwa klabu hiyo tatu zinaendelea kufanya mazungumzo ya karibu na meneja wa mshambuliaji huyo ili kuhakikisha inanasa saini yake.

Samatta alitua Genk mwaka 2016, akitokea TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), na nyota huyo mwenye umri wa miaka 27 alikuwa Mfungaji Bora wa Ligi Kuu Ubelgiji na kuwa mchezaji wa kwanza kutoka Afrika Mashariki kushinda tuzo ya Soulier d'ébène, ambayo hutolewa kwa nyota wa Afrika aliyefanya vema kwenye ligi hiyo.

Eintracht Frankfurt na Lazio pia nazo zimetajwa kuonyesha nia ya kumsajili Samatta katika dirisha dogo la Januari, ingawa zinaamini mshambuliaji huyo anapendelea kutua kwenye ligi ambazo zinafuatiliwa kwa karibu na Watanzania.

Brighton ndiyo inaonekana kuwa mbele katika mbio za kuwania saini ya Samatta, huku Kocha wake, Graham Potter, akitaka kuimarisha safu yake ya ushambuliaji kufuatia kuwapo kwa tetesi za Neal Maupay kutakiwa na Aston Villa wakati Newcastle ikimwinda, Glenn Murray (36).

Norwich yenyewe pia inamtaka nahodha huyo wa Taifa Stars ili kuungana na mshambuliaji kinara wa timu hiyo, Teemu Pukki, ili kujinusuru na janga la kushuka daraja wakati wa kukosekana kwa huduma ya Christian Benteke, ambaye ni majeruhi inamaanisha kuwa Palace inatakiwa kuing'oa sokoni kusaka mshambuliaji mpya atakayeisaidia timu hiyo.

## ZISIKUPITE

### LEMAR ATAKIA SPURS

TOTTENHAM inajipanga kumsajili kwa mkopo kiungo wa Atletico Madrid na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Thomas Lemar (24), huku pia ikijiandaa kutoa dau la pauni milioni 51 ili kumnunua hapo baadaye. ***(Independent)***

### UTD, CITY ZAMGOMBEA WINKS

KIUNGO wa Tottenham na Timu ya Taifa ya England, Harry Winks, ambaye ana umri wa miaka 23, anatajwa kuwindwa na Manchester City pamoja na Manchester United. ***(Athletic, via Mirror)***

### CHELSEA, UNITED VITANI

CHELSEA na Manchester United zimefanya mawasiliano na straika wa Paris St-Germain na Timu ya Taifa ya Uruguay, Edinson Cavani (32), ambaye anaamini anakaribia kukamilisha mchakato kujiunga na Atletico Madrid, katika dirisha dogo la Januari. ***(L'Equipe, via Sun)***

### SKRINIAR ATAKIWA CITY

MANCHESTER City imeweka wazi nia yake ya kusaka saini ya beki wa Inter Milan na Timu ya Taifa ya Slovakia, Milan Skriniar (24), ambaye anatajwa pia kuwindwa na klabu za Barcelona na Real Madrid. ***(Mirror)***

### CONTE AMTAJA VIDAL

INTER Milan imewasilisha ofa ya pauni milioni 20 ili kunasa saini ya kiungo wa Tottenham na Timu ya Taifa ya Denmark, Christian Eriksen (27), lakini Kocha Antonio Conte anapendelea kuona klabu yake inamsajili kiungo wa Barcelona, Arturo Vidal (32). ***(Mirror)***

### MILAN YAMWANIA GIROUD

INTER Milan inaongoza katika vita ya kuwania saini ya mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Olivier Giroud (33), ambaye anawania na Aston Villa pamoja na Newcastle United. ***(Telegraph)***

### AUBAMEYANG: SIONDOKI

STRAIKA wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang (30), anahusishwa na mipango ya kuondoka Gunners lakini nyota huyo na Timu ya Taifa ya Gabon amesema kuwa bado anahitaji kuitumikia klabu hiyo. ***(Mail)***

### UNITED YAMWAZA MADDISON

MANCHESTER United imesema inafahamu mchakato wa kumnasa kiungo wa Leicester City, James Maddison (23), katika dirisha dogo la Januari ni mgumu, lakini itaendelea zoezi hilo. ***(Sky Sports)***

### FOFANA ANUKIA EVERTON

EVERTON imeingia kwenye vita ya kuwania saini ya beki Mfaransa wa St Etienne, Wesley Fofana, ambaye ana umri wa miaka 19, na anawindwa na klabu mbalimbali za Ulaya. ***(Star)***

### MODRIC KUTUA MAREKANI

KIUNGO wa Real Madrid na Croatia, Luka Modric (34), yuko kwenye mazungumzo na klabu ya DC United inayoshiriki Ligi Kuu Marekani, klabu ambayo aliichezea Wayne Rooney. ***(The Athletic - subscription required)***

### CAKIR ATAJWA LIVERPOOL

LIVERPOOL imewasilisha ofa ya kumwania golikipa wa Trabzonspor na Timu ya Taifa ya Uturuki, Ugurcan Cakir. ***(Metro)***

# Azam, Mtibwa zasonga mbele

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MABINGWA watetezi wa mashindano ya Kombe la Mapinduzi, Azam FC na Mtibwa Sugar zimefanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo inayoendelea visiwani hapa.

Azam imesonga mbele baada ya kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Mlandege katika mchezo uliochezwa juzi usiku kwenye Uwanja wa Amaan, shukrani kwa Mzambia Obrey Chirwa aliyefunga goli hilo dakika ya 56.

Akizungumzia baada ya mechi hiyo kumalizika, Kocha Msaidizi wa Azam, Iddi Cheche, alisema licha ya kupata ushindi huo, mchezo huo ulikuwa mgumu kutokana na mtindo unaochezwa katika mashindano ya mwaka huu.

Cheche alisema mtindo wa mtoano huzifanya timu kucheza kwa kutumia nguvu kubwa, ili kuhakikisha haipotezi mchezo na kusonga mbele katika kinyang'anyiro hicho.

Aidha, alisema wachezaji walijituma ili kuhakikisha wanafikia lile lengo la kusonga mbele katika michuano hii na hata kutetea ubingwa wake. Naye Kocha Mkuu wa Mlandege, Sheha Khamis, alisema timu yake ilicheza vizuri na ilitengeneza nafasi nyingi na nzuri kuliko wapinzani wake, lakini tatizo lilikuwa katika umaliziaji.

Khamis alisema wachezaji walijitahidi katika kushambulia lakini hawakuwa bahati, huku Azam wakiitumia vema nafasi waliyoipata na kufunga bao lililowapa ushindi katika mchezo huo.

Mtibwa Sugar yenyewe ilisonga mbele baada ya kuifunga Chipukizi penalti 4-2 baada ya dakika 90 za kawaida kukamilika wakiwa sare ya bao 1-1.

# Yanga Princess, JKT hapatoshi

**Na Mwandishi Wetu**

LIGI Kuu ya Wanawake Tanzania inatarajia kuendelea kwa Yanga Princess kuwakaribisha mabingwa watetezi JKT Queens katika mechi itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Karume jijini Dar es Salaam.

Yanga Princess itashuka uwanjani leo ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya Panama Queens wakati JKT Queens yenyewe ililazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Ruvuma Queens.

Nahodha wa JKQ Queens, Asha Rashid, alisema jana wamejiandaa kupambana kuhakikisha wanashinda na kuendelea kufufua matumaini ya kutetea taji wanalolishikilia.

"Tumejiandaa vizuri kuelekea mchezo wa leo, msimu huu ligi imekuwa ngumu, lakini tunaahidi kupambana kupata ushindi,'' alisema nahodha wa JKT Queens, Asha Rashid.

Alliance Queens ya jijini Mwanza ndiyo inaongoza katika msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 19 ikifuatiwa na Simba Queens yenye pointi 14, huku JKT Queens wenye pointi 13 wakiwa ya tatu.

# KATWILA AMULIKA REKODI KUBWA MAPINDUZI CUP

**Na Isaac Kijoti,** ZANZIBAR

HUKU timu yake ikifanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali ya Kombe la Mapinduzi, Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, amesema anataka kuandika rekodi ya kulitwaa kombe la michuano hiyo, kwa mara ya pili akiwa kocha baada ya kufanya hivyo wakati akiwa mchezaji.

**Akizungumza na waandishi wa habari kisiwani hapa, Katwila alisema amefurahi kuona Mtibwa Sugar imepata nafasi ya kushiriki michuano hiyo mwaka huu, baada ya kutoshirikishwa kwa muda sasa.**

Katwila alisema mara ya kwanza kwake kushiriki michuano hiyo alikuwa mchezaji na walifanikiwa kulibeba kombe hilo, jambo ambalo atafurahi kama atalitwaa akiwa kocha.

"Hii ni mara yangu ya pili kuja hapa (Pemba), mara ya kwanza nilikuja kama mchezaji na tulitwaa ubingwa nitafurahi kuubeba sasa nikiwa kocha," alisema.

Juzi Mtibwa Sugar ilifanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali baada ya kuitoa Chipukizi kwa mikwaju ya penalti 4-2 kufuatia mechi kumalizika kwa sare ya bao 1-1 katika dakika 90 za kawaida.

Katika mchezo huo uliopigwa kwenye Uwanja wa Gombani kisiwani Pemba, Chipukizi ilikuwa ya kwanza kuliona lango la Mtibwa dakika ya tano kupitia kwa Suleiman Nassor.

Mtibwa ilibidi kusubiri hadi dakika ya 63 kabla ya Haroun Chanongo kuisawazishia na kufanya mechi hiyo kumalizika kwa sare ya bao 1-1 ndipo changamoto ya mikwaju ya penalti ilipochukua nafasi yake.

Katika changamoto ya mikwaju ya penalti kipa wa Mtibwa, Said Mohammed 'Nduda' aliibuka shujaa baada ya kucheza penalti mbili zilizosaidia kuipeleka timu yake nusu fainali.

Nduda alizicheza penalti ya Jumaa Kassim na Abdallah Mohamed wakati zilizozama kimyani zilikuwa za Salim Abdul na Abdullah Khalisan.

Wafungaji wa matuta ya Mtibwa walikuwa ni Omar Sultan, Abdulhalim Humuod, Riffat Khamis na Dickson Job.

Kwa matokeo hayo Mtibwa Sugar nusu fainali sasa itakutana na mshindi wa mechi kati ya Jamhuri na Yanga keshokutwa kwenye Uwanja wa Amaan.



Wachezaji wa timu ya kikapu ya wenye ulemavu ya Mkoa wa Dar es Salaam, wakifanya mazoezi kujiandaa na mashindano mbalimbali kwenye Uwanja wa Jakaya Mrisho Kikwete (JMK Park) jijini jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Tanzania yajipanga kuimaliza Burundi*

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Taifa ya wanawake wa umri chini ya miaka 17 inatarajia kuwakaribisha wenzao kutoka Burundi katika mchezo wa kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Dunia utakaochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Fainali za Kombe la Dunia kwa yosso hao zimepangwa kufanyika baadaye mwaka huu nchini India.

Timu hizo zilikutana kwenye mashindano ya Kombe la Chalenji Desemba mwaka jana na kutoka sare ya mabao 3-3, Burundi ikitoka nyuma na kurudisha magoli yote.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu timu ya Tanzania, Bakari Shime, alisema kikosi chake kinaendelea vizuri na mazoezi na anaamini mchezo huo utakuwa na ushindani kutokana na matokeo waliyopata walipokutana mjini Jinja, Uganda. Shime alisema kuwa kikosi chake hakina mchezaji majeruhi na kila nyota anaonekana kujipanga imara kuhakikisha wanaanza vema kampeni hiyo ya kuelekea India.

"Tuko salama, vijana wote wako salama, maandalizi yanaendelea vizuri, sisi tutakuwa wenyeji wa kwanza dhidi ya Burundi, tunaamini mchezo huu utakuwa na ushindani kutokana na ubora wa vikosi vyote viwili," alisema Shime.

Aliongeza kuwa baada ya maandalizi ya muda mrefu, watacheza kwa kujilinda na tahadhari katika mchezo huo ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

"Hii ni mechi nyingine, na mashindano mengine, vijana wamejifunza kutokana na makosa, benchi la ufundi pia limejifunza kutokana na mchezo wa kwanza, tunawaomba Watanzania waje kwa wingi uwanjani, kutushangilia, hatutawaangusha," Shime alisema.

# Michezo

Jumatano Januari 8, 2020

Nipashe




Safari ya Samatta England yakaribia HABARI UK.30



Winga wa Arsenal, Reiss Nelson (kulia), akifunga bao pekee huku kipa wa Leeds United, Illan Meslier akishindwa kuokoa shuti hilo katika mchezo wa Kombe la FA uliochezwa kwenye Uwanja wa Emirates juzi usiku. **PICHA: MTANDAO**

# *Simba, Azam FC kurudia fainali Mapinduzi ya 2019*

## ● ● ● Ni baada ya Bocco, Shiboub na Ajibu kuifanyia kitu mbaya Zimamoto katika Uwanja wa Gombani kwa...

**Na Isaac Kijoti,** ZANZIBAR

MARUDIO ya mechi ya fainali ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi itashuhudiwa tena Ijumaa wiki hii katika Uwanja wa Amaan mjini Unguja wakati Simba itakapokutana na Azam FC katika hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo.

**Mwaka jana katika michuano hiyo, timu hizo zilikutana fainali iliyopigwa kwenye Uwanja wa Gombani kisiwani Pemba na Azam kulibeba kombe hilo baada ya kushinda kwa mabao 2-1.**

Simba ambayo imefanikiwa kutinga nusu fainali baada ya kuichapa Zimamoto mabao 3-1 kwenye mechi iliyopigwa Uwanja Gombani, Pemba jana, itakutana na Azam iliyoitoa Mlandege kwa bao 1-0 juzi usiku.

Katika mechi ya jana, Zimamoto ilikuwa ya kwanza kufika langoni mwa Simba na jaribio lao la kwanza lilikuwa dakika ya nne kupitia kwa Ibrahim Hilika ambaye shuti lake lilichezwa na kipa Ally Salim.

Simba ambayo ilianza kwa mchezo wa taratibu, huku ikionekana kunufaika zaidi na ukubwa wa Uwanja wa Gombani kwa kucheza kwa kufunguka, ilifika langoni mwa Zimamoto kwa mara ya kwanza dakika ya tano na kuandika bao lake la kwanza. Ilikuwa ni 'gonga' nzuri iliyoanzia kwa Hassan Dilunga na kumpasia Ibrahim Ajibu ambaye alimmegea nahodha John Bocco aliyeuzamisha mpira kimyani.

Dakika tatu baadaye kona iliyochongwa na Ajibu iliunganishwa kwa kichwa na Kennedy Juma na kuchezwa na kipa Mwinyi Hassan 'Casilas' kabla ya kumkuta Sharaf Shiboub aliyeuzamisha nyavuni.

Uzembe wa Erasto Nyoni wa kushindwa kufanya uamuzi wa haraka ya kucheza mpira mrefu uliopigwa langoni mwao huku akimtegea Salim adake, ulileta madhara kufuatia Hilika kumzidi ujanja na kuuzamisha kimyani dakika ya 29.

Simba ingeweza kwenda mapumziko ikiwa mbele kwa mabao 3-1, lakini mwamuzi, Seif Kesi alilikataa bao la Ajibu huku wengi wakiamini angeweza kutoa penalti kufuatia Miraji Athumani kusukumwa ndani ya eneo la 18, lakini aliamuru faulo ipigwe kuelekea langoni mwa Wekundu wa Msimbazi hao.

Akionyesha ubora wake jana, kipindi cha pili Ajibu alimchambua vema beki wa Zimamoto na kuiandikia Simba bao la tatu kwa guu lake la kulia katika dakika ya 54 baada ya kupokea pasi kutoka kwa Shiboub.

Kwa matokeo hayo Simba sasa itakutana na Azam FC katika hatua ya nusu fainali itakayopigwa Ijumaa wakati Mtibwa Sugar iliyoitoa Chipukizi kwa mikwaju ya penalti 4-2 baada ya sare ya 1-1, ikikutana na mshindi wa mchezo wa jana usiku kati ya Yanga na Jamhuri katika Uwanja wa Amaan kesho.

# Mkwasa, Kahata wang'ara Bara

**Na Mwandishi Wetu**

KIUNGO mshambuliaji wa kimataifa wa Simba, Francis Kahata, amechaguliwa kuwa Mchezaji Bora wa Desemba wa Ligi Kuu ya Tanzania Bara msimu wa 2019/2020, imefahamika.

Kahata amepata tuzo hiyo baada ya kuwazidi pointi wachezaji wenzake wawili, kiungo wa Simba, Hassan Dilunga na beki tegemeo wa Coastal Union ya jijini Tanga na Timu ya Taifa (Taifa Stars), Bakari Mwanyeto.

Kiungo huyo aliyetua Simba akitokea kwa mabingwa wa Ligi Kuu Kenya, Gor Mahia, ameisaidia timu yake kuendeleza kasi ya ushindi na kujiimarisha katika msimamo wa Ligi Kuu ambayo huyo mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Naye Kocha Mkuu wa Yanga, Boniface Mkwasa, amechaguliwa kuwa Kocha Bora wa Desemba wa Ligi Kuu baada ya kuwashinda Juma Mgunda wa Coastal Union na Sven Vandenbroeck wa Simba. Mkwasa amekuwa na matokeo mazuri, tangu alipochukua mikoba ya Mkongomani Mwinyi Zahera, ikiwamo kuwa timu ya kwanza kuwafunga 'Maafande' wa Tanzania Prisons ambao walikuwa hawajapoteza mchezo hata mmoja msimu huu.

Kahata na Mkwasa, wataungana na washindi wengine kuwania tuzo ya mwaka itakayotolewa baada ya kumalizika kwa msimu huu wa 2019/20.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002